

KIPINDI 1: Barua ya Petro ya Kwanza: *Utangulizi (Sehemu ya Kwanza)* Steve Lancaster

Kwa vipindi hivi viwili vinavyofuata, ninataka tutumie muda, kuangalia historia ya barua hii, na ili tuweze kufanya hivi, nataka tulenge katika mistari miwili ya kwanza, ya barua hii – na mistari mitatu ya mwisho. Na ninataka nianze kwa kuuliza maswali sita: **Namba moja:** Je, nani aliandika barua hii? **Namba mbili:** lini iliandikwa? **Namba tatu:** wapi iliandikwa? **Namba nne:** Je, akina nani waliandikiwa barua hii? **Namba tano:** kwa nini barua hii iliandikwa? Na **namba sita:** Je, mawazo makuu ya barua hii ni nini? **1 Petro 1:1-2 & 1 Petro 5:12-13** **. Ngoja tuangalie swali la kwanza, na ninafikiri kwamba hili ni swali rahisi! Nani aliandika barua hii? Jibu lipo kwenye mstari wa kwanza: “*Petro, mtume wa Yesu Kristo*”. Inaonekana kwamba, huyu ni Petro yule yule, ambaye alikuwa mwanafunzi wa Yesu. Na wasomi wengi, kwa karne nyingi, wamekubaliana na jambo hili. Kwa kweli, katika Injili tunajifunza mambo mengi kuhusu Petro. Kwa hakika, tunajua zaidi kuhusu yeye, kuliko wanafunzi wengine. Je, tunajua nini? Tunajua kwamba alitambulishwa kwa Yesu, na ndugu yake Andrea. Na tunajua kwamba, wote walikuwa wanafunzi wa kwanza wa Yesu. Hata jina lake lilibadilishwa na Yesu, kutoka Simoni, kuwa Petro.

Tunajua kwamba Petro alikuwa mvuvi katika ziwa Galilaya. Kwa kweli, alizaliwa katika kijiji cha Bethsaida, karibu na ziwa Galilaya, lakini pia, tunajua kwamba aliishi katika mji wa Kapernaumu. Je, tunajuaje hili? Kwa sababu katika **Luka 8**, inasema hivi: “*Yesu akatoka kwenye sinagogi huko Kapernaumu, na akaenda nyumbani kwa Simoni Petro*”. Na kifungu hiki hiki pia, kinatuambia kwamba, huko ndiko Yesu alimponya mama mkwe wa Petro. Kwa hiyo, jambo hili linatuambia nini? Linatuambia kwamba Petro alikuwa ameo, alikuwa na mke, ingawa hatumjui jina lake. Katika **1 Wakorintho 9**, mtume Paulo anasema kwamba, wakati Petro alipokuwa anasafiri, na kuihubiri injili, mara kwa mara, alimchukua mke wake kwenda pamoja naye – walisafiri pamoja. Pia, tunajua kwamba Petro alikuwa rafiki wa karibu wa Yesu, kama Yakobo, na Yohana walivyokuwa. Inaonekana kwamba, watu hawa watatu walikuwa rafiki maalumu sana kwa Yesu. Wakati mwingine, Yesu aliwaambia kwenda naye, lakini aliwaacha wanafunzi wengine nyuma. Kwa mfano: katika nyumba ya Yairo, wakati Yesu alipomponya msichana mdogo, aliwaambia Petro, Yakobo, na Yohana, kwenda naye. Mfano mwingine: katika Bustani ya Gethsemani, Yesu aliwachukua watu watatu hawa pamoja naye, na aliwaambia kukesha.

Na pia, juu ya mlima ambapo sura ya Yesu ilibadilika, ambapo Musa na Eliya walionekana. Je, unakumbuka Petro alisema nini? Petro aliogopa, na alianza kuongea bila kufikiri! Alimwambia Yesu kuwa ingefaa, kujenga vibanda vitatu juu ya mlima! Luka anatuambia (**Luka 9:33**) kwamba, Petro hakujua alichokuwa anaongea! Petro alikuwa mtu ambaye mara kwa mara, alifungua mdomo wake, kabla ya kufikiri kitu cha kusema! Alikuwa mtu wa kuongozwa na hisia – na mara kwa mara, hii ilimweka kwenye matatizo. Huyu ndiye mtu, ambaye alimkemea Yesu, alipokuwa anasema kuhusu msalaba wake. Huyu ni mtu yule yule ambaye, mara tatu alikana kwamba hakumjua Yesu – lakini masaa machache kabla ya hapo, alikuwa amemwambia Yesu kwamba, asingemkana kamwe!

Huyu ni mwanafunzi yule yule, ambaye mara ya kwanza, hakutaka kumwacha Yesu amuoshe miguu yake, katika Chumba cha Juu. Huyu ndiye mtu, ambaye alivuta upanga wake, na kutaka kuwaua watu waliomkamata Yesu. Huyu ndiye mtu, aliyetembea juu ya maji, lakini baadaye akaogopa, alipouona upepo na mawimbi. Katika matukio mengi, Petro alisema mambo, ambayo hakumaanisha - na alifanya mambo, ambayo Yesu hakuyakubali. Lakini unakumbuka nini kilitokea, walipokuwa wanapata chakula cha asubuhi, juu ya ufukwe wa ziwa Galilaya? Tukio hili lilitokea wiki chache, baada ya Yesu kufufuka kutoka kwa wafu. Yesu alimuuliza mara tatu: “*Petro unanipenda*”? Petro alijibu kwa kusema: “*Ndiyo Bwana, unajua kwamba nakupenda*”.

Na Yesu alimsamehe kosa lake, la kumkana mara tatu, na akamchagua kuwa kiongozi katika kanisa la kwanza. Je, unajua – kwamba hii ni habari njema kwetu?! Tunajua kwamba Petro alifanya makosa mengi, na tunaposoma kuhusu yeye katika injili, mara kwa mara tunakumbushwa kuhusu sisi wenyewe. Tunajua kwamba sisi tuko kama Petro. Tunasema mambo, ambayo siyo sahihi. Tunafanya mambo yasiyo sahihi. Dakika moja tunasema kwamba tunampenda Mungu, lakini dakika moja mbele, tunamuasi. Sisi tuko tu kama Petro! Na pengine ndiyo maana, yeye ni mwanafunzi tunaye vutiwa naye sana! Ingawa Petro alishindwa na kufanya makosa mengi, bado Yesu alimsamehe, na kumpa nguvu za kuwa kiongozi wa kimungu katika kanisa la kwanza. Mungu ni mwema sana kwetu.

Kama tutatubu dhambi zetu kweli kweli - haijalishi makosa yetu ni makubwa kiasi gani, Mungu atatusamehe, kwa sababu ya kile ambacho Yesu alifanya msalabani. Anauwezo wa kutufanya upya, na anauwezo wa kututumia katika kazi ya ufalme wake, ni kama tu alivyofanya kwa Petro. Na uthibitisho wa jambo hili, tunaweza kuuona katika **Matendo 2** katika siku ya Pentekoste, majuma sita tu, baada ya Petro kumkana Yesu mara tatu. Roho Mtakatifu alimiminwa juu ya wanafunzi, na mkutano ulikusanyika kuona kilichokuwa kinatokea. Petro akasimama kwa ujasiri, na kuhubiri kwa makutano, na zaidi ya watu elfu tatu, wakaokoka, na kubatizwa! Hapa ni mtu aliyekuwa ameshindwa, lakini Yesu amemchagua, amemsamehe, na kumwezesha kuwa kiongozi mwenye nguvu sana, katika kanisa la kwanza. Kwa shukrani, tunamtumikia Mungu, ambaye ni mwema, na mwenye upendo.

“Petro, mtume wa Yesu Kristo”. Je, neno ‘*mtume*’ lina maana gani? Kwa Kiebrania lina maana ya ‘*mtu aliyetumwa*’. Kwa hiyo wanafunzi walikuwa ‘*wametumwa*’ na Yesu. Na jina hili ‘*mtume*’ walipewa wale wanafunzi kumi na wawili wa Yesu. Aliwachagua, na kuwatumia kwenda kuwa mashahidi wake – na Petro alikuwa mmoja wa wanafunzi hao. Neno ‘*mmisionari*’ pia linatokana na neno hili, ‘*mtume*’. Katika siku za nyuma, mmisionari ni mtu aliyetumwa kutoka nchi nyingine, kwenda kumshuhudia Kristo. Na kwa hiyo, barua ya Petro ingeanza kwa kusema hivi: *“Petro – mmisionari aliyetumwa na Yesu Kristo”*. Kwa hiyo, wasomi wengi wanaamini kwamba ni mtume Petro ndiye aliyeandika barua hii. Hata baada ya miaka mia nne baada ya Kristo, walimu wote maarufu wa Biblia, bado waliamini kwamba, mwandishi wa barua hii alikuwa Petro. Kwa hiyo kwa nini tunafikiri kwamba alikuwa Simoni Petro, na siyo Petro mwingine? Kuna ushahidi mwingi katika barua. Fungua **1 Petro 5:1**. Tunajua kwamba mtume Petro alikuwa mzee, au mchungaji, katika kanisa la kwanza - na tunajua kwamba Petro alimwona Yesu akiteseka. Aliona kilichotokea.

Pia kuna mstari mwingine katika sura ya pili, ambao unapendekeza kwamba mwandishi wa barua hii, alikuwepo wakati Yesu anahojiwa. Fungua **1 Petro 2:23**. Mwandishi anaweza kusema: *‘nili kuwa pale wakati Yesu anahojiwa. Niliyaona mambo haya yakitokea’*. Na tunajua kwamba, baada ya Yesu kukamatwa, Petro aliwafuata maaskari katika uwanja wa Kuhani Mkuu, na alishuhudia mambo haya. Hebu fungua tena **1 Petro 5:13**. Tuli soma hapo nyuma. Na hii ni sababu nyingine ya kutufanya tufikiri kwamba mwandishi wa barua hii, alikuwa mtume Petro: *“Mwenzenu mteule hapa Babeli awasalimu, na Marko mwanangu”*. Je, huyu ni Marko yupi? Siyo mwanaye wa kimwili – lakini inawezekana ni Marko yule yule, ambaye aliandika mojawapo ya injili. Tangu siku za kanisa la kwanza, watu wamewajua Petro na Marko, kuwa walikuwa rafiki wa karibu. Kwa kweli, wasomi wengi wanafikiri kwamba, Petro alihusika kumfanya Marko awe Mkristo - na kwa hiyo, Marko alikuwa mtoto wa kiroho wa Petro. Na pia inadhaniwa kwamba, Marko alipoandika injili yake, alipata taarifa zake nyingi, kutoka kwa mtume Petro – ni kweli. Kwa hiyo, ushahidi huu wote unamwonesha mtume Petro kuwa mwandishi wa barua hii.

KIPINDI 2: Barua ya Petro ya Kwanza: *Utangulizi (Sehemu ya Pili)* Steve Lancaster

Maswali mawili yanayofuata, ambayo ninataka tuyaangalie ni: *barua iliandikwa lini?* na *wapi iliandikwa?* Na kwa sababu maswali haya yako pamoja, tutayaangalia pamoja. Na sitatumia muda mwingi, katika maswali haya. Kwa upande mwingine siyo kitu cha muhimu, kujua wapi na lini, kitabu kiliandikwa; taarifa hizo haziongezi kitu chochote katika kifungu. Lakini, kwa upande mwingine, inavutia kujifunza kuhusu historia ya barua. Fungua **1 Petro 5:13**. Tuliangalia mstari huu wakati tunaangalia uhusiano kati ya Petro, na Marko, lakini mstari huu pia, unasema kitu fulani kuhusu wapi barua iliandikwa. “*Mwenzenu mteule hapa Babeli awasalimu*”. Petro anahitimisha barua yake, na anataka kutuma salamu, kutoka kwa kanisa ambalo anahudumia. Katika makanisa yetu leo, ni kawaida kwa wageni kusimama, na kujitambulisha wenyewe. Na mara kwa mara, huwa wanaleta salamu kutoka kwa makanisa yao. Hiki ndicho anachofanya Petro hapa. Anasema, ninawaletea salamu kutoka kwa Wakristo wa hapa Babeli.

Kwa hiyo, ingeonekana kwamba, Petro anaandika kutoka Babeli. Lakini, kuna mjadala fulani hapa. Babeli – kweli? Tunajua kwamba Wayahudi wa Yerusalemu, walikuwa utumwani Babeli, karibu miaka mia sita kabla ya Yesu – na unaweza kusoma jambo hili, katika kitabu cha Wafalme wa Pili, na Mambo ya Nyakati ya Pili. Mfalme Nebukadneza alikuwa kiongozi wa Babeli, na alitawala ufalme wenye nguvu sana, kwa kipindi hicho. Lakini Petro alipokuwa hai, Babeli ilikuwa imeharibiwa, na ilikuwa imebaki kijiji kidogo tu. Kwa kweli, ilijulikana kwamba, mji mkuu ulikuwa umegeuka jangwa! Kwa hiyo – kwa nini Petro angeishi Babeli kwa kipindi hicho? Katika Agano Jipya, hatuna kumbukumbu ya Petro kutembelea Babeli. Kwa hiyo, kwa nini anasema kwamba “*kwa wale walioko Babeli wanatuma salamu zao*”? Kwa kweli halleti maana kabisa.

Baadhi ya wasomi wanafikiri kwamba, Petro anatumia jina ‘*Babeli*’ kwa ajili ya kutaja jiji la Roma, katika Italia. Na kuna baadhi ya ushahidi ambao unaonesha kwamba, Babeli lilikuwa jina la utani kwa ajili ya jiji la Roma. Kwa kweli unaposoma kitabu cha Ufunuo, Yohana anatumia jina ‘*Babeli*’ mara nyingi - na wasomi wa Biblia wanafikiri kwamba, anatumia jina ‘*Babeli*’ kutaja jiji la Roma. Na katika baadhi ya matoleo ya Biblia, unaposoma katika 1 Petro 5:13 kwa kweli inasema ‘*Roma*’, badala ya ‘*Babeli*’. Wengi wa wasomi wa Biblia wa kanisa la mwanzo; watu kama Eusebius, ambaye aliishi miaka mia mbili baada ya Petro, anasema kwamba, Petro aliandika barua hii kutoka Roma.

Sasa, hakuna kitu chochote katika Agano Jipya, ambacho kinatuambia kwamba Petro alienda Roma, lakini historia ya kanisa inatuambia kwamba, alijihusisha na kanisa huko katika kipindi fulani. Na pia tunajua kutoka kumbukumbu za kihistoria kwamba, Petro aliuawa huko Roma, na mfalme wa Kiroma aliyelitwa Nero, yapata mwaka sitini na tano, baada ya Kristo kuzaliwa. Kulikuwa na mateso mengi kwa Wakristo, kwa wakati huo, na inaonekana kwamba, Petro alisulubiwa na Waroma kwa sababu ya imani yake katika Kristo.

Wanahistoria wengi pia wanasema kwamba, Petro aliomba kusulubiwa kichwa chini miguu juu! Hakujisikia kusulubiwa kwa namna ile ile, aliyosulubiwa Yesu. Hatujui jambo hili kwa uhakika, lakini hivi ndivyo kanisa la Roman Katholoki linavyosema. Kwa hiyo, kwa kuhitimisha, inawezekana kwamba barua hii iliandikwa katika Roma - ingawa tunaweza kutaka kumuuliza Petro: ‘*kama uliandika katika Roma, kwa nini hukutaja Roma, badala ya Babeli*?!’ Kwa kurejea tarehe ya barua hii, wasomi wengi wanasema kwamba, iliandikwa yapata mwaka sitini na tatu, baada ya Kristo kuzaliwa.

Kwa hiyo sasa, tufungue Biblia zetu, ili tuone nani aliandikiwa barua hii. **1 Petro 1:1** “*Kwa wateule wa utawanyiko, wakaao hali ya ugeni katika Ponto, Galatia, Kapadokia, Asia, na Bithinia*”. Katika notsi zako, utaona ramani inayokuonesha maeneo haya yalipo. Kwa leo nchi hii inaitwa “**Uturuki**”, lakini katika siku za Agano Jipya, iliitwa Asia Ndogo. Tunajua kwamba Paulo alitumia muda mwingi, katika maeneo ya kusini mwa nchi hii; maeneo kama Derbe, Lystra, Kolosai na Efeso. Majina matano, ambayo yametajwa katika mstari wa kwanza, ni mikoa, au majimbo ya Asia Ndogo, ambayo ilikuwa sehemu ya Dola la Roma. Na kwa kweli, baadhi ya majina haya, yametajwa pia katika kitabu cha Matendo.

Katika siku ya Pentekoste, tunasoma kwamba kulikuwa na Wayahudi waliokaa Yerusalemu, ambao walikuwa “*wametoka kila taifa chini ya mbingu*” – na kisha, inataja nchi zote, na mikoa yote, ambako watu hao walikuwa wametoka. Katika kifungu hiki inatajwa Kapadokia, Ponto, na Asia. Kwa hiyo, tunajua kwamba katika siku hiyo, palikuwa na watu kutoka maeneo haya, ambao walikuwa wamesikia injili. Labda baadhi yao walikuwa Wakristo katika siku hiyo na kisha walirudi nyumbani kwao katika Asia Ndogo, na wakaanzisha makanisa huko walikoishi. Labda watu hawa walipokuwa Yerusalemu, walikutana na Petro uso kwa uso, na wakamwalika kwenda, na kuwatembelea katika nyumba zao katika mikoa hii. Wasomi wengi wanafikiri kwamba, Petro alitembelea maeneo haya, na kupanda makanisa huko, na ndiyo maana anawaandikia. Kama tukifikiri kuhusu mtume Paulo na huduma yake, alipoandika barua zake – aliwaandikia watu wasehemu, ambazo alikuwa amefanya kazi. Kwa hiyo, nafikiri tunaweza kusema kwa uhakika kwamba, Petro anapoandika barua hii, anayaandikia makanisa, na watu ambao anawajua kinaga ubaga. Ninafikiri alikuwa ametumia muda katika maeneo haya, akiwatia moyo Wakristo huko.

Kwa kweli, katika Agano Jipya, kwa mara yetu ya mwisho kumuona Petro, ni katika **Matendo** sura ya **kumi na tano** (AD50), wakati yupo Yerusalemu, akizungumza katika mkutano wa baraza maalumu la kanisa. Baada ya hapo, hatujui alifanya nini. Tunajua alikufa huko Roma (AD65) lakini inaamana kwamba kuna miaka kumi na tano, ambayo hatujui alichokuwa anafanya. Lakini wasomi wanasema kwamba alikuwa anafundisha, na kuhubiri, katika Yerusalemu, na pia katika maeneo haya ya kaskazini mwa Uturuki.

Na kwa hiyo, tunajua mahali ambako wasomaji walikuwa wanaishi. Lakini tunajua nini kuhusu wao? Katika mstari wa kwanza, na wa pili, Petro anawataja kama ‘*wateule*’ au ‘*waliochaguliwa*’. Pia anaatumia maneno haya haya katika sura ya pili, mstari wa tisa: “*Ninyi ni watu wateule*”. Na hii inarejea wasomaji wa barua hii - lakini pia kwa kila mmoja ambaye ni muamini wa kweli katika Kristo. Kumbuka hili – kama wewe ni muamini, umechaguliwa na Mungu! Na hili ni neno muhimu sana kwetu. Tutakapoangalia sura ya pili kesho, tutatumia muda zaidi, kuangalia maana ya kuchaguliwa na Mungu.

Lakini kirai cha pili, ambacho Petro anatumia, katika mstari wa kwanza ni “*utawanyiko, wakaao hali ya ugeni*”. Hivi ndivyo inavyosema, katika toleo la Union. Hii inamaana gani? Biblia Habari Njema inatumia neno ‘*wakimbizi*’. Kirai “*utawanyiko*” ni kirai, ambacho kilitumika kuelezea kilichokuwa kinatokea kwa Wayahudi katika utumwa huko Babeli, mwaka mia tano themanini na saba, kabla ya Kristo. Je, kitu gani kilitokea katika mwaka huo? Tumekwisha kutaja jina lake asubuhi hii. Mfalme Nebukadnezar alivamia Israeli, akaliharibu hekalu katika Yerusalemu, na kuwapeleka Waisraeli Babeli na maeneo mengine. Wayahudi walikuwa wametawanyika; walipelekwa mbali na nchi yao; katika nchi ya ugeni; sehemu ambako walikuwa wakimbizi.

Na katika kipindi cha karne nyingi kila mara Wayahudi walipotaka kuwa huru; kila walipolazimishwa kuishi katika nchi zingine, waliita jambo hili ‘*utawanyiko*’. Walikuwa wakimbizi wakiishi katika nchi

zingine. Ni watu wa *'utawanyiko'*. Unaweza kukumbuka mwanzoni kabisa mwa Biblia katika kitabu cha Mwanzo, Mungu alimwita Abrahamu (hakuwa Myahudi), kutoka katika nchi yake aliyozaliwa, na kwenda katika nchi nyingine. Alitii, na kwenda Kanaani, au Israeli. Tunajua vizuri hadithi hii. Baada ya kifo cha mke wake, Sara alisema hivi kwa Wahiti: *"Mimi ni mgeni, na mkimbizi kati yenu"* (**Mwanzo 23:4**).

Kwa maneno mengine, Abrahamu hakuwa amezaliwa Kanaani. Hakuwa wa huko. Alikuwa mkaaji wa muda, akishi mbali na nchi yake. Kirai hiki pia, kinanielezea mimi! Nilizaliwa Uingereza lakini kwa sasa, ninaishi hapa Tanzania kwa muda fulani. Na katika pasporti yangu, nina kibali cha kuishi ambacho kinasema nimeruhusiwa kuishi hapa, kwa miaka miwili, na baada ya muda huo kuisha, nitahitaji kuomba tena. Mimi ni mkaaji wa Tanzania, lakini siyo raia wa Tanzania. Mimi ni mgeni – mimi siyo wa hapa. Hii siyo nchi yangu. Mimi siyo mwenyeji hapa. Ni mkaaji wa muda ninayeishi mbali na nchi yangu.

Katika Agano Jipya, pia tunaweza kuona kirai hiki. Je, unakumbuka kifungu katika Kitabu cha Waebrania kinachozungumza kuhusu mashujaa wa imani? Kuna orodha ya watu, walioishi kwa imani: Abrahamu, Nuhu, Henoko, Isaka, Yakobo, na Habili, na wengine wengi. Fungua **Waebrania 11:13**. Lakini tambua kwamba, kuna kitu fulani cha tofauti hapa, tunapolinganisha na kile ambacho Abrahamu alisema. Watu hawa katika sura hii ya Waebrania, hawasemi kuwa ni wakimbizi katika Israeli - lakini wanajitaja wao wenyewe kama wageni, na wakiimbizi, hapa duniani.

Sifikiri kama toleo la Union linatumia neno *'dunia'*, lakini matoleo mengi yanatumia neno *'dunia'*. Watu hawa katika Kitabu cha Waebrania, hawakuwa wanasema kuhusu kuwa watu wa nchi fulani. Hawasemi kuhusu utawanyiko wa Wayahudi. Ngoja nisome **Waebrania 11:16**, na hii itakuonesha kile ambacho walikuwa wanafikiri. *"Walikuwa waki-tarajia nchi bora zaidi; mbinguni"*. Je, hii inamaana gani? Kwa watu hawa wa Mungu, hawakujisikia kuwa ni wa hapa duniani, hata katika nchi waliyozaliwa. Waliamini kwamba, nyumba yao ya kweli ilikuwa mbinguni. Walijisikia kama wakimbizi, hata katika nchi zao, kwa sababu nyumba yao ya kweli; yaani nyumba yao ya kiroho, ilikuwa mbinguni. Na hiki ndicho anachosema Petro katika mstari wa kwanza, anapowaita wasomaji wake kuwa watu wa *'utawanyiko'* au wageni, au wakimbizi.

Baadhi ya watu katika mikoa hii, walikuwa Wayahudi. Baadhi yao katika ma kanisa haya, walikuwa watu wa mataifa – kwa hiyo, kulikuwa na mchanganyiko mkubwa wa watu, katika makanisa haya. Baadhi ya watu katika makanisa haya, walikuwa hata wametoka Yerusalemu, katika kipindi cha utawanyiko wa Wakristo, baada ya kifo cha Stefano. Kilikuwa kipindi cha mateso makubwa, na Wakristo wengi waliondoka Israeli kwa sababu ya mateso yaliyoongozwa na mamlaka ya Wayahudi dhidi ya kanisa. Na Petro anawaita watu hawa *'wakimbizi katika dunia'*, ingawa baadhi yao katika makanisa haya, waliishi maisha yao yote katika maeneo haya.

Petro anazungumzia ukweli kwamba, kama Wakristo, sisi sote ni wakimbizi hapa duniani. Hatufai kuwa ndani ya dunia, pamoja na watu wadunia hii. Sisi ni watu tofauti, kwa sababu tuna Roho Mtakatifu ndani yetu. Na tuko tofauti kwa sababu, nyumba yetu ya milele ni mbinguni. Kwa wale wasio Wakristo, makao yao ni hapa duniani, basi wanapokufa, kwa huzuni makao yao yatakuwa jehamu. Lakini, kwetu sisi waamini, tuna makao mengine ambayo tunayatarajia.

Kwa kweli Petro anatumia kirai hiki tena, katika barua hii. Angalia **sura 2: 11**. Anasema: *"Wapenzi, nawasahi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili"*. Petro anasema, kama Wakristo, tunahitaji kuwa watu tofauti. Tusienende kama watu wasio Wakristo, kwa sababu sisi ni watu wa ufalme mwingine. Kwa watu wengine, mtu anapokuwa Mkristo, maisha yake yanabadilika sana.

Tabia zao zinabadilika. Wanaacha kufanya walichokuwa wanafanya mwanzoni, na wanaanza kuishi kwa ajili ya Kristo. Na hata wanajisikia kwamba wao siyo wa hapa duniani tena. Je, huwa unajisikia hivi? Ninaporudi nyumbani Uingereza, ninaona jinsi watu wanavyo-enenda. Watu wengi wanampuuza Mungu. Hawana muda wowote kwa ajili yake. Na sheria zinazotengenezwa na serikali siyo za Kikristo. Kwa hiyo, hata katika nchi yangu, huwa ninajisikia kama mgeni, na mkimbizi! Najisikia kama siyo wa huko. Kwa nini? Kwa sababu mimi ni mtoto wa Mungu, na katika maana ya kiroho, mimi ni wa mbinguni, na siyo wa duniani. Na hivi ndivyo Petro anavyowaandikia wasomaji wake, katika Asia Ndogo. Kwa wateule; kwa wakimbizi katika dunia hii; kwa wale msio jisikia kuwa ni wa hapa duniani, *“Neema na amani iwe kwenu kwa wingi”*.

Maswali mawili ya mwisho, tunaweza kuyajibu kwa pamoja, kwa sababu yameunganika. Je, kwa nini barua hii iliandikwa, na mawazo makuu ya barua hii ni nini? Kwa maneno mengine, nini tutakuwa tunajifunza katika hizi siku tatu zijazo? Barua ya Kwanza ya Petro ni barua fupi; kuna sura tano tu, na jumla ya mistari mia moja na tano tu. Kwa hiyo, hii siyo barua kubwa – lakini ingawa ni ndogo, inataja mafundisho mbali mbali, na mambo mengi ya kusema kuhusu maisha ya Kikristo, na wajibu wa Kikristo. Baadhi ya wasomi wa Biblia wanasema kwamba, barua hii ni msingi wa mafundisho, ambayo Petro aliwapa Wakristo wapya walipokuwa wanabatizwa - na ninafikiri inawezekana kuwa hivyo. Kwa mfano: sura ya kwanza, mstari wa ishirini na mbili, unasema kwamba: *“Mkiisha kujitakasa roho zenu, kwa kuitii kweli”*. Inaashiria kwamba, watu hawa ndiyo wanaanza safari ya maisha yao ya kiroho. Mfano mwingine: **sura 2:2**. Hapa tena, inashiria kwamba, ndiyo wanaanza safari ya maisha yao ya kiroho – ni kama watoto wadogo.

Mfano mwingine: Katika sura ya tatu, Petro anazungumza kuhusu Nuhu na watu wa familia yake, ambao waliokoka na gharika. Anasema katika mstari wa ishirini na moja, kwamba: *“waliokoka kwa maji”*. Kisha anaongeza, *“mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi”*. Kwa hiyo, Petro anataja ubatizo na utakaso, na anazungumza kuhusu kukua katika imani kama watoto wadogo – kwa hiyo barua hii ingeweza kuwa barua ya mafundisho kwa ajili ya watu, ambao wamebatizwa hivi karibuni – lakini hatujui kwa uhakika.

Lakini hebu tufungue tena katika **sura 5:12**, kwa sababu Petro mwenyewe, anatuambia kwa nini aliandika barua hii. Na nitasoma mstari huu kutoka toleo la New Living Translation, kwa sababu liko wazi sana. *“Lengo langu katika kuwaandikia ni kuwatia moyo ninyi, na kuwapa uhakika kwamba, neema ya Mungu iko pamoja nanyi, bila kujali nini kinatokea”*. Hii inaonekana kuwa wazi sana – siyo? Niliandika barua hii ili kuwatia moyo na kuwapa uhakika.

Petro anataka kuwatia moyo. Anataka kupanua ufahamu wa imani ya Kikristo, ndiyo maana anazungumza kuhusu msalaba, wokovu, tumaini, imani, na neema ya Mungu. Anaandika kuhusu wokovu wa mtu binafsi – inamaana gani kwa mtu kuokoka, lakini pia anatumkumbusha kwamba, pia tumeokolewa kwa kuwekwa ndani ya familia ya Mungu. Katika sura ya pili anasema kwamba, sisi ni mawe yaliyo hai, na tumejengwa pamoja katika hekalu la kiroho. Anasema kwamba, sisi ni watu wa taifa takatifu, wateule wa Mungu. Na huu ni ukumbusho kwetu kwamba, ingawa wokovu ni wa mtu binafsi, pia ni kitu tunachofanya pamoja. Tunamilikiwa katika mwili wa waamini, yaani kanisa, na tunapaswa kufanya bidii katika wokovu wetu, na kukua katika Kristo, kadri tunavyokutana pamoja.

Mojawapo ya mawazo makuu, katika barua hii, ni somo la *‘mateso’*. Na unapoisoma barua hii, utaona kwamba, somo hili limetajwa mara nyingi. Kwa kweli, neno *‘mateso’* limetumika mara kumi na saba katika barua hii. Kumbuka, Petro yawezekana anaandika barua hii kutoka Roma – na anapoandika barua hii, anafahamu kwamba, mateso ya Wakristo yanatokea zaidi na zaidi;

yanafanywa na Wayahudi, na Warumi pia. Wafalme wa Roma walikuwa na wasiwasi na Wakristo, na tunahitaji kukumbuka kwamba, Ukristo ulikuwa dini mpya, ambayo ilijitenga na dini ya Kiyahudi. Na Wakristo hawa, walikuwa wanasema: “*sisi tutamwabudu Mungu tu*”. Shida ilikuwa kwamba – kila mtu alipaswa kumwabudu mfalme wa Roma, na kutoa sadaka kwa miungu mbali mbali. Hii ilikuwa sheria, na mtu alipaswa kuitimiza. Na kama ungepuuza sheria hii, ungewekwa gerezani, au hata kuuawa. Na Wakristo walikuwa wanasema: “*hatutamwabudu mflame; tutamwabudu Mungu pekee*”.

Kwa hiyo unaweza kuona jinsi ambavyo Wakristo, waliwekwa katika kipindi kigumu. Na Petro anajua kwamba, mateso haya yataongezeka zaidi na zaidi. Na kwa hiyo, anataka kuyaandaa makanisa katika Asia Ndogo, na kuwaonya kwa ajili ya mambo yanayoweza kutokea. Na anawatia moyo kwamba, wawe watiifu kwa Kristo – hata kama kutakuwa na mateso. Anasema “*simameni imara*”. Imani yenu itajaribiwa – lakini aminini katika Mungu. Na kumbukeni kwamba, kwa sababu ya Kristo na msalaba wake, mnatumaini. Hata kama hali ni mbaya, endeleeni kutumaini katika Kristo. Na mara tisa katika barua, Petro anawakumbusha kwamba Yesu atarudi. Hili ni wazo lingine – kurudi kwa Yesu Kristo. Kumbuka, anasema Yesu anakuja tena, na kwa sababu ya nafasi yenu katika Kristo, mtakuwa salama ndani yake.

Wazo lingine, ambalo Petro analenga ni ‘*utii*’, ambalo pia limeunganika na wazo la mateso. Petro anajaribu kuwafundisha kwamba, katika hali zote, wanapaswa kuwa na moyo wa utii, hata kama hawajatendewa vyema. Na anaangalia mazingira manne, ambayo anawataka wasomaji wake wawe watiii. Katika sura 2:13 anasema hivi: “*Tiini kila kia-mriwacho na watu*”. Na hapa, anazungumza kuhusu mamlaka ya serikali, mflame, au raisi. Petro anasema, kwa ajili ya Kristo, muwe watii kwa watu. Katika sura hii hii, anawaambia watumwa kuwa watii kwa bwana zao. Na kwa hiyo, wazo hili linahusu utii kwa bosu wako, kazini. Katika mstari wa kwanza wa sura ya tatu, Petro anawaagiza wake kuwa ‘*watii*’ kwa waume zao – anasema hivi: “*Enyi wake, nataka muwe watii kwa waume zenu*”. Je, hii inamaana gani? Basi, kwa siku chache zijazo, tutaangalia maana yake. Petro pia anawaambia waume, katika kifungu kile kile. “*Enyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili*”.

Na hatimaye, katika **sura 5**, anawaagiza vijana wa kiume, kuwa watii kwa wazee. Kwa hiyo, kuna mazingira manne ya utii: serikali, watumwa au wafanyakazi, wake, na vijana wa kiume. Lakini pia, anasema hivi katika **sura 5:5**: “*nanyi nyote, jifungeni unyenyekevu mpate kuhudumiana*”. Petro anasema, ninataka mhudumiane nyinyi kwa nyinyi, kwa moyo wa unyenyekevu. Na kwa kweli, tutahitaji kujifunza kutoka maneno haya. Basi, ngoja nihitamishe kwa mawazo haya. Fungua **Sura 1:1-2**. Tambua Petro anapoanza barua yake - anataka kutaja Utatu Mtakatifu. Mungu Baba, Yesu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu. Wote watatu wamehusika katika mchakato wa wokovu wetu. Tumechaguliwa na Mungu Baba. Tumetakaswa na Mungu Roho Mtakatifu, na tumenyunyizwa kwa damu ya Yesu.

Je, kirai hiki cha mwisho kinamaana gani? “*Tumenyunyizwa kwa damu ya Yesu*’. Kinasikika kama kitu kigeni katika masikio yetu, siyo? Lakini kwa kweli, ni alama ya kile ambacho Yesu alifanya msalabani kwa ajili yetu. Ni picha ya sadaka ya Yesu. Kumbuka katika Agano la Kale, sadaka ilipotolewa, kuhani alichukua baadhi ya damu ya mnyama, na kuinyunyiza juu ya madhabahu. Na hiyo ilipotokea, watu walikumbushwa kwamba, uhai umetolewa. Mnyama ameuawa, na kutolewa sadaka kwa Mungu, na kwa sababu ya kifo cha mnyama huyo, Mungu alikuwa amewasamehe, na kukubali sadaka yao.

Kwa kweli kulikuwa na nyakati tatu, ambapo watu walinyunyizwa kwa damu katika Agano la Kale. Jambo hili halisikiki vizuri - siyo? Lakini lilikuwa jambo muhimu sana. Katika tukio moja, Haruni na wanaye, walikuwa makuhani. Walikuwa wametengwa kwa ajili ya kufanya kazi ya Mungu. Mnyama alitolewa sadaka, na baadhi ya damu, ilinyunyizwa juu yao, kama alama ya kuonesha kwamba, walikuwa wamesamehewa na kusafishwa. Na ninafikiri kwamba, Petro anatumkumbusha hapa, kwa kutumia picha kutoka Agano la Kale, kwamba Wakristo wote, wamewekwa wakfu. Tumesimikwa kama makuhani katika ufalme wa Mungu; tumeoshwa dhambi zetu, kwa sababu tumenyunyizwa kwa damu ya Yesu. Na sasa, tumekubalika kwa Mungu. Hii ni habari njema kwetu – na hii ilikuwa habari njema kwa wasomaji wa kwanza wa barua hii. Ninafikiri kwamba, ingawa walikuwa wanateseka, walitiwa moyo na maneno haya.

KIPINDI 3: 1 Petro 1:13-16: “Iweni Watakatifu Kwa Sababu Mimi Ni Mtakatifu” Steve Lancaster

Fungua katika Biblia yako, kutoka **1 Petro 1**, na tutasoma kutoka mst **13-16**. Ninataka tuangalie kuhusu utakatifu wa Mungu, na agizo kwetu la kuwa watakatifu, katika mistari hii. Lakini, kabla ya kuangalia juu ya utakatifu wa Mungu, tambua jinsi Petro, anavyoanza kifungu hiki. Katika Biblia yangu ya Kingereza, anaanza na maneno: “*Andaeni akili zenu kwa matendo, na muwe na kiasi*”. Na ninafikiri hili ni rahisi kuelewa, si ndivyo? **Petro** anasema: jiandaeni na muwe tayari; muwe tayari kumwona Mungu akifanya kazi katika maisha yenu, na itikieni kwake moja kwa moja. Lakini ninajua kwamba, katika toleo la Kiswahili la Union, inasema kwamba: “*vifungeni viuno vya nia zenu*”. Je, hii inamaana gani? Kama hujui sana kuhusu utamaduni wa Biblia, toleo hili ni gumu kulielewa! “*Vifungeni viuno vya nia zenu*”? Je, inamaana gani? Ninafikiri inasikika kuwa kitu cha ajabu.

Ili kutusaidia kuelewa maana yake, ngoja nisome kutoka **Wafalme ya Kwanza 18:46**: “*Nguvu za Bwana zikaja juu ya Eliya, na akaifunga kanzu yake katika kiuno chake kwenye mkanda, akakimbia mbele ya Ahabu hadi Yezreel*”. Baada ya muda mrefu wa ukame, Eliya aliona wingu dogo angani, na akajua kwamba mvua kubwa itanyesha. Na kwa hiyo, akajiandaa kukimbia. Katika siku hizo, wanaume walivaa kanzu ndefu; hawakuwa wakivaa suruali. Hata leo hapa Tanzania, baadhi ya wanaume wa Kiislamu huvaa kanzu. Sasa, kama umevaa kanzu – ni vigumu sana kukimbia haraka! Kwa hiyo, **Eliya** alifanya nini? Alikunja kanzu yake, juu ya miguu yake, na akaifunga kwa mkanda kwenye kiuno chake, ili kwamba aweze kukimbia haraka.

Maneno haya haya, yametumika katika Kitabu cha **Kutoka 12:11**: Mungu alimpa maagizo **Musa**, kuhusu namna Waisraeli watakavyojiandaa kwa ajili ya Pasaka ya Kwanza. Mungu akasema: “*Tena mtamla hivi; mtakuwa mmefungwa viuno vyenu, mmevaa viatu vyenu miguuni, na fimbo zenu mikononi mwenu*”. Walipaswa kuwa tayari kwa ajili ya kusafiri haraka. Mara baada ya **Farao** kukubali kuwaacha watoke **Misri**, walihitaji kuondoka moja kwa moja. Mungu aliwaambia kwamba walipaswa kuondoka muda huo huo baada ya kujua. Fungeni kanzu zenu, katika mikanda ya viuno vyenu, ili kwamba muweze kukimbia haraka.

Pia kuna mfano katika Agano Jipya. Labda Petro alikuwa anafikiri kuhusu maneno ya Yesu, katika **Luka 12:35**. Katika toleo langu, inasema hivi: “*Muwe tayari mmejifunga mkanda kiunoni, kwa ajili ya kutumika*”. Katika toleo la Union, inasema hivi: “*Viuno vyenu na viwe vimefungwa*”. Ninafikiri inasikika kuwa kitu cha ajabu! Lakini Yesu alikuwa anawaagiza wanafunzi wake, kuwa tayari kwa matendo. Alisema itakuwa vizuri, kama bwana atawakuta watumishi wanasubiri kwa ajili yake,

atakapokuja kwenye nyumba. Kama watumishi wamelala, na hawajajiandaa bwana atakapo gonga mlangoni, hawafanyi kazi yao vizuri. “*Muwe tayari mmejifunga mkanda kiunoni, kwa ajili ya kutumika*”. Yesu alisema ‘*msiwe wavivu*’. Hakikisheni muko tayari kwa ajili ya kazi ya Mungu, anapowaambia kufanya.

Kwa namna hiyo hiyo, Petro anatumia kirai hiki katika **mst 13**. Anasema, “*vifungeni viuno vya nia zenu*”. Hana maana ya jambo la kimwili. Hatuambii kujiandaa na kukimbia kwa miili yetu. Lakini anatumia tuhakikishe kwamba, akili zetu zimejiandaa. Kwa maneno mengine, hakikisheni kwamba muko hai, na tayari kiroho. Hakikisheni kwamba mmejiaandaa kiroho. Hakikisheni kwamba mnakua katika imani yenu. Hakikisheni kwamba mko tayari kwa ajili ya kazi ya Mungu, katika maisha yenu, na kwamba mnaweza kumwitikia Mungu, moja kwa moja katika utii kamili.

Na kisha, katika **mst 14**, Petro anasema hivi: “*kama watoto wenye utii, msifuatisha nia ambazo mlikuwa nazo, kabla ya kuwa Wakristo*”. Je, wewe ni mtii kwa Baba yako wa mbinguni? Kama mtoto wa Mungu, anakuhitaji utii amri zake – kwa hiyo, wewe ni mtii kwake? Au kuna baadhi ya maeneo katika maisha yako, ambapo hauko mtii kwa Mungu? Petro anasema, “*msifuatisha nia ambazo mlikuwa nazo kabla ya kuwa Wakristo*”. Msifuate njia za ulimwengu. Mmeitwa kuwa watu walio tofauti.

Kwa kweli, Petro anasema, umeitwa kuwa mtakatifu. Umeitwa kwa ajili ya kufanana na tabia ya Mungu. **Mst 15&16**: “*Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa, Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu*”. Na hapa Petro ananukuu kutoka Agano la Kale, Kitabu cha **Mambo ya Walawi** (11:44). Kwa kweli, kirai hiki kimeandikwa mara tatu katika Mambo ya Walawi, wakati Mungu anaongea na Waisraeli katika jangwa la **Sinai**. Hii ilikuwa amri ya Mungu kwa watu wake wateule. Na kwa hiyo, ninataka tuangalie kwa ukaribu juu ya utakatifu wa Mungu, kwa sababu ni somo muhimu sana. Je, inamaana gani kuwa mtakatifu? Na kama Petro anasema kwamba, tunapaswa kuwa watakatifu, katika kila jambo tunalofanya, tunawezaje kufanya hivyo? Je, ni kwa namna gani tunajifunza kuwa watakatifu, hata kama tu watu wenye dhambi?

Tunaposema kuhusu ‘*utakatifu wa Mungu*’, Je, tunafikiri nini? Ninafikiri kwamba tunaposema neno ‘*utakatifu*’, mara kwa mara, tunakuwa na picha tofauti, katika akili zetu – hata kama ni Wakristo. Nilikuwa ninasoma kitabu kimoja juu ya utakatifu, kilichoandikwa na mwalimu wa Biblia huko Marekani, na alisema hivi: “*Nilipokuwa mvulana mdogo, nikiendelea kukua katika kanisa, nilifikiri utakatifu kilikuwa kitu cha kuchosha. Sikuwapenda watu watakatifu kwa sababu kamwe hawakuwa watu wa kutabasamu, na wasio furahia kitu chochote! Walikuwa wanachosha, na walikataa kitu chochote, ambacho kilikuwa cha kuburudisha, na kufurahisha. Huu siyo utakatifu*”. Kama alipokuwa anakua katika kanisa, na alipowaangalia watu waliokuwa Wakristo, mara zote alikuwa akiambiwa kwamba, watu hao walikuwa watakatifu. Lakini walionekana kuwa na huzuni! Huu siyo utakatifu.

Kwa hiyo, utakatifu wa Mungu ni nini hasa? Hakuna maana rahisi ya utakatifu. Kuna vitu vingi sana, katika neno hili ‘*utakatifu*’. Utakatifu wa Mungu ni mkubwa sana, na wa kushangaza kwetu kama wanadamu, kwamba ni vigumu kuelezea kwa usahihi maana yake. Na katika Biblia, neno ‘*utakatifu*’ limetumika katika namna nyingi sana - lakini ngoja nijaribu kuelezea maana ya utakatifu. Ninafikiri kwamba maana ya kwanza, tunayofikiri tunaposikia neno ‘*utakatifu*’ - ni ‘*usafi*’; kitu kisicho na dhambi na uchafu; kitu halisi na safi; na Biblia inatumia neno hili, katika namna hii - lakini pia lina maana nyingi zaidi ya hiyo.

Maana ya neno 'utakatifu', imeungana na neno la Kiebrania '**kwadesh**' – na linatokana na neno la zamani lenye maana ya '**kutenga**'. Huko Uingereza tuna methali, ambayo inaweza kusaidia kueleza maana ya neno hili. Kama tunataka kushona nguo, au suti, huwa tunaenda dukani, na kuangalia vitambaa mbali mbali. Muuza duka anaweza kusema: '*je unapenda kitambaa hiki?*' Au '*vipi kuhusu kitambaa kile pale?*' Na huwa tunaangalia vitambaa mbali mbali, na kuvishika ili kuona jinsi vilivyo. Na muuza duka anaweza kusema, '*kitambaa hiki ni cha gharama kuliko kile pale, kwa sababu kina ubora zaidi*'. Na kwa hiyo, baada ya kuangalia vitambaa mbali mbali, kama una pesa za kutosha, utataka kuchagua kitambaa bora zaidi. Kwa hiyo, nitasema: '*kitambaa hiki ni bora kuliko vingine vyote; kitambaa hiki kimejitenga na vitambaa vingine; ni kitakatifu; kimejitenga na vitu vingine*'.

Ngoja niwape mfano mwingine, na safari hii, nitatumia mpira wa miguu! Tunapotazama mechi ya mpira wa miguu, kuna wachezaji **22**, ndani ya uwanja. **11** kwa kila upande. Unapotazama mechi, utagundua kwamba, baadhi ya wachezaji ni bora kuliko wachezaji wengine. Kwa kweli, unaweza kugundua kwamba, kuna mchezaji mmoja, ambaye ni bora zaidi ya wote. Ana ujuzi zaidi; anakimbia haraka kuliko wengine; anafunga magoli mengi kuliko wengine. Ninafikiri kuhusu wachezaji kama **Messi**, au **Ronaldo**, au kwa siku za nyuma, **David Beckham**, au **Zidan**! Hawa ni wa-chezaji maalumu. Na kwa hiyo, ninapozungumza kuhusu mchezaji, ambaye ni bora kuliko wengine, ninaweza kusema kwamba: "*yuko juu, lakini wengine wote, wanafuata chini yake. Yeye ni maalumu lakini wengine wote ni wa kawaida. Yeye ni wa tofauti kuliko wengine. Yeye amejitenga na wachezaji wengine*".

Ninatumaini kuwa mifano hii, inatusaidia kuelewa maana ya utakatifu, tunapozungumza kuhusu Mungu. Kumbuka, neno hili 'utakatifu', limetokana na neno la Kiebrania '**kwadesh**', lenye maana ya '**kutenga**'. Tunapomlinganisha Mungu na vitu vingine katika ulimwengu, yeye **amejitenga** kutoka vitu vyote. Yeye ni maalumu; yeye ni halisi; yeye ametengwa; yeye yuko juu ya vyote; yeye ni mtakatifu. Kwa kweli, utakatifu wa Mungu uko hata zaidi ya hivyo. Utakatifu wa Mungu unaenda zaidi ya mipaka ya uzoefu wetu; uko juu ya kila kitu tunachokijua. Mungu yuko juu tena zaidi yetu, ana nguvu kamili juu ya ulimwengu. Je, wajibu wetu kwa Mungu aliye mtakatifu ni nini? Kuna vifungu vingi katika Biblia, ambavyo vinatunyesha utakatifu wa Mungu, lakini kwa dakika chache, ninataka tuangalie kifungu kidogo, katika kitabu cha Isaya. Tufungue **Isaya 6:1-5**. Hiki ni kifungu maarufu kinachohusu utakatifu wa Mungu, na tunonesha jinsi tunavyopaswa kuitikia utakatifu wake.

Hapa kuna swali kwako. Je, umewahi kuguswa na utakatifu wa Mungu? Kumbuka, ndani ya Biblia, Mungu anaitwa mtakatifu, kuliko majina yote. Nguvu zake ni takatifu. Huruma yake ni takatifu. Pendo lake ni takatifu. Hekima yake ni takatifu. Haki yake ni takatifu. Tabia zote hizi ni takatifu; kila kitu kuhusu yeye ni kitakatifu. Na hiki ndicho kinachomfanya yeye kustahili sifa, na ibada zetu. Tunapotambua jinsi Mungu alivyo mtakatifu, tunachoweza kufanya ni kumwabudu yeye; tunachoweza kufanya ni kuinama chini mbele zake – kama vile **maserafi** katika maono ya Isaya. Tambua kwamba katika **mst 2** wa kifungu hicho, maserafi wanajiwasilisha katika uwepo wa Mungu: "*kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka*".

Maserafi ni nini? Na wakoje? Hatujui kwa uhakika, kwa sababu Biblia haitupi picha yoyote. Inaonekana kwamba, wao ni malaika wa mbinguni. Wametajwa kwa jina tu hapa katika **Isaya 6**, ingawa baadhi ya wasomi wanafikiri kwamba, pia wanaweza kuwa ndio wale viumbe wa-nne, waliotajwa katika Kitabu cha **Ufunuo**. Waliumbwa na kutengenezwa kwa ajili ya kusudi moja - kutangaza utakatifu wa Mungu. Hiyo ndiyo kazi yao – kuuimba utakatifu wa Mungu. **Ufunuo 4:11**, unasema hivi: "*Usiku na mchana, viumbe hawa hawaachi kuimba: 'mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu*".

ni Bwana Mungu Mwenyezi". Lakini hata hivyo walikuwa katika uwepo wa Mungu wakati wote, na ingawa waliumbwa kwa ajili ya kumsifu Mungu, utakatifu wake ulikuwa unameremeta na ni msafi sana, walijifunika macho yao, ili wasiangalie kwenye uso wa Mungu. Hawakuweza kumwangualia Mungu moja kwa moja – alikuwa mtakatifu sana. Je, unakumbuka ombi la Musa katika **Kutoka 33, mst 20**? Aliamua kumuuliza Mungu swali kijasiri. Hivi ndivyo alivyo sema: "*Mungu tafadhali nioneshe utukufu wako; nioneshe uso wako*". Je, jibu la Mungu lilikuwa nini? "*Musa, huwezi kuuona uso wangu, kwa sababu hakuna anayeweza kuuona uso wangu, na akaishi*". Kwa maneno mengine, 'huwezi kuuona utakatifu wangu, na ukapona'. Lakini Mungu alikuwa mwenye huruma kwa Musa; alimpeleka kwenye ufa katika mwamba, na kumfunika kwa mikono wake, wakati alipopita katika utukufu wake – lakini baadaye, akamruhusu Musa, kuuona mgonga wake, wakati anapita.

Mungu anasema: "*uso wangu haowezi kuonekana. Mimi ni mtakatifu sana siwezi kuonwa na wanadamu. Utakatifu wangu una nguvu na msafi sana, hata maserafi na malaika, hawawezi kuuangalia*". Kadri maono ya Isaya yanavyoendelea, maserafi hawa si kwamba wanajifunika macho yao tu, lakini pia wanaita kila mmoja katika **mst 3**. "*Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiye Bwana Mwenyezi Mungu; dunia yote imejaa utukufu wake*".

Mbali na **Ufunuo 4**, nafikiri kwamba hii ni sehemu pekee katika Biblia, ambapo tabia ya Mungu imejirudia mara tatu. Na imerudiwa mara tatu, kwa ajili ya kuweka msisitizo jinsi Mungu alivyo mtakatifu. Maserafi hawamwelezei Mungu kama '*mtakatifu*' tu, au kama '*mtakatifu, mtakatifu*' – lakini wanataka kutumia neno hili mara tatu. Mungu wetu, siyo kwamba ni mtakatifu tu; wala siyo kwamba ni mtakatifu mara mbili tu; lakini Mungu wetu ni mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu! Unajua, hatusomi kirai '*Mungu ni pendo, pendo, pendo*', ingawa unapenda kuzungumza kuhusu upendo wa Mungu. Hatusomi kirai '*Mungu ni mwenye neema, neema, neema*', na bado tunajua kwamba Mungu amejaa '*neema*'. Na hapa, Mungu ameelezewa kama '*mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu*'. Utakatifu wa Mungu umeinuliwa juu kuliko tabia zingine zote – na kwa hiyo, hili ndilo wazo kuu kuhusu Mungu alivyo. Hili linapaswa kutufanya tutetemeke. Kama inavyosema **1 Petro 1:17**: tunapaswa kuishi maisha yetu katika hofu ya heshima. Tunapaswa kushangazwa kwamba, mtu ambaye ni mtakatifu sana, anataka kufanya uhusiano pamoja nasi, kama wanadamu tulio na dhambi.

Tambua kitu gani kinatokea **maserafi** wanapolia katika **mst 4**. "*Na misingi ya vizingiti ikatikisikia kwa sababu ya sauti yake aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi*". Na kwa Isaya, hii lazima ilikuwa inashangaza. Je, umewahi kushuhudia tetemeko la ardhi? Labda umewahi kuliona katika TV – na kuona kilichotokea wakati wa tetemeko. Ardhi huwa inaanza kucheza, na kuta huanza kuanguka chini; majengo huanguka. Linaweza kuwa linatisha. Na hiki ndicho kinachotokea, karibu na Isaya katika maono yake – hekalu linatikisika. Lakini, hili halina uhusiano wowote na tetemeko la ardhi la asili – huu ni mwitikio tu wa jengo dhidi ya utakatifu wa Mungu! Milango na misingi ilitikisika. Matofali na mawe, yalikuwa yanatikisika. Hata vitu hivi visivyo na uhai, vilikuwa vinasukumwa na utakatifu wa Mungu! Kwa kweli, katika Agano la Kale, hili lilikuwa jambo la kawaida. Mara kwa mara, tunasoma kuhusu vitu vya asili vikiitikia utakatifu, na utukufu wa Mungu. Hata tunasoma kuhusu milima ikitikisika! Hebu fikiriri kuhusu wakati, ambapo **Mlima Sinai** ulitikisika katika **Kutoka 19:16-18**. Hii ni dunia ikitikia utakatifu wa Mungu.

Je, ni kitu cha kushangaza kwamba, tunaposoma Biblia, tunaona kwamba milima na majengo, milango na tofali za mawe; vitu visivyo na uhai – vinaguswa na uwepo na utakatifu wa Mungu? Lakini sisi, tulio hai kimwili, na pia tulio hai kiroho, mara kwa mara hatuguswi na utakatifu wa Mungu! Baadhi yetu, tunapoenda kanisani, tunaweza hata kuchoshwa na jambo la kumwabudu

Mungu! Hili ni tusi lililoje kwa Mungu! Je, utakatifu wa Mungu huwa unakugusa wewe, au umechoshwa na jambo la kumwabudu Mungu? Kwa kweli, katika makanisa yetu, mambo mengi tunayoyaita ibada, siyo ibada kabisa. Katika makanisa yetu, je, huwa tunakuja mbele za Mungu, kwa heshima na hofu, au huwa tunasahau jinsi Mungu alivyo mtakatifu? Tunapaswa kuwa tunaomba: *'Baba, tupe angalau picha kidogo ya utakatifu wako. Tusaidie kukutendea kwa hofu ya heshima, ili kwamba tuweze kukuabudu katika Roho na kweli, kwa moyo wetu wote'*. Kwa kweli, kuna mstari wa ajabu, katika Kitabu cha **Waebrania**, ambao unajumuisha jinsi maombi yetu yanavyo takiwa yawe: **Waebrania 12:28**: *"Tuwe na shukrani na kumwabudu Mungu kwa namna itakayompendeza, kwa ibada na hofu"*.

Je, nini mwitikio wa Isaya katika kukutana kwake na Mungu mtakatifu? **Mst 5**, unasema hivi: **"Ole wangu! Kwa maana nimepotea, kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu"**. Hapa ni Isaya, mtu mwenye haki, nabii na kiongozi mkuu. Hapa ni mtu mwenye nafasi ya kuingia katika mahakama ya kifalme, na aliweza kuongea katika maisha ya wafalme angalau watano wa Yuda. Alijua kuwa kilikuwa kitu cha namna gani, kukutana na wafalme na marais – lakini hapa katika hekalu, akiwa ameuona utakatifu wa ajabu wa Mungu, alijinyenyekeza kabisa! Neno lililotumiwa katika toleo la Union ni *"kupotea"*: *"Ole wangu! Kwa maana nimepotea"* – lakini sifikiri kama hii ni tafsiri nzuri. Haioneshi kikamilifu jinsi Isaya anavyojisikia. Toleo la **Habari Njema** linasema hivi: *"Ole wangu! Mimi nimeangamia"*. Isaya anasema, kwa sababu ya kile nilichokiona, najisikia kuvunjika. Ninagundua kwamba mimi siyo kitu chochote, ninapomwona Mungu huyu mtakatifu.

Na bado, **Isaya** alichukuliwa kama mtu miongoni mwa watu watakatifu sana, katika **Yerusalemu**. Alikuwa anaheshimiwa sana kama nabii. Lakini – alipouona utakatifu wa Mungu, aligundua ni jinsi gani ni mwenye dhambi, na anajinyenyekeza sana mbele za Mungu. Kama unataka kujua ikiwa mtu anakua katika utakatifu, angalia mwitikio wake dhidi dhambi, katika maisha yake. Kadri unavyokua katika utakatifu, ndivyo unavyojua jinsi ulivyo mwenye dhambi, katika maisha yako, na ndivyo inavyokugusa zaidi. Je, unajali swala la dhambi katika maisha yako? Je, unafanya kwa bidii kupinga majaribu? Kama unafanya, basi hiyo ni ishara kwamba unakua katika utakatifu, na kwamba hutaki kumuudhi Mungu mtakatifu.

Je, unakua katika utakatifu? Je, unafanya bidii kuwa mtakatifu? Petro anatuamuru kuwa hivyo. Angalia **1:15**: *"Kama yeye aliyewaita, iweni watakatifu katika yote mnayofanya – iweni watakatifu"*. Je, inawezekana kwetu kuwa watakatifu? Tunajua kwamba sisi ni wenye dhambi, na tumeona kwamba, Mungu Mwenyezi ni mtakatifu – kwa hiyo, inawezekanaje mimi na wewe, tulio wanadamu tu, kuwa watakatifu? Ni fumbo – mpaka tuelewe alichofanya Yesu msalabani! Ngoja niwasomee mstari mwingine wa ajabu, katika Kitabu cha **Waebrania**, na hakikisha unasikiliza vizuri hapa! **Waebrania 10:10**: *"Katika mapenzi hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu"*. Kama wewe ni Mkristo wa kweli; kama ni mkristo uliyezaliwa upya; kama unamfuata Yesu Kristo – umetakaswa. Yesu alikufa ili akutakase. Na kwa hiyo, Mungu Baba anapotuona, haoni dhambi tulizofanya siku zilizopita - badala yake, anaona utakatifu wa Yesu. Kwa sababu ya damu ya Yesu – tumesamehewa; tumetakaswa!

Tunapokuwa watoto wa Mungu; tunapompa yeye maisha yetu; Roho Mtakatifu anapoingia katika maisha yetu – tunakaribishwa katika familia yake, na tunakuwa **watakatifu**. Hivi ndivyo Wakristo wa kwanza walivyoitwa. Mtakatifu Yohana, Mtakatifu Marko, Mtakatifu Paulo - na kadhalika. Kama wewe ni Mkristo, hivi ndivyo unavyoitwa; mtakatifu. Na bado tupo kwenye hatua ya kufanywa watakatifu. Tunatakaswa na kukamilishwa kadri tunavyoendelea kutembea pamoja na Mungu, katika maisha ya kila siku. Lakini bado, hatutakamilika kuwa watakatifu, mpaka tufike mwisho wa safari yetu, ya kuingia mbinguni.

Neno '*watakatifu*' linapotumiwa leo, huwa tunafikiri kwamba neno hili, ni kwa ajili ya watu, ambao wamekuwa Wakristo maalumu tu. Huwa tunafikiri kwamba neno hili, linamwelezea mtu fulani, ambaye ni mtakatifu sana, na mwenye haki, na ambaye amefanya mambo makubwa sana, kwa ajili ya Mungu. Je, unajua kwamba Kanisa la Roman Katholiki, wana orodha ya watu wa watakatifu? Na Papa akitaka anaweza kuamua kumfanya mtu fulani kuwa mtakatifu! Wamelichukua neno '*mtakatifu*', na kuwapa watu wachache tu, ambao walifanya mambo mema, katika siku za nyuma.

Lakini, Agano Jipya linatumia neno '*mtakatifu*', kwa ajili ya waumini wa kawaida – kwa ajili ya kila mtu, ambaye ni Mkristo wa kweli. **Mtume Paulo**, anapoya-andikia makanisa katika Agano Jipya, anaelekeza barua zake nyingi kwa '*watakatifu*'. Na kwa hiyo, barua kwa kanisa katika **Efeso** inanza: "*Kwa watakatifu walioko Efeso*". Paulo alipoliandikia kanisa katika **Kolosai**, alisema hivi: "*Kwa ndugu watakatifu, waaminifu katika Kristo, walioko Kolosa*". Kwa maneno mengine – kwa watakatifu; kwa wale walio chaguliwa; kwa wale waliotakaswa. Na bado, inaonekana jambo la ajabu kuwaelezea baadhi ya Wakristo hawa kama watakatifu, siyo? Tunaposoma barua za **Paulo**, tunajua kwamba, wasomaji wengi wa barua zake, walikuwa wanapambana na aina zote za dhambi, katika maisha yao. Paulo anaanza barua zake kwa neno '*kwa watakatifu*', lakini mara kwa mara, anaendelea kuwakemea baadhi yao, kwa sababu ya dhambi zao, na tabia zao, mbaya!

Na tunahoji jinsi gani maneno '*mtakatifu*' na '*mwanadamu*', yanaweza kwenda pamoja. Tunaona kwamba watu wateule, katika Biblia, waliitwa '*watakatifu*', siyo kwa sababu walikuwa tayari safi, na wakamilifu - lakini kwa sababu walikuwa wameteuliwa, na kufanywa watakatifu, kwa sababu ya Kristo na msalaba wake. Kama vile Waisraeli, walivyoitwa na kuchaguliwa kama watu wa Mungu – sisi pia, kama Wakristo, tumeteuliwa na kufanywa watakatifu. Kwa hiyo, hapa kuna swali. Kama Mungu ametufanya watakatifu, kupitia kazi ya Yesu msalabani, na kama tayari anatuona kama watakatifu katika ufalme wake - je, kwa nini Petro anatuagiza kuwa watakatifu? Je, kwa nini Mungu anataka tuishi maisha matakatifu, kama tayari tumefanywa watakatifu? Katika Agano Jipya kulikuwa na kundi la watu walioitwa '**Gnostic**', na walifikiri kuhusu swali hili - lakini walifikia jibu, ambalo siyo sahihi! Walisema: '*tumesamahewa na Mungu; dhambi zetu zote zimeondolewa na Mungu; tumeokolewa – kwa hiyo hatunahaja ya kujisumbua kuwa watakatifu*'. Waliamini kwamba, hawakuhitaji kutii amri ya kuwa watakatifu, kwa sababu tayari walikuwa wametakaswa. Na kwa hiyo, waliendelea kutenda dhambi katika maisha yao. Walienenda kama watu wasiyo Wakristo. Kwa kweli, hawakuwa waumini wa kweli, na hawakuelewa ujumbe wa msalaba.

Biblia zetu zinatambia kwamba, kwa sababu ya Yesu, wale ambao ni Wakristo wa kweli wametakaswa. Lakini Biblia pia inasema kwamba, tunapoishi maisha yetu kama Wakristo, pia tuna kazi ya kufanya. Tunapaswa kufanya bidii ya kutafuta utakatifu. Tunapaswa kuipinga dhambi kwa bidii. Tunapaswa kukua katika utakatifu kama watoto wake, na ili tufanye hivyo, tunapaswa kufanya bidii. Hii ndiyo maana ya ufuasi. **Waebrania 12:14** unasema hivi: "*Fanyeni kila bidii ili muwe watakatifu*". Na kama tunampenda Mungu kweli, na kama tunaelewa alichofanya kwa ajili yetu kupitia Yesu, hakika tutataka kumpendeza yeye, na tutataka kufanya bidii ya kuwa watakatifu zaidi na zaidi, katika maisha yetu. Tumetakaswa – lakini pia, tunapaswa kufanya bidii ya kuwa watakatifu.

Napenda nihitamishe kwa maswali machache. Ninataka ufikiri kuhusu maswali haya, na kuyajibu moyoni mwako. Je, unatamani kuwa mtakatifu zaidi? Je, unafanya bidii kuutafuta utakatifu? Je, unautafuta msaada wa Mungu, ili uwe mtakatifu? Je, unafanya bidii kuidhibiti dhambi, katika

maisha yako, au amekata tamaa kupambana dhidi ya dhambi? Agizo la Petro kwetu leo ni hili: *“Iweni watakatifu katika kila mfanyalo, kwa sababu Mungu aliyewaita ni mtakatifu”*.

KIPINDI 4: 1 Petro 1:3-12: “Kusifu, kuzaliwa upya, tumaini, urithi, kujaribiwa, wokovu”

Steve Lancaster

Tufungue Biblia zetu, na tutasoma kutoka **1 Petro 1:3-12**. Hili ni fungu ambalo limejaa mafundisho ya Kikristo. Petro hapa anazungumza kuhusu misingi ya imani yetu. Anataja tumaini ambalo tunalo katika Kristo, kwa sababu ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu. Anazungumza kuhusu kuzaliwa upya. Anatuambia kwamba tunaurithi, ambao haowezi kuharibika. Anasema kwamba, kadri tunavyoishi, imani yetu itajaribiwa na kuthibitishwa. Pia anazungumza kuhusu wokovu ambao tunao katika Kristo.

Jambo la kwanza ambalo nataka tutambue ni kwamba, Petro anaanza na **sifa**. Angalia **mst 3**: *“Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo”!* Kwa hiyo, mwanzo wa barua yake, anapoanza mafundisho yake, Petro anataka kumsifu Mungu. Anataka kumheshimu Baba. Anataka kumshukuru Mungu. Na Petro siyo mtu peke anayeanza kwa maneno haya. Katika **Waefeso 1 na 2 Wakorintho 1**, Paulo anatumia maneno yale yale (Waefeso 1:3, 2 Kor 1:3). *“Ahimidiwe Mungu - atukuzwe Mungu”*. Inaonekana kwamba, hii ilikuwa salamu yenye kiwango katika kanisa la kwanza. Hata kama utarudi katika Agano la Kale, kuna kirai kile kile kilichokuwa kikitumiwa. Tunasoma mara kwa mara katika vitabu vya Agano la Kale: *“Ahimidiwe Bwana, Mungu wa Israeli”*. Na kwa hiyo, Petro anaendelea katika utamaduni huu wakumsifu Mungu, na kuwatia moyo wengine kuungana naye katika sifa.

Nimegundua kwamba katika kanisa la **AIC**, maneno *“Bwana Yesu asifiwe”* yanasemwa sana! Maneno haya yanatumiwa kama salamu, unapokutana na mtu fulani. Na ni sahihi kumsifu, na kumwabudu Mungu. Ni sahihi kumpa shukrani, na heshima. Lakini pia, nimegundua kwamba, wakati mwingine, maneno haya hayasemwi kwa kumaanisha! Wakati mwingine hayaelekezwi kwa Mungu – bali kwa watu katika kusanyiko! Mara kwa mara yanasemwa kwa sababu mtu anayehubiri, au kuongea, hajui maneno ya kusema! Wakati mwingine maneno haya yanasemwa na mchungaji kwa sauti kubwa, ili kuwaamsha watu wanaposinzia! Wakati mwingine maneno haya yanasemwa tena na tena, ili kuvuta usikivu wa watu, na mtu anayeyasema, hamaanishi. Sisemi hivi ili kuwavunja moyo msiyatumie maneno haya - lakini tunapaswa kuwa makini. Haya ni maneno ya thamani. Tunapoyatumia maneno haya, yanapaswa kutoka moyoni, na siyo kutoka mdomoni tu.

Petro anaanza mafundisho yake kwa kumsifu Mungu, na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo. Kwa nini? Ni kwa sababu gani, Petro anaanza na sifa, katika mstari huu? Yesu alifufuka kutoka kwa wafu! Hii ndio sababu! Na kwa sababu Mungu wetu, amejaa rehema kwetu, tumezaliwa upya – na tunatumaini lililo hai. Bwana Yesu asifiwe! Lakini maneno haya yanamaana gani? *“Tumezaliwa upya - ametuzaa mara ya pili”*. Kama ukiangalia mbele katika **mst 23**, utaona kwamba Petro anatumia maneno yale yale tena. Anasema: *“Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili, kwa neno la Mungu lenye uzima”*. Baadhi ya watu pia wanatumia maneno ‘kuzaliwa tena’.

Haya ni maneno ambayo baadhi ya watu huwa hawayaelewi. Hata baadhi ya Wakristo hawayaelewi maneno haya - *“kuzaliwa mara ya pili”* au *“kuzaliwa tena”*. Baadhi ya Wakristo watasema: *“Je, umezaliwa tena?”* Na baadhi ya Wakristo watasema: *“Je, umeokoka?”* Virai hivi

vyote vina maana moja. Na tunapaswa kukumbuka kwamba maneno haya “*kuzaliwa tena*”, na “*kuokoka*”, haya ni maneno ya kibiblia! Usiogope kutumia maneno, “*Je, umeokoka*”, kwa sababu ni maneno ya kibiblia. Je, ni wapi Yesu anatumia maneno haya: “*kuzaliwa tena*” au “*kuzaliwa mara ya pili*”? Tufungue **Yohana 3**, kuna hadithi maarufu ya Nikodemo. **Yohana 3:1-5**.

Utaona katika mstari wa kwanza kwamba **Nikodemo** alikuwa Farisayo, na pia alikuwa mjumbe wa baraza la Wayahudi. Tunaposoma Injili, tunaona kwamba Mafarisayo wengi hawakumpenda Yesu; walitaka kumfukuza. Lakini, kulikuwa na Mafarisayo wachache, ambao kwa siri walitaka kumfuata Yesu, na Nikodemo alikuwa miongoni mwa hao watu. **Mst 2** unatuambia kwamba alienda kwa Yesu usiku, labda kwa sababu hakutaka kuonekana akizungumza na Yesu. Labda aliogopa Mafarisayo wengine kwamba watamwona na kumkemea. Hatujui – lakini hivi ndivyo anavyosema kwa Yesu: “*Mwalimu, tunajua ya kuwa u mwalimu umetoka kwa Mungu, kwa maana hakuna mtu awezaye kuifanya miujiza hii unayofanya wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye*”. Tambua kwamba hapa haulizi swali; anatumia kauli. Lakini Yesu anajua kitu gani Nikodemo anafikiri.

Yesu anajua kwamba Nikodemo anatafuta ukweli, na anajua kwamba kwa wakati huu, yuko inje ya ufalme wa Mungu. Na kwa hiyo anamwambia katika **mst 3**: “*Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona uflame wa Mungu*”. Ninafikiri kwamba Nikodemo anasimama pale mbele ya Yesu, akikuna kichwa chake. Haelewi Yesu anamaanisha nini. **Mst 4**. Nikodemo anasema: “*Je, hili lawezaje kutokea? Ni kwa namna gani mtu ataweza kuzaliwa tena wakati ni mzee? Haiwezekani kabisa! Kwa hakika, hawezi kurudi tena tumboni mwa mama yake, na kuzaliwa tena*”. Unaona, Nikodemo anafikiri kuhusu kuzaliwa kimwili – lakini Yesu anazungumza kuhusu kuzaliwa kiroho. Na anamwambia katika **mst 5**: “*Na kwambia ukweli, hakuna mtu anayeweza kuuona ufalme wa Mungu mpaka azaliwe kwa maji na kwa roho*”. Je, Yesu anasema kitu gani hapa? Anasema hivi: hakuna mtu anayeweza kuwa sehemu ya familia ya Mungu; hakuna mtu anayeweza kukaribishwa katika ufalme wa Mungu; hakuna mtu anayeweza kupata uzima wamilele - isipokuwa amekuwa hai kiroho. Nikodemo, hakika kwa sasa, wewe umekufa kiroho. Ni mwenye dhambi, na kwa sababu ya dhambi zako, umetengwa na Mungu. **Unahitaji kuzaliwa tena**.

Unahitaji kuzaliwa kwa Roho Mtakatifu. Unahitaji kufanywa hai kiroho. Nikodemo – ninaongea kuhusu kuzaliwa kiroho, siyo kuzaliwa kimwili. Na katika **mst 10**, Yesu hata anamkemea Nikodemo, kwa kushindwa kuelewa jambo hili. Anamwambia hivi: “*wewe ni mwalimu katika Israeli; kwa nini sasa huelewi ni nacho kuambia*”? Kama wewe ni mchungaji au mwinjilisti katika **AIC**, Je, unaelewa maana ya kuzaliwa tena? Unawajibika katika afya ya kiroho ya kanisa lako. Kama mtu unayefundisha kanisani – Je, unaweza kuelezea jambo hili kwa watu wako? Na tumaini hivyo, kwa sababu ni jambo linalojenga msingi wa maana ya kuwa Mkristo. Yesu anasema: “*hakuna anayeweza kuingia katika ufalme wa Mungu, isipokuwa amezaliwa tena; isipokuwa amezaliwa kwa maji, na kwa Roho*”.

Alama ya mwamini wa kweli, ni mtu ambaye ana Roho Mtakatifu akiishi ndani yake – lakini ili jambo hili litokee, mambo fulani yanapaswa kutokea. Mtu anahitaji kumwamini Yesu. Mtu anahitaji kuamini katika kifo, na kufufuka, kwa Yesu. Pia mtu anahitaji kukubali kwamba ni mwenye dhambi; aliyetengwa na Mungu. Anahitaji kutubu dhambi zake, na kuomba msamaha wa Mungu. Anahitaji kuoshwa dhambi zake – na katika **mst 5**, Yesu anapotaja ‘*maji*’, inawezekana anamaanisha jambo la ubatizo. Mtu aliyezaliwa tena amefanya mambo hayo yote – na ameamua kutoa maisha yake kwa Yesu. Amefanywa hai kiroho. “*Ahimidiwe Mungu, na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, kwa sababu katika rehema yake kuu, tumezaliwa upya - tumezaliwa tena*”. Kuna kitu kingine ambacho **Petro**, anamsifu Mungu kwa ajili ya hicho. Angalia **mst 4**. Mara tunapofanywa hai kiroho, “*tunakuwa tumezaliwa katika urithi, ambao hauwezi kuharibika, na uchafu, usiyonyauka* –

uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu". Je, urithi huu ambao Mkristo anaupata ni kitu gani? Watu wanapokufa, kwa kawaida huwa wanaacha pesa zao, vitu vyao, na mali zao, kwa watu wa familia zao. Kabla hawajafa, huwa wanaandika maelekezo.

Kwa mfano: *'nitakapokufa, ninataka pesa zangu zote wapewe watoto wangu, au nataka nyumba yangu apewe mke wangu'*. Wanaacha urithi kwa familia zao. Wakati mwingine, kuna weza kutokea mabishano kati ya wanafamilia, na mambo yanaweza kuwa mabaya sana! Kwa kweli, katika **Luka 12:13** jambo hili lilitokea. *"Mtu mmoja katika mkutano akamwambia Yesu, 'mwalimu, mwambie ndugu yangu anigawie urithi wetu'*". Urithi unaweza kusababisha matatizo katika familia! Je, unakumbuka hadithi ya mwana mpotevu? Mwana mdogo alimwambia baba yake: *'Nipe urithi wangu sasa. Sitaki kusubiri hadi ufe; nautaka sasa hivi'*. Hili lilikuwa tusi kwa baba. Kwa sababu fulani fulani, baba akampa mwanaye urithi wake. Na tunajua kwamba, mwana alienda mbali, na akachezea urithi wote. Akatumia vyote, na baadaye akajutia.

Kumbuka kwamba, unaweza kufurahia urithi wa namna hii, wakati ukiwa hai hapa duniani tu. Ni wa muda mfupi. Hauwezi kwenda nao utakapokufa. Vitu, nyumba, pesa; vitu unavyoweza kuurithi mwisho wake vitaharibika; ni vitu vya kuchakaa na kunyauka. Ni vitu vya kuharibika, kama Petro anavyosema katika **mst 18**. Kinyume na hili, Mungu hatuahidi urithi wa muda mfupi – Yeye amewaahidi watoto wake urithi usioharibika. Kama tutashikilia imani yetu, na kama tutaendelea kutembea na Bwana, urithi wetu umelindwa. Hakuna mtu wa kuuondoa. Hapatakuwa na mabishano kuhusu urithi huu! Ni ahadi – na tunajua kwamba, Mungu havunji ahadi zake. Katika **Waefeso 1:14**, Paulo anasema hivi: *"Mlipoamini katika Kristo, mlipigwa muhuri, ahadi ya Roho Mtakatifu. Yeye ni mdhamini wa urithi wenu"*. Hii ni ahadi ya ajabu!

Na angalia **urithi** huu ulipo. **Mst 4** unasema hivi: *"Urithi wenu umetunzwa mbinguni kwa ajili yenu"*. Urithi wetu wa kiroho, siyo kitu cha kidunia, lakini ni kitu cha thamani zaidi. Ni urithi wa kiroho, ambao umetunzwa katika mji wa milele wa Mungu. Na bado, kwetu sisi kama wanadamu, ni vigumu kupata picha ya jinsi mbinguni kulivyo - siyo kweli? Unaweza kusema, hatujui sana kuhusu mbinguni, kwa hiyo tutawezaje kufikiri kuhusu hili? Hatujui jinsi kulivyo. Labda, hatujui sana kuhusu mbinguni, kwa sababu hatujatumia muda mwingi, kujifunza zaidi jinsi Biblia inavyosema kuhusu jambo hili. Tumesongwa na kazi nyingi sana, katika maisha yetu hapa duniani, ndiyo maana mara kwa mara hatufikiri kuhusu mbinguni! Macho yetu yameangalia sana duniani, kiasi kwamba tunashindwa kuangalia juu, na kuzingatia mambo ya mbinguni.

Kama tu waaminifu, tunafikiri kuhusu mambo ya kimwili, kuliko mambo ya kiroho. Lakini kama urithi wetu uko mbinguni; na kama tutaishi milele mbinguni, haipaswi kuwa hivi. Kulikuwa na muhubiri maarufu huko Uingereza aliyeitwa **John Ryle**. Alikuwa askofu aliyeishi miaka **150** iliyopita. Hivi ndivyo anasema kuhusu mbinguni: *"Kama unaondoka kwenye nchi uliyozaliwa, na unapanga kwenda na kuishi katika nchi nyingine kwa maisha yako yote, ni kawaida kwamba utataka kutafuta kujua zaidi, kuhusu nchi hiyo kabla hujafika. Utataka kujua zaidi kuhusu nchi hiyo. Kama tunatumaini kwamba siku moja, tutaishi mbinguni milele, hakika tunapaswa kutafuta kujua kila kitu kuhusu mbinguni. Kabla ya kwenda katika nyumba yetu ya milele, lazima tujue kuhusu mbinguni"*. Na pia alisema hivi: *"Ninajisikia huruma kwa mtu, ambaye hajawahi kufikiri kuhusu mbinguni"*.

Je, huwa unafikiri kuhusu mbinguni? Kama Wakristo, Biblia inatuambia kwamba tunahitaji kufikiri kuhusu wakati ujao – hasa kuhusu makao yetu ya wakati ujao. Je, unajaribu kujifunza zaidi, kuhusu sehemu ambayo utaishi milele? Je, unatazamia kwenda mbinguni? Katika **Wafilipi 1:23**, Paulo anasema hivi, katika Biblia Habari Njema: *"Nakabiliwa na haya mawili yaliyo sawa. Natamani kuyaacha maisha haya nikakae pamoja na Kristo, jambo ambalo ni bora zaidi"*. **Mst 24**: *"Lakini - ni*

jambo la maana zaidi kwenu kama nikiendelea kuishi". Paulo alitamani kuwa mbinguni pamoja na Kristo. Je, unatazamia kuwa mbinguni? Je, unafikiri kuhusu mbinguni?

Je, unajua kwamba Mtume Paulo hakika alitumuru kufikiri kuhusu mbinguni? **Wakolosai 3:1** unasema hivi katika Biblia Habari Njema: "*Basi, ikiwa mmefufuka pamoja na Kristo, panieni mambo ya juu, kule Kristo aliko, ameketi upande wa kulia wa Mungu*". Hebu fikiria kuhusu mambo haya, anasema Paulo. Tafuteni kile ambacho Biblia inasema kuhusu makao yenu ya wakati ujao. Fanyeni bidii zaidi, kufikiri kuhusu urithi wenu. Kama wewe ni mfuasi wa kweli wa Kristo, kuna chumba kimetunzwa kwa ajili yako mbinguni! Na mlango wake una jina lako juu yake! Hii inapaswa kukupa shauku! Jambo hili linapaswa kukufanya ufurahi - hata kama unateseka kwa sasa. Kumbuka, wasomaji wa kwanza wa barua hii, walikuwa wanateseka. Petro anataka kuwatia moyo, na anawaambia kwamba, pamoja na hali mliyonyo, na ingawa mnateseka, furahini na kumsifu Mungu.

Katika rehema zake, Mungu ametunza nafasi kwa ajili yako, katika ufalme wake wa mbinguni. Umezaliwa upya, katika urithi usioharibika, kuchakaa, au kunyauka. Na umetunzwa mbinguni, kwa ajili yako! Na hii ni ahadi ya ajabu sana! Je, unakumbuka wakati Yesu alipokuwa anajiandaa kuwaacha wanafunzi wake, katika usiku ule alipokamatwa? Aliweza kuona kwamba walikuwa wamekata tamaa na kuhuzunika, na alitaka kuwatia moyo. **Yohana 14:2**: "*Nyumbani mwa Baba yangu, mna makao mengi. Ninakwenda huko kuandaa makao kwa ajili yenu. Na nikimaliza kuandaa makao kwa ajili yenu, nitarudi tena, na kuwachukua kwenda kukaa pamoja name - ili kwamba nilipo mimi nanyi muwepo*". Ni ahadi iliyoje hii!

Na kwa sababu ya imani yenu, katika Yesu Kristo, na kwa sababu mnaamini katika Yeye, Mungu atawalinda hadi muupokee wokovu wenu. Hivi ndivyo unavyosema **mst 5**. Na hapa, Petro anaingiza neno lenye fundisho kubwa – **wokovu**. Hili ni neno ambalo tunatumia sana katika kanisa, lakini linamaana gani? Kama mtu fulani angekuja kwako, na kusema '*nielezee maana ya wokovu ni nini*' - Je, ungeweza kuelezea kwake? Katika maneno rahisi, neno '*wokovu*' linamaana ya: "*kuokoa kitu fulani kisiangamie, au kuharibika*". Kwa mfano: kama mtu anazama ndani ya mto, na mtu mwingine akarukia ndani, na kumvuta mtu huyu kwa usalama, tungesema kwamba, mtu huyu ameokolewa dhidi ya kifo. Mfano mwingine: kama kuna moto katika nyumba, watu wanajaribu kutoka nje ya jengo hilo haraka. Lakini pia, wanajaribu kuchukua baadhi ya vitu, kuvitoa nje ya nyumba hiyo. Na wangesema: '*tumeweza kuokoa vitu vichache kutoka motoni*'. Lakini, neno hili linamaana gani kwa Mkristo? Wokovu ni kile kinachotokea, pale mtu anapookolewa kutoka maisha ya dhambi, na uharibifu wa milele. Na kuna mtu mmoja tu, katika ulimwengu huu, ambaye anaweza kutuokoa. Hatuwezi kujiokoa wenyewe – lakini tunamtegemea **Mwokozi** wetu atuokoe, na kutuweka huru kutoka maisha ya dhambi, na matokeo yake.

Katika kitabu cha **Matendo 4**, Petro na Yohana, walikuwa wamekamatwa kwa sababu ya kumponya mtu, katika eneo la hekalu. Na viongozi wa Wayahudi wakawaweka gerezeni. Siku iliyofuata, wakawahoji Petro na Yohana, na wakawaambia waeleze matendo yao. Petro alikuwa amejazwa na Roho Mtakatifu, na aliwajibu hivi: "*Wokovu haupatikani kwa mtu yeyote yule, kwa maana hakuna jina jingine chini ya mbingu, linaloweza kuwaokoa wanadamu*". Je, hili ni jina gani? Kwa hakika, ni jina la Yesu Kristo, Bwana na Mwokozi wetu. Hili ni jina lake; Yeye anayeleta wokovu. Yesu yupo katika shughuli ya kuokoa maisha! Na sote tumesikia hadithi, za watu jinsi walivyo okolewa na Yesu. Na kama wewe ni Mkristo, una hadithi ya kusimilia kuhusu siku, ambayo uliokolewa na Yesu; ushuhuda wako. Umeokolewa kutoka katika dhambi zako; nafsi yako imeokolewa kutoka katika kuangamia; nafsi yako imeokolewa kutoka jehanamu. Tumeokolewa, kwa imani katika Yesu, na bado huyu ni mtu, ambaye hatujawahi kukutana naye kimwili! Angalia **mst**

8, Petro anasema hivi: “*Ingawa hamjamuona, mnamwamini; na ingawa hammuoni sasa, mnaamini katika yeye*”. Na kisha, Petro anasema nini? “*Mmejazwa nafuraha isiyo elezeka*”.

Kwa nini? Kwa sababu “*mnapokea malengo ya imani yenu, wokovu wa nafsi zenu*”. Tambua anachosema Petro hapa: Anazungumza kuhusu maisha yako, ya sasa hivi. Anazungumza kuhusu wokovu wako, katika wakati uliopo. Kama unavyoishi maisha yako sasa hivi, katika wakati uliopo, unapokea wokovu wa nafsi yako.

Unaona, Biblia inazungumza kuhusu wokovu, katika nyakati tatu. Uliopita, uliopo, na ujao (past, present, and future). Ulipokuwa Mkristo kwa mara ya kwanza – uliokolewa; wokovu katika wakati uliopita. Unapoendelea kuishi maisha yako kwa sasa - unaokolewa. Unafanywa mtakatifu – wokovu katika wakati uliopo. Lakini, bado haujakamilika katika kuokolewa, kwa sababu katika wakati ujao, Yesu atakaporudi, utaokolewa. Wokovu wako utakamilishwa; wokovu katika wakati ujao. Na hiki ndicho **mst 5** unasema: “*Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu, kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa, wakati wa mwisho*”. Tuliokolewa. Tunaokolewa, na tutaokolewa. Wakati - uliopita, uliopo, na ujao. Jambo hili ni gumu sana kwetu kulielewa. Katika namna nyingi, wokovu ni fumbo – lakini ni ukweli wa ajabu, ambao unapaswa kutufanya tufurahi. Na tumeambiwa katika **mst 10-12** kwamba, manabii wa Agano la Kale, walichunguza kwa umakini ili kujua zaidi kuhusu wokovu huu. Shukrani kwa Mungu kwa mpango wa wake wa ajabu wa wokovu wetu! Tumezaliwa tena. Tunatumaini lililo hai. Tumeokolewa.

Kuna mstari moja zaidi, ambao nataka tuangalie, kabla ya hatujamaliza kipindi chetu mchana huu. **Mst 7**; swala la **imani** yetu. Katika **mst 6**, Petro anazungumza kuhusu majaribu mbali mbali, ambayo tutakutana nayo, katika maisha ya Kikristo – na baadaye katika masomo yetu, tutaangalia somo la mateso kwa Wakristo. Lakini katika **mst 7**, Petro anasema kwamba, majaribu tunayopitia, katika maisha yetu, yanatokea kwa sababu maalumu. Hivi ndivyo anavyosema: “*Majaribu haya yamewapata, ili imani yenu ipimwe*”. Kwanza, imani ni nini? Hatuna muda wa kutosha kuangalia swala hili kwa undani, lakini imani inaweza kuelezewa katika njia nyingi. Kama tunasema kwamba tuna imani katika Mungu, inamaana kwamba tunauhakika, na tumaini, katika yeye. Na imani hii, haitegemei uthibitisho. Angalia **mst 8** tena: “*Ingawa hammuoni Yesu sasa, mna amini katika yeye*”. Hii ni imani.

Kuamini na imani, yanaenda pamoja. Hatujawahi kumuona Yesu, lakini kupitia **imani**, tuna amini kwamba yupo. Hatuwezi kuthibitisha hili. Siwezi kukuonesha Yesu Kristo sasa, lakini Biblia inaniambia kwamba, Yesu alisulubiwa, na kufufuka kutoka kwa wafu – na nimechagua kuamini hivyo. Je, unakumbuka nini kilitokea Yesu alipowatokea wanafunzi, baada ya kufufuka kutoka kwa wafu? Wanafunzi walikuwa pamoja sehemu fulani katika Yerusalemu. Milango ya nyumba, ilikuwa imefungwa, kwa sababu walikuwa wamewaogopa Wayahudi. Na ghafla, Yesu akatokea mbele yao (Yohana 20:24). Lakini kulikuwa na mwanafunzi mmoja ambaye hakuwepo pale; **Tomaso**. Baadaye wanafunzi wakamwambia Tomaso: “*Tumemwona Bwana*”. Je, Tomaso alisema nini? “*Haiwezekani! Siwaamini. Mpaka nione makovu ya misumari katika mikono yake, na kuweka kidole changu katika makovu ya misumari, bila hivyo siwezi kuwaamini*”.

Kwa sababu Tomaso hakuweza kumwona Yesu mbele yake, hakuwa na imani ya kuamini maneno ya wanafunzi wenzake. Na watu wengi, ulimwenguni hata leo, hawaamini katika Yesu, kwa sababu hawawezi kumwona. Hawana imani katika Yeye. Basi, tunajua kilichotokea baadaye. Wiki moja baadaye, Yesu anawatokea tena wanafunzi wake, na safari hii, **Tomaso** yupo pale. Na Yesu anamwambia: “*Tomaso, usiwe na mashaka, ila amini. Weka kidole chako hapa – angalia mikono*

yangu na ubavu wangu". Na kisha Yesu anasema: "Wamebarikiwa wale, ambao hawajaniona, lakini wanaamini".

Na kwa hiyo, ukiamini katika Kristo leo, hata kama hujawahi kumwona kwa macho yako, Yesu anasema kwamba "**umebarikiwa**". Wewe ni mtu wa imani. **Waebrania 11:1** unasema hivi: "*Imani ni kuwa na uhakika wa mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana*". Na kadri tunavyoendelea kukua kama Wakristo, imani yetu katika Mungu pia inakua. Na kadri tunavyopitia majaribu, na mateso, imani yetu katika Mungu inapimwa. **Mst 7**: "*Majaribu haya yamewapata ili imani yenu ipimwe*". Majaribu haya ni kwa ajili ya kupima imani yenu tu, ili kuonesha kama iko imara, na safi. Kama Mungu angetaka, angeweza kuondoa majaribu kwetu kwa urahisi sana – lakini anaruhusu yatokee ili kupima imani yetu katika Yeye. Anatutaka tukue katika imani yetu. Anatutaka tumwamini zaidi na zaidi. Mambo yanapoenda vizuri katika maisha yetu, ni rahisi sana kumtumaini Mungu, sivyo? Lakini mambo yanapoenda vibaya, na maisha yanapokuwa magumu, ni vigumu kumtumaini Mungu. Na kwa hiyo, Mungu anaruhusu majaribu yatokee – kwa sababu anataka kuona kama tutaendelea kutumaini katika Yeye, wakati maisha ni magumu.

Lakini angalia Petro anasema nini, kuhusu imani yetu, katika **mst 7**: "*Imani yenu yenye thamani kuliko dhahabu. Imani yenu inajaribiwa kama dhahabu inavyojaribiwa, na kusafishwa, wakati inapo-thibitishwa kwa moto*". Moto unakatasa dhahabu. Ninafikiri neno ambalo limetumika, katika Biblia ya toleo la Union ni '*kujaribu*'. Lakini neno ambalo limetumika katika toleo langu la Kiingereza, ni '*kutakasa*'. Moto ni njia bora ya kutakasa, au kuthibitisha, **dhahabu**. Kwa hiyo, kama unataka kuifanya dhahabu iwe na thamani zaidi, utaiweka kwenye **tanuru** la moto mkali sana, na utaiyeyusha katika kimiminika. Uchafu wote utaumuka juu. Na unaweza kuuondoa uchafu. Mara baada ya kuondoa uchafu, utabaki na dhahabu safi. Lakini ili upate dhahabu halisi, inapaswa kupitishwa kwenye moto mkali sana, ambapo joto ni zaidi ya nyuzi elfu mbili! Hili ni joto kubwa sana! Unapochemsha maji, joto ni zaidi ya nyuzi **100** tu - kwa hiyo unaweza kupiga picha, ni jinsi gani joto ni kubwa unapoithibitisha dhahabu, au fedha.

Mungu anataka kuifanya imani yetu safi. Lakini ili afanye hivyo, anahitaji kuongeza joto. Anahitaji kuitakasa imani yetu. Kumbuka, anataka kutufanya watakatifu. Na hii inaweza kutupa maomivu sana, na isifurahishe kwetu. Huwa hatupendi sana majaribu yanapokuwa ya moto sana, sivyo? Lakini wakati mwingine, Mungu hutuweka kwenye moto, na anaruhusu tupitie majaribu, ili kwamba uchafu katika maisha yetu, uunguzwe. Na kupitia mchakato huu, uchafu unatolewa - na imani yetu inakuwa imara zaidi, safi zaidi, na yenye thamani zaidi. Tunakuwa watakatifu zaidi, na imani yetu inakua imethibitishwa kuwa halisi kabisa.

1 Petro 1:7: Majaribu yaliyokwenu yamekuja, ili kuijaribu imani yenu. Kumbuka hili, Petro anasema: imani yenu inathamani zaidi kuliko dhahabu, au fedha. Imani yenu inatakaswa, kama moto utakasavyo dhahabu. Na kama imani yenu itabaki imara, kupitia majaribu, basi hili linaleta sifa, na utukufu, na heshima kwa Yesu Kristo atakaporudi tena. Natumaini kwamba, jambo hili litatupa moyo, tunapopitia magumu. Shukrani kwa Mungu – kwa sababu tuna tumaini lililo hai; tumezaliwa tena; tuna urithi wa ajabu uliotunzwa mbinguni; tume-okolewa kwa damu ya Yesu, na Yeye anatu-takasa ili kwamba, tuwe kama Yeye.

KIPINDI 5: 1 Petro 1:17-2:3: “Ukombozi na Upendo”

Steve Lancaster

Hebu tufungue **1 Petro 1:17 - 2:3** **. Mistari hii imejaa mafundisho. Katika **mst 13**, Petro anatuambia kuandaa akili zetu, kwa ajili ya kitendo, na kuwa na kiasi. Anatuambia kuweka tumaini letu, katika neema ya Mungu. Katika **mst 17**, anatuambia kuishi katika hofu yenye heshima – na mwanzoni mwa sura ya pili, anatuambia “*wekeni mbali uovu wote, na hila, na unafiki, na husuda, na masingizio yote*”. Kwa hiyo, kuna mafundisho mengi sana hapa. Lakini pia kuna ukweli mwingi wa Biblia, ambao unajenga msingi wa ujumbe wa injili. Baadhi ya mistari, imejaa baraka za kiroho kwa ajili yetu - na itatufanya tujisikie kubarikiwa, na wenye shukrani kwa kile, tulichonacho katika Kristo. Sasa, ninataka tuangalie mambo mawili. Nini maana ya sisi kukombolewa kwa damu ya Yesu? **Mst 18 & 19**. Na kisha, nini maana ya kupendana kwa undani? **Mst 22. Ukombozi, na Upendo**. Kwa hiyo, kama anavyosema **Petro** katika **mst 13**, “*vifungeni viuno vya nia zenu*”, na jiandaeni kujisikia mmebarikiwa.

Angalia **1:18-19**: “*Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwanakondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo*”. Na ni neno hili ‘**ukombozi**’ ambalo nataka tuangalie sasa, pamoja na msaada wa baadhi ya mistari mingine, na pia kuna hadithi moja yenye nguvu, ambayo itatusaidia kuelewa maana ya neno hili. Hapa kuna mistari michache, ambayo napenda tusome pamoja: **Mathayo 20:28** “*Kama vile Mwana wa Adamu, asivyo kuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi*”. Kumbuka neno ‘**fidia**’. **1 Wakorintho 7:23** unasema hivi: “*Mlinunuliwa kwa thamani, msiwe watumwa wa wanadamu*”. Kumbuka neno ‘**nunuliwa**’. **Waefeso 1:7** unasema hivi: “*Katika yeye, tunaukombozi kupitia damu yake*”. Kumbuka neno ‘**ukombozi**’. **Fidia, nunuliwa, ukombozi** – maneno haya yote yana maana moja katika hadithi ya wokovu. Kwa hiyo, sasa, unapokumbuka maneno haya, ngoja ni waambie hadithi, ambayo natumaini itatusaidia kuelewa kikamilifu maana ya jambo hili. **

“*Sasa, wewe ni wangu mara mbili, kwa sababu nilikutengeneza, na nilikununua*”. Na hii ndiyo maana kamili ya ukombozi; malipo ya bei, au fidia ya kununua kitu fulani tena. Mvulana mdogo aliukomboza mtumbwi wake. Ingawa alikuwa ameutengeneza mtumbwi; ingawa ulikuwa wake, alipaswa kuulipia gharama; aliununua mtumbwi wake mwenyewe, na sasa ulikuwa wake tena. Katika Agano la Kale, kama mtu angekuwa mtumwa, kama matokeo ya kuchukuliwa mateka, angeweza kukombolewa, na ndugu wa karibu - lakini ingekuwa hivyo kama tu ndugu yule, alikuwa na nia ya kulipa gharama. Hii ilifanywa pia, kwa mtu aliyekuwa gerezani. Mfungwa angeweza kufunguliwa – lakini kama tu ndugu wa karibu, alikuwa na nia ya kulipa gharama. Ndugu alikuwa na uwezo wa kununua uhuru kwa ajili ya mtumwa. Mtumwa hakuwa na uwezo wa kufanya chochote, ili aupate uhuru wake - lakini ndugu alikuwa na uwezo huo. Katika Agano Jipya, maneno ‘*ukombozi, au kukombolewa, au fidiwa*’, yametumika kuelezea gharama, ambayo Yesu alilipa kwa ajili ya uhuru wetu. Kwa sababu ya anguko; kwa sababu ya uasi wa **Adamu** na **Hawa**, katika Bustani ya Edeni, wanadamu wote wakarithi dhambi. **Warumi 3:23** unasemaje? “*Wote wametenda dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu*”.

Kwa maneno mengine, wanadamu walikuwa katika soko la utumwa wa dhambi. Shetani alikuwa amewateka wanadamu, na uhusiano wetu na Mungu, ulikatwa. Wanadamu hawakuweza kufanya chochote, ili kujikomboa wenyewe kutoka dhambini; tusingeweza kufanya chochote, ili kukomboa uhusiano wetu na Mungu. Lakini kulikuwa na mtu mmoja, ambaye angeweza kufanya kitu kuhusu hili.

Mungu Baba alikuwa na mpango wa kutuweka huru, kutoka kwenye soko la utumwa – lakini ili afanye hivyo, alihitaji kulipa gharama. Na gharama hiyo ilikuwa kifo cha Yesu msalabani. Mungu alimtoa mwanaye pekee, ili kwamba tuweze kukombolewa. Katika Agano la Kale, ndugu wa karibu angeweza kulipa kiasi fulani cha pesa; angetumia fedha, au dhahabu, ili kumkomboa mtumwa, lakini Mungu alifanya hivyo kwa kulipa kitu cha thamani zaidi. **Mst 18** unasemaje? “*Mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu, mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa, mlioupokea kwa baba zenu*”. **Mst 19**: “*Bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo*”.

Mungu alilipa fidia ili akuokoe kutoka dhambini. Hakulipa kwa pesa – lakini alilipa kwa damu ya dhamani ya Yesu. Ingawa Mungu alituumba, bado alihitaji kulipa gharama, ili atununue tena, kutuokoa kutoka utumwa wa dhambi. Tusingeweza kufanya chochote kuhusu hili. Lakini Mungu, katika neema yake, na huruma yake, na upendo wake, aliamua kutununua tena – na kumtoa mwanawe pekee ili afe msalabani. Na sasa, kama yule mvulana mdogo aliyeununua mtumbwi wake, Mungu anaweza kusema “*sasa, wewe ni wangu mara mbili, kwa sababu nilikuumba, na nimelipa gharama ya kukununua tena*”. Je, hii inakufanya kujisikia vipi? Inapaswa kukufanya ujisikie kupendwa na Mungu. Inapaswa kukufanya ujisikie kushukuru, kushangazwa, na kubarikiwa. Na inapaswa kukufanya ujisikie kwamba, unahitaji kumtumikia yeye, kwa moyo wako wote. Kumbuka, kama **Paulo** anavyosema katika **1 Wakorintho** – “*mlikombolewa kwa gharama*”, na kwa wale ambao ni waumini wa kweli, sasa, ni wa Mungu. Na katika kuitikia upendo huu, tunapaswa kumpenda Mungu, na kumtumikia.

Ngoja twende kwenye **mst 22**, ambao unalenga juu ya somo la ‘**upendo kwa kila mmoja**’. “*Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo*” - pendaneni ninyi kwa ninyi. Sasa, kuanzia mwanzo, tunahitaji kufahamu ni upendo wa aina gani, ambao Petro anazungumzia. Hazungumzi kuhusu upendo wa mahaba, au upendo wa kimapenzi, kati ya mwanaume na mwanamke. Upendo ambao Petro anazungumzia hapa, na upendo ambao Yesu anazungumzia katika injili, ni upendo wa aina ya tofauti. Neno la Kigriki kwa upendo huu ni ‘**agape**’. Huu ni upendo unaotoka kwa Mungu. Upendo wa agape ni upendo wa kujitoa mwenyewe. Ni upendo usio na mashariti. Ni upendo wa kujitoa usio na mwisho. Ni kitendo cha nia, ambapo mtu anaamua kwamba, ataonesha upendo kwa mtu mwingine, hata kama upendo huo haujalipwa.

Sasa, ninahitaji kusema kwamba, somo la upendo wa agape, linaweza kutufanya tusijisikie vizuri. Kwa nini? Kwa sababu ni changamoto kubwa. Petro anasema kwamba, upendo tulionao kwa ajili ya ndugu zetu, unapaswa kuwa wa kweli; unapaswa kuwa halisi. Na sote tunajua kwamba katika kanisa, na miongoni mwa waumini wengine, wakati mwingine ni vigumu kupendana kwa undani. Kuna watu katika makanisa yetu, ambao wanaweza kutuudhi! Tunaweza hata kuona vigumu kuwapenda wachungaji na wainjilisti wengine! Wanaweza kuwa wamesema kitu fulani, kuhusu wewe ambacho siyo kweli. Wanaweza kuwa wamekufanyia kitu ambacho siyo kizuri - na kwa hiyo tunaona vigumu kuwa penda. Kwa hiyo, tunaposoma mstari kama huu, ambao unatuambia kupendana kila mmoja kwa undani, ni changamoto kubwa kwetu. Hata wamisionari wakati mwingine huwa wanaona vigumu kuwapenda wengine! Wakati mwingine, wale wanaopaswa kuwa watu wa Mungu, hushindwa kuonesha upendo wa Mungu kwa wengine. Kama Wakristo na wachungaji, tunajua kuhusu upendo wa Mungu, na huruma yake. Tunahubiri kuhusu upendo wa Mungu, lakini je, kweli huwa tunaonesha upendo wa Mungu kwa wengine? Hii ni changamoto kubwa. Na bado somo hili, limetajwa mara nyingi katika Agano Jipya.

Paulo alipokuwa anawaandikia **Wathesalonike**, katika barua yake ya kwanza (I Wathesalonike 4:9&10), alisema hivi: “*Katika habari ya upendano, hamna haja niwaandikie; maana ninyi wenyewe mmefundishwa na Mungu kupendana. Kwa maana mnafanya neno hili kwa ndugu wote walio katika Makedonia yote. Lakini twawasih, ndugu, mzidi sana*”. Wakristo hapa, walipendana kila mmoja; walikuwa wanatii amri ya Kristo, lakini Paulo bado anawaagiza kuendelea kupendana – na hiki ndicho kitu tunachopaswa kukifanywa kazi.

Kupendana kila mmoja ni vigumu, na tunahitaji msaada wa Mungu, ili tuweze kufanya hivyo. Mtume **Yohana** ameandika mara nyingi sana, kuhusu upendo katika injili yake, na barua zake, na kama utafungua injili yake, **sura 13**, utaona kwamba, kuna mistari miwili maarufu sana, ambayo walipewa wanafunzi katika Chumba cha Juu. **Yohana 13:34-35**. Natumaini mnajua vizuri mistari hii. “*Amri mpya nawapa: mpendane. Kama vile lilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo; hivyo watu wote watatambua yakuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu*”.

Je, unagundua nini kuhusu mistari hii miwili? Mara tatu Yesu anasema maneno ‘*pendaneni*’. Petro anasemaje katika **1 Petro 1:22**? Anatumia maneno haya haya: ‘*pendaneni*’. Kumbuka kwamba, Petro alikuwepo katika Chumba cha Juu, wakati Yesu aliposema maneno haya - na kwa hiyo, labda anapoandika barua hii, anafikiri kuhusu wakati, ambapo Yesu aliwaambia kupendana. Anataka kuisisitiza amri ya Yesu, kwa sababu anajua kwamba, amri hii ni muhimu sana katika kanisa. Na hii siyo sehemu pekee, ambayo Petro anazungumza kuhusu kupendana. Katika **1 Petro 2:17** Petro anatumkumbusha: “*Wapendeni ndugu*”. Na kisha katika **1 Petro 4:8**: anasema tena: “*zaidi ya yote, iweni na juhudi nyingi katika kupendana*”. Somo hili lilikuwa muhimu sana kwa Yesu, na pia lilikuwa muhimu sana kwa Petro – na kwa hiyo, ni muhimu sana kwetu leo.

Hebu rudi katika **Yohana 13:34**, kwa sababu kuna kitu muhimu ambacho tunahitaji kukijua. Je, mfano wetu ni nani? Je, huwa tunamwangalia nani, tukitaka kujua jinsi ya kupendana? Yesu anawaambia wanafunzi wake: “*nataka mpendani ninyi kwa ninyi – kama mimi nilivyo wapenda ninyi*”. Fikiri kuhusu mstari huu. Yesu aliwaambia kupendana, kwa namna ile ile alivyoonesha upendo kwao. Kisha alisulubiwa msalabani kwa ajili yao, na kwa ajili yetu pia, akituonesha ni kwa kiasi gani alitupenda sisi. Upendo wake ni mkamilifu. Upendo wake hauna mashariti. Upendo wake ni wakujitoa – amejiandaa kufa kwa ajili yetu, kwa sababu upendo wake ni wa kina; upendo wake ni wa uaminifu. Na Yesu anasema – ninataka mpendane hivyo hivyo, kama nilivyowapenda ninyi. Hili linawezekana? Kama wanadamu wenye dhambi, je, inawezekana kupendana sisi kwa sisi, kama vile Yesu alivyotupenda sisi? Hapa kuna jibu: kwa nguvu zetu, hapana – lakini katika nguvu ya Roho Mtakatifu, ndiyo.

Hatuwezi kupendana kama Yesu, kama tutajaribu kufanya hivyo kwa nguvu zetu wenyewe. Kila mara tutashindwa. Lakini tukiwa na Yesu akiishi ndani yetu, tunaweza kufanya. Kama tutaendelea kutembea pamoja na Roho Mtakatifu, na kama tutaaruhusu upendo wa Mungu kutujaza – basi tuta-wezeshwa kutii amri hii ya Yesu. Ngoja nithibitisha wazo hili. Je, unakumbuka kitu gani kilikuwa kimetokea katika Chumba cha Juu? Kabla ya chakula kupakuliwa, na kabla ya Yesu kuosha miguu ya wanafunzi wake, kuna mjadala kati ya wanafunzi. Luka anatumambia jinsi mjadala huo ulivyokuwa.

Luka 22:24 unasema hivi: “*Yakatokea mashindano kati yao, kwamba ni nani anayehesabiwa kuwa mkubwa*”. Je, unaweza kuamini hii? Huu ni mlo wa mwisho ambao Yesu atakula, kabla ya kwenda msalabani. Anataka kutumia muda pamoja na wanafunzi wake – lakini, wao wanataka kushindana kuhusu nani ni mkubwa!

Ni kama kundi la wachungaji wakibishana kwamba yupi ni mchungaji bora kuliko wengine! Mchungaji mmoja anasema: “*mimi ni mchungaji bora katika dayosisi*”, na mwingine anasema, “*hapana, mimi ndiye mchungaji bora; mimi ni wa muhimu zaidi, kwa sababu mimi ni rafiki wa karibu wa askofu*”. Na kisha mchungaji mwingine anasema: “*Hapana, wote mmekosea. Mimi ndiye mchungaji mkuu; nilipitia chuo cha Biblia, ninauzoefu mwingi, na mimi ni muhubiri bora!*” Je, haya yanatokea katika makanisa leo? Katika Chumba cha Juu, Yesu anataka kusema kwa wanafunzi wake. “*Acheni kufanya kama watoto! Ninataka muwe watu wanaotumika, kama mimi nilivyowatumikia ninyi, na ninataka mpendane ninyi kwa ninyi, kama mimi nilivyowapenda ninyi*”.

Lakini tambua kilichotokea kwa wanafunzi hawa, wiki chache tu baadaye. Katika **Matendo 2:44-47** kanisa la mwanzo lilikuwa linaendelea kukua, na tumeambiwa kwamba **. Tambua kwamba yamekuwepo mabadiliko makubwa sana hapa! Hakuna ubinafsi sasa! Hakuna anayesema ‘*mimi ni bora kuliko wewe*’. Badala yake, tuna maneno kama ‘*pamoja, kushirikiana, furaha, uaminifu*’ – na ninafikiri tunaweza kuongeza neno ‘*upendo*’ katika orodha hii. Je, kwa nini kumetokea mabadiliko, katika kipindi cha majuma sita tu? Kwa nini wanafunzi katika kanisa la mwanzo, waliweza kuishi namna hii, ambapo majuma sita kabla, walikuwa wakibishana kila mmoja? Neno moja: Pentekoste! Au maneno mawili: Roho Mtakatifu! Yesu amepaa mbinguni, na Roho Mtakatifu amekuja kwa nguvu juu yao, na kuwapa nguvu ya kupendana. Hapakuwa na namna ya kuwafanya wapendane kwa nguvu zao – lakini katika nguvu za Roho Mtakatifu, waliweza.

Kadri walivyojikabidhi kwa Yesu katika utii, na kadri walivyo mruhusu Roho Mtakatifu kuongoza maisha yao, ndivyo walivyoweza kupendana wao kwa wao. Kirai cha mwisho, katika **Matendo 2** kinasema: “*wakapendwa na watu wote*”. Kwa maneno mengine, watu nje ya kanisa, walivutiwa nao. Watu walitazama kundi hili la Wakristo, na wakatambua kwamba walikuwa watu tofauti – na walipendezwa na kile walichokiona. Waliona namna walivyomwabudu Mungu, katika hekalu, na walitambua kwamba Wakristo hao, walionekana kupendana. Na matokeo yake, watu wengi zaidi na zaidi, wakaanza kuwa Wakristo, na kujiunga na kanisa la mwanzo. Na hapa, unaweza kuona sababu mojawapo ya sisi, ‘*kupendana sisi kwa sisi*’ - ni kwa ajili ya kusudi la uinjilishaji. Hebu rudi katika maneno la Yesu, katika **Yohana 13:35**: “*Hivyo watu wote watatambua yakuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi*”. Kwa maneno mengine, Yesu anasema, kadri mtakavyopendana ninyi kwa ninyi, watu watafutwa kwangu. Hawataweza kupuuza kwamba ninyi ni wanafunzi wangu – watatambua na kuvutwa kwangu, kupitia upendo. Unaona, upendo ni kuwa na alama ya mfuasi wa Kristo, na tumaini ni kwamba ulimwengu huko nje; wale wasio Wakristo, wataona namna, ambavyo tunapendana sisi kwa sisi, na kuvutwa kanisani.

Nina maswali kadhaa ya changamoto kwako. Je, unawapenda watu katika kanisa lako? Je, unafikiri kwamba, unafahamika kama mchungaji anayewapenda watu wake? Je, vipi kuhusu kanisa lako? Je, unafikiri kwamba kanisa lako linajulikana kwa upendo wake? Je, watu wa kanisa lako huoneshona upendo wao kwa wao, na pia kwa watu walio nje ya kanisa? Je, unafikiri kwamba AIC inajulikana kama dhehebu lenye upendo? Haya ni maswali magumu! Unaona, injili yote ni kuhusu upendo. Kumbuka alichosema **Paulo** katika **1 Wakorintho 13:13**: “*Basi, sasa inadumu: imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo, lililo kuu ni upendo*”. Kama Wakristo, wachungaji, na kanisa, hawaoneshi upendo kwa kila mmoja, basi kitu fulani hakiko sawa! Kama hatuna upendo – basi sisi si kitu chochote. Hivi ndivyo Paulo anavyosema kuhusu upendo katika kifungu hiki, katika **1 Wakorintho 13** **

Katika **1 Petro 1:22** tumeambiwa kwamba, “*tuwe na upendo wa ndugu usio na unafiki, na kwamba tupendane sisi kwa sisi kwa moyo*”. Hii pia ni amri ya Yesu. Lakini tunawezaje kufanya

hivyo? Tunahitaji kumwagalia Yesu aliye mfano wetu. Tunahitaji kuendelea kutembea na Roho Mtakatifu, na kumruhusu atawale maisha yetu. Tunahitaji kukaa ndani ya mzabibu – kwa sababu kadri tunavyofanya hivyo, ndivyo tunavyo tayarishwa, na kuimarishwa, ili kuonesha upendo kwa wengine. Lakini hii inahitaji uvumilivu na bidii. Ili tupendane sisi kwa sisi, kuna haja ya kuwa na nidhamu katika maisha yetu ya kiroho. Kama tukiipuuza misingi ya nidhamu ya kiroho, basi ujumbe wa upendo katika maisha yetu utaharibika. Tunahitaji kutumia muda katika Neno la Mungu kila siku. Tunahitaji kula upendo wa Mungu. Tunahitaji kuloanishwa kwa injili ya neema, na tunahitaji muda wa mara kwa mara wa kutiwa nguvu. Na kama tutashindwa kufanya mambo haya, basi tutaona vigumu zaidi na zaidi, kutii amri hii, ya kupendana sisi kwa sisi.

1 Wathesalonike 3:12: “*Bwana na awaongeze, na kuwazidisha katika upendo, ninyi kwa ninyi, na kwa watu wote, kama vile sisi nasi tulivyo kwenu*”.

KIPINDI 6: 1 Petro 2:4-12: “Kristo – jiwe lililo hai, jiwe la pembeni, jiwe la kujikwaa” (1)
Steve Lancaster

Fungua **1 Petro 2** na tutasoma **mst 4-12**. Kristo – Jiwe lililo hai, jiwe la pembeni, jiwe la kujikwaa. Ninafikiri kwamba Petro alipoandika ujumbe huu, kulikuwa na tabasamu kubwa, juu ya uso wake – kwa sababu nafikiri, labda alikuwa anakumbuka mara ya kwanza alipokutana na Yesu. Je, unaikumbuka hadithi hii? Simoni Petro alipokutana na Yesu mwanzoni mwa huduma yake. Katika injili ya **Yohana 1:41** tumeambiwa kwamba, **Andrea** alienda kumtafuta **Simoni** – na akamwambia “*tumemwona Mesia*”. Na kisha Andrea akampeleka Simoni kwenda kukutana na Yesu. Na Yesu alimwambia: “*Najua kwamba jina lako ni Simoni, lakini nitakupua jina jipya. Utaitwa Kefa*”. Na katika lugha ya Kiaramu, neno ‘Kefa’ linamaana ya ‘mwamba’, lakini tunapolitafsiri katika Kigriki, tunapata neno ‘Petro’, ambalo linamaana ya ‘jiwe’. Hilo lilikuwa jina ambalo Yesu alimpa Simoni. Simoni mwamba; Simoni jiwe.

Kwa nini alimwita hivyo? Unaposoma injili, utagundua kwamba Petro hakuwa kama mwamba. Hakuwa mtu wa kutegemewa na kuaminika. Hakuwa imara. Na kwa kweli, jina la ‘*Simoni*’ linamaana ya ‘*matete*’; aina ya mmea unaopatikana karibu na maji. Siyo mmea wenye nguvu. Ni mmea unaoinama kwenye upepo, na ni rahisi kuvunjika. Na kwa hiyo, jina la ‘*Simoni*’ lilimfaa sana, wakati wa kipindi chake cha mwanzo, kwa sababu hakuwa imara. Lakini tunaposoma kitabu cha **Matendo**, tunamwona Petro aliye tofauti. Sasa amekuwa kama mwamba kweli kweli. Amebadilika kwa sababu ya nguvu za Roho Mtakatifu ndani yake. Amekuwa mmoja wa viongozi wakuu katika kanisa la kwanza; ni miongoni mwa mawe ya msingi katika kanisa; alikuwa kiongozi imara. Lakini, unapofikiria kuhusu jambo hili, inashangaza kwamba, Yesu alimpa jina hili – kwa sababu, sasa, wakati Petro anaandika barua yake, anaamua kumwita Yesu ‘jiwe’. **Mst 4:** “*Mmwendee yeye, Jiwe lililo hai, lililo-kataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima*”. Hapa ni Yesu Kristo, ambaye ni Jiwe lililo hai – na siyo Simoni Petro.

Sasa, inaweza kuonekana kitu cha ajabu, kumlinganisha Yesu na **jiwe** au **mwamba**, kwa sababu tunajua kwamba, mawe ni vipande tu katika vitu vigumu kutoka kwenye udongo. Jiwe halina uhai wowote. Ni kitu kilichokufa. Haliwezi kupumua. Haliwezi kuongea. Haliwezi kujongea lenyewe. Na bado inavutia kusoma kwamba watu wengi katika uliwengu, wanaamini kwamba baadhi ya mawe na miamba vina uhai, na nguvu za kishirikina. Huko **Australia** – kuna mwamba mkubwa sana, unaitwa **Ayres Rock**. Una urefu zaidi ya meta **300** kwenda juu. Kama ungetaka kutembea kuzunguka mwamba huo, ungehitaji kutembea umbali wa kilometa **8**! Huu ni mwamba mkubwa

sana! Watu wa asili, walioitwa “*aborigine*”, wanaamini kwamba mwamba huo ni mtakatifu, na kwamba una nguvu; wanaamini kwamba uko hai.

Waislamu wanapotembelea **Makka**, huwa wanatembea kuzunguka jengo kubwa, linaloitwa ‘*Kaaba*’. Katika jengo hilo, kuna kitu kinachoitwa **jiwe jeusi**. Waislamu wanaamini kwamba, jengo hilo ni takatifu kuliko maeneo yote katika Uislamu. Wanasema kwamba, jiwe hili lilianguka kutoka mbinguni, ili kumwonesha **Adam na Eva** mahali pakujenga madhabahu ya kwanza. Baadhi ya Waislamu wanafikiri kwamba, jiwe hilo linanguvu ya kusamehe dhambi. Wanapotembea kuzunguka jengo hilo, wanapita kati kati ya jiwe hilo, wanajaribu kuligusa na kulibusu, kwa sababu wanafikiri kwamba linauhai na nguvu. Lakini kwa kweli, tunajua kwamba miamba haina uhai. Haina nguvu za kufanya kitu chochote; inabaridi na ni migumu; haiwezi kuongea - au kujongea yenyewe; ni vipande vya vitu vilivyo kufa tu. Kwa hiyo, kwa nini Petro anamzungumza Yesu kama ‘*jiwe*’? Utagundua katika **mst 4**, Petro anaweka kivumishi muhimu sana mbele ya neno ‘*jiwe*’. Jiwe hili ni tofauti! “*Mmwendee yeye, Jiwe lililo hai*”. Petro anataka kuwakumbusha wasomaji wake kwamba, hawamwabudu mtu fulani aliyekufa.

Hawamwabudu mtu fulani, ambaye bado amezikwa katika kaburi la jiwe – bali wanaabudu Jiwe lililo hai, ambalo lilifufuka kutoka wafu, na liko hai kabisa! Yesu Kristo ni **Jiwe lililo hai**! Kwa kweli, unaposoma Biblia, utaona kwamba **Mungu Baba** pia ameelezwa kama mwamba - kwa sababu miamba na mawe, vina tabia fulani ya kufanana na Mungu na nguvu zake. Mungu ni wa milele – kama mwamba. Hawezi kusogezwa – kama vile jiwe kubwa. Katika **Mwanzo 49 mst 24**, Mungu ametajwa kama “*mwamba wa Israeli*”. **Zaburi 18:2** inasema hivi: “*Bwana ni jabali langu, na boma langu, na mwokozi wangu, Mungu wangu, mwamba wangu, ninayemkimbilia*”. Na sikia maneno haya, kutoka **Kumbukumbu la Torati 32:4**: “*Yeye Mwamba, kazi yake ni kamilifu, Maana, njia zake zote ni haki*”. Hapa katika **1 Petro 2**, Petro hataki tumfikiria Yesu kama vipande vya mawe vilivyokufa - bali anataka tumfikiria Yesu kama Jiwe lililo hai, ambaye ni wa milele, wa kutegemewa, na imara. Yesu ni mtu ambaye juu yake maisha yetu yanaweza kujengwa, kama mjenzi anavyojenga nyumba yake, juu ya msingi imara.

Je, unajua kuna kifungu kingine katika Agano la Kale, ambacho kinataja mwamba ambao kwa kweli kinahusu Yesu Kristo? Je, unamkumbuka mflame **Nebukadneza** katika kitabu cha **Danieli**? Usiku moja aliota ndoto yenye nguvu sana – na alichoona katika ndoto kilimsumbua sana. Na kwa hiyo, aliwaita washauri wake, lakini hakuna hata mmoja wao aliyeweza kutoa tafsiri ya ndoto hiyo. Katika ndoto, kulikuwa na sanamu kubwa. Biblia inasema kwamba, ilikuwa ya ajabu sana katika mwonekano wake (Dan 2:31). Kichwa chake kilikuwa cha dhahabu. Kifua na mikono vilikuwa vya fedha. Tumbo na miguu vilikuwa vya shaba. Miguu ilitengenzwa kwa chuma, na nyao za miguu yake, zilichanganywa kwa chuma na nusu ya udongo.

Danieli 2, inatambia kwamba mfalme alipokuwa akiangalia sanamu ile, mwamba uliokuwa umekatika kutoka kwenye mlima, ghafla ukaipiga ile sanamu katika miguu. Sanamu yote ikaanza kusambaa, na ikaharibiwa. **Danieli 2:35** unasema hivi: “*lile jiwe lililoipiga hiyo sanamu, likawa mlima mkubwa, likaijaza dunia yote*”. Kisha Danieli akamweleza mfalme maana ya ndoto hiyo. Sanamu inawakilisha falme mbali mbali, ambazo zitakuja kushindwa. Lakini katika kipindi cha mwisho wa ufalme, ufalme wa **Roma**, Mungu wa mbinguni atasimamisha ufalme, ambao hautashindwa, na utadumu milele. Je, nani ni mwamba katika kifungu hiki? Ni Yesu Kristo. Hiki ni kifungu katika Agano la Kale, ambacho kinatabiri kuja kwa Mesia katika ulimwengu. Mwamba ni Yesu, na ufalme wake utakua ili uijaze dunia yote. Yesu ni Jiwe lililo hai!

Sasa, sijui kama Petro alifikiri kuhusu kifungu hiki katika Danieli, wakati alipoamua kumzungumza Yesu kama jiwe – sijui. Lakini utaona katika kifungu chetu katika **1 Petro 2:6,7,8** kwamba Petro anatomia vifungu vitatu, kutoka Agano la Kale, ambavyo vinazungumza kuhusu mawe; kumzungumzia Yesu Kristo. Katika **mst 6**, Petro anamwelezea Yesu kama **jiwe la pembeni**, na anatomia mstari kutoka kitabu cha **Isaya**. Kumbuka Isaya alikuwa nabii miaka **700**, kabla ya wakati wa Yesu, na bado, Mungu alimwezesha kuona mambo ya wakati ujao, wakati Mesia atakapokuja. Na mstari ambao Petro anatomia, ni **Isaya 28:16**: “*Tazama, naweka jiwe katika Sayuni, liwe msingi, jiwe lililojaribwa, jiwe la pembeni lenye thamani, msingi ulio imara; yeye aaminiye hatafanya haraka*”. Kwa hiyo – Yesu ni Jiwe lililo hai. Na pia Yesu ni jiwe la pembeni – lakini jiwe la pembeni ni nini hasa? Jiwe kubwa la pembeni ni jiwe la kwanza kuwekwa. Ni jiwe la muhimu zaidi katika jengo zima. Ni jiwe maalumu – linapaswa kuwa na ubora wa hali ya juu; linapaswa kuwa linalolingana, na kuwa mraba, kwa sababu mawe mengine yote yanapimwa na hili jiwe. Jiwe kubwa la pembeni linaweka nyuzi sahihi, kwa ajili ya mawe mengine yote katika jengo zima. Kama jiwe hilo halijanyoka katika incha zake, na kama halijakaa vizuri katika msingi, mawe mengine pia hayatakaa vizuri – kuta zitakuwa zimepinda – zitakuwa shaghalabagala!

Kwa sababu jiwe hili ni muhimu sana katika jengo, mara zote huwa ni jiwe kubwa sana, na waashi wako makini sana wanapoweka jiwe hili katika sehemu yake. Wakati Petro anapozungumza kuhusu Yesu kuwa ‘*jiwe la pembeni*’, ninafikiri kwamba anafikiri pia kuhusu hekalu katika Yerusalemu. Mawe ambayo yalitumika kujenga hekalu yalikuwa makubwa sana – na baadaye, mfalme **Herode** alipoamua kujenga kuta kulizunguka hekalu, mawe aliyotumia pia, yalikuwa makubwa sana. Hata leo, kama utatembelea Yerusalemu, unaweza kuona kuta hizo, ambazo Herode alijenga kuzunguka hekalu. Hekalu kati kati – sasa halipo. **Waroma** walilibomoa miaka **40** baada ya Yesu. Lakini kuta ambazo Herode alijenga, bado zipo hadi leo. Na ukubwa wa matofali ya mawe unashangaza sana.

Wakati wa huduma ya Yesu, Petro na wanafunzi wengine, walilifahamu vizuri eneo la hekalu. Walilijua vizuri kwa sababu walilitembelea mara nyingi. Wakati wa kanisa la mwanzo, Petro na waumini wengine, walitumia eneo la hekalu kama sehemu ya kukutania. Kwa hiyo, Petro anapoandika burua hii, ninafikiri kwamba alikuwa anafikiri kuhusu unabii wa **Isaya**, na mmekumbushwa kuhusu mawe haya makubwa katika eneo la hekalu, na hasa hasa, mawe makubwa ya pembeni. Labda pia, amekumbuka wakati Yesu alipozungumza kuhusu mawe haya, katika eneo la hekalu. Fungua **Marko 13:1**: “*Yesu alipokuwa anatoka hekaluni, mmoja wa wanafunzi wake walimwambia, Mwalimu, tazama jinsi mawe haya na majengo haya yalivyo ya ajabu!*” Na unaweza kupiga picha katika akili, Petro amesimama pale, akiangalia mawe haya makubwa sana! Lakini, Yesu anasema nini? **Mst 2**: “*Je, unayaona majengo haya makubwa? Hakuna hata jiwe moja litakalosalia juu ya lingine; kila kitu kitabomolewa*”. Hili lilikuja kutimia wakati hekalu lilipobomolewa na Waroma. Hekalu lote lilibomolewa kabisa.

Petro alijua vizuri namna jiwe la pembeni lilivyo, kwa sababu alikuwa ameyaona katika hekalu. Alijua jinsi yalivyo makubwa. Alijua jinsi jiwe la pembeni lilivyo muhimu - lakini wazo analotaka kusisitiza hapa, katika mstari wa **sita**, ni kwamba Yesu ni jiwe kuu la pembeni. Ni jiwe kubwa zaidi la pembeni. Yeye ni msingi wa imani yetu. Yeye ni kitu cha muhimu zaidi katika maisha yetu. Yeye ni jiwe kubwa katika jengo, na kila kitu tunachofanya kimejengwa juu yake. Na baadaye, tutaangalia **mst 5 & 9**, ambayo inataja kuhusu waumini kuwa mawe katika jengo la kanisa. Kwa sasa, tutalenga juu ya Yesu kama jiwe. Je, Mungu anasema nini kwa Isaya? “*Tazama, naweka jiwe katika Yerusalemu, liwe msingi, jiwe lililojaribwa, jiwe la pembeni lenye thamani, msingi ulio imara; yeye aaminiye hatafanya haraka*”. Na hapa tuna ahadi ya ajabu sana! Kama unaamini

katika Yesu, na kama unaendelea kuwa na Yesu; kama jiwe la pembeni katika maisha yako, hautaibika; hautavunjika moyo. Yeye hawezi kukuangusha.

Lakini angalia pia kuna kitu kingine, katika mstari huu, kuhusu jiwe hili la pembeni. **Mst 6:** ni jiwe teule, na la thamani. Katika **mst 4** tumeambiwa kwamba, Jiwe lililo hai ni la thamani kwa Mungu. Katika **mst 6** tunaona kwamba, jiwe la pembeni limeelezwa kama jiwe la thamani, na kisha katika **mst 7**, tunasoma kwamba “*kwa watu wanaoamini, jiwe hili ni la thamani*”. Mara tatu katika mistari mi-nne, tunaliona neno hili ‘*thamani*’ au ‘*heshima*’. Je, Petro anataka tutambue nini hapa? Jibu linajulikana – anataka tujue kwamba - Yesu ni wa thamani. Yeye ni kito cha thamani. Katika sehemu za Afrika, chini ya ardhi, kuna madini mbali mbali, na vito vya thamani. Baadhi yake yana thamani ya fedha nyingi sana. Yanaitwa vito vya thamani, na yanopochimbwa kutoka chini, yanaweza kusafishwa, na kufanywa kuwa vito. Katika **Kutoka 28** unaweza kusoma kuhusu vito, ambavyo vilitumika kushona nguo, ambazo kuhani **Haruni** alivaa. Inataja **topazi**, na **amethisto**, na vingine vingi. **Almasi** ni vito vya thamani – na baadhi yake vinathamani ya fedha nyingi sana – almasi moja ndogo inaweza kugharimu maelfu ya dola.

Hapa Tanzania, mna vito vya thamani, vinaitwa **Tanzanite**, ambavyo vinaweza kupatikana mkoa wa Manyara pekee. Na vito hivi vinauzwa ulimwenguni kote. Baadhi ya vito hivi ni vya thamani kubwa sana. Kama una miliki moja, unahitaji kuwa makini sana. Unapaswa kuweka katika sehemu ya siri, kwa sababu hutataka wezi wakuibie. Ni ya thamani sana. Hapa kuna swali! Petro anasema kwamba, kwa wale wanaoamini, Jiwe lililo hai ni la thamani sana. Wakati mwingine, tunahitaji kuyapima maisha yetu, na tunahitaji kujiuliza wenyewe, Yesu ni wa thamani kiasi gani kwangu? Je, Yesu ana thamani gani? Je, tunaishi maisha yetu kama kwamba yeye ni wa thamani kuliko vitu vyote tulivyonavyo? Je, Yesu ni wa thamani kiasi gani kwako leo? Katika makanisa nchini Uingereza, wakati mwingine, huwa wanaimba wimbo unaotaja jinsi Yesu alivyo wa thamani. Hebu sikiliza maneno haya: “*Bwana, wewe ni wa thamani kuliko fedha. Bwana, wewe ni wa thamani kuliko dhahabu. Bwana, wewe ni mzuri kuliko almasi, na sina kitu cha kukufananisha na wewe*”. Je, maneno haya ni ya kweli kwako wewe? Je, maneno haya ni ya kweli kwangu mimi? Wakati mwingine ni rahisi kuimba maneno ya wimbo, lakini ni vigumu kuyamaanisha katika moyo wako. Je, Yesu ni wa thamani zaidi kwako kuliko kitu chochote katika maisha yako?

Je, unakumbuka mfano, ambao Yesu aliwaambia wanafunzi wake, kuhusu hazina, ambayo ilikuwa imefichwa shambani? Mfano unaelezea jinsi ufalme wa mbinguni ulivyo wa thamani. Lakini, kwa kuwa Yesu mwenyewe, ni mfalme wa ufalme huo, na kwa kuwa Yeye ndiye anayeufanya uwe wa thamani, mfano huo pia unamuhusu yeye. **Mathayo 13:44**. Unasema hivi: “*Ufalme wa mbinguni umefanana na hazina iliyositirika katika shamba, ambayo mtu alipoiona, aliificha*”. Kwa nini aliificha? Alijua kwamba hazina hiyo ilikuwa ya thamani – hakutaka mtu mwingine aione. Alijisikia furaha kubwa kuiona hazina. Kwa hiyo, aliamua kuuza vitu vyote alivyonavyo, na pesa aliyopata, alienda kununulia shamba hilo. Alikuwa na furaha kuuza kila kitu alichonacho, kwa sababu alijua kwamba hazina katika shamba ni ya thamani zaidi. Ni mfano rahisi kuelewa. Yapasa Yesu awe wa thamani zaidi katika maisha yako. Je, unaweza kumwamini na kumpa vyote ulivyonavyo, ili kwamba awe wa thamani kuliko vitu vyote?

Je, kweli Yesu ni wa thamani kwako? Je, Yesu ni wa thamani kwa watu katika kanisa lako? Au, ngoja niulize swali katika namna nyingine. Je, Yesu ni kitovu cha kanisa lako? Au, watu wamemweka pembeni – kando ya njia? Inasikitisha, katika makanisa mengi, Yesu siyo kitovu. Kama hatuko makini, vitu vingine katika ibada zetu, vitakuwa vya muhimu zaidi, na Yesu hatapata heshima anayopaswa kupewa. Je, katika kanisa lako, Yesu ni wa thamani? Mwalimu mmoja wa Biblia alisema hivi: “*Kama hutahisi jinsi Yesu alivyo wa thamani; kama hutahitaji kama vile mtoto*

mchanga anavyohitaji maziwa, basi kuna haja ya kupima imani yako. Je, mizizi yako inagusa chini kwenye jiwe la msingi la Yesu? Au inasambaa kwenye tabia ya miamba mikavu, utamaduni, na desturi? Je, unamsukumo wa shauku ya kuwa naye? Au unamsukumo wa matarajio ya familia, majukumu, na shughuli za mazoea ya kanisa?”

Katika **mst 4**, tunasoma kwamba Yesu ni wa thamani kwa Mungu Baba. Katika **mst 7**, Petro anasema kwamba, Yesu ni wa thamani kwa wale wanaoamini katika yeye. Je, Yesu ni wa thamani kwako – na Je, maisha yako yanaonesha hivyo? Tumeona kwamba Yesu awe Jiwe lililo hai, na pia Yeye awe jiwe la pembeni. Yeye ni jiwe la thamani kwa wale wanaoamini katika Yeye. Lakini tambua pia, katika **mst7** kwamba baadhi ya watu hawafikiri kwamba Yesu ni jiwe la thamani, badala yake, hawampendi na wamechagua kumkataa. *“Jiwe walilo likataa waashi imekuwa jiwe la pembeni”*. Na maneno ambayo Petro anatumia hapa, yametoka **Zaburi 114: 22**. Pia Yesu anatumia maneno haya haya, anapowasimulia Mafarisayo mfano wa watumwa. Anatumia maneno haya kujielezea mwenyewe. Anawaambia – mimi ni jiwe la pembeni, lakini ninyi mmenikataa. Paulo pia anatumia maneno haya haya, katika kitabu cha **Waroma 9**.

Petro pia ametumia maneno haya katika sehemu nyingine – katika kitabu cha **Matendo 4**. Je, unakumbuka wakati Mafarisayo walipomkamata Petro na Yohana, katika eneo la hekalu? Walikuwa wakifundisha kuhusu Yesu, na watu wengi wakamwamini Yesu – lakini viongozi Wayahudi hawakupenda. Hata hawakuwa nafuraha kwamba Petro na Yohana, walikuwa wamemponya omba omba, mwenye ulemavu katika mlango wa hekalu! Kwa hiyo, waliwaweka gerezani, na siku iliyofuata, wakawaleta mbele ya mahakama. Viongozi wa Wayahudi wakamuliza Petro na Yohana: *“kwa mamlaka gani mnafanya mambo haya”?* Na Petro, akijawa na Roho Mtakatifu, akajibu: *“Tunafanya mambo haya katika jina la Yesu Kristo, ambaye ninyi mlimsurubisha, bali Mungu akamfufua kutoka wafu”*. Na kisha Petro anatumia mistari hii, kutoka **Zaburi 118**, na anasema: *“Jiwe mlilolikataa ninyi waashi limekuwa jiwe la pembeni”*. Tambua, hapa anawaambia moja kwa moja: *“jiwe mlilolikataa ninyi waashi”*. Petro hapa anazungumza na viongozi wa Wayahudi – uso kwa uso! Nafikiri kwamba Mafarisayo, na Makuhani, hawakuwa na furahia kabisa – hasa Petro anaponukuru kutoka Agano la Kale, ili kuelezea wazo lake. Inashangaza, katika nguvu za Mungu, mwisho wa kifungu, Petro na Yohana wameachiwa huru kutoka gerezani. *“Jiwe walilolikataa waashi limekuwa jiwe la pembeni”*.

Lakini tambua kwamba, katika **mst 8**, jiwe hili ni kitu kingine pia. Kwa wale waliomkataa Yesu, na hawaamini katika Yeye – amekuwa **jiwe la kujikwaa**. Na safari hii, Petro anarejea nyuma katika kitabu cha **Isaya**, na kunukuru kutoka **sura 8:14**. Yesu ni: *“jiwe la kuwafanya watu wajikwae, na mwamba wa kuwaangusha”*. Ninahakika kwamba wote mnajua jinsi unavyoweza kujisikia ukijikwaa kwenye kitu fulani! Labda uliutembea katika mtaa, huku ukimwandikia mtu ujumbe kwenye simu yako, na huoni ni kitu gani kipo kwenye njia – na kwa hiyo ulijikwaa kwenye jiwe! Labda, kama una watoto wadogo nyumbani, umewahi kujikwaa juu ya mojawapo ya midori, ambayo ilikuwa imeachwa juu ya sakafu. Labda, umewahi kujigonga mguu wako kwenye meza, au kiti, wakati ulitembea kwenye nyumba – na inaumiza sana! Wote tunajua jinsi unavyoweza kujisikia pale ukijikwaa kwenye kitu fulani, na kama unaanguka chini, unaweza kusimama ukiwa umeumia sana. Katika siku za Yesu, Mafarisayo walimkataa Yesu – hawakumkubali kama jiwe la pembeni. Hawakumwona kama alivyokuwa. Kwa maneno mengine, katika namna ya kiroho, walijikwaa juu yake; walijikwaa na kuanguka chini.

Neno *‘kujikwaa’* hapa, pia linamaana ya *‘kukataa’*, na *‘kutotii’*. Viongozi wa Wayahudi walimkataa Yesu; waliikosa njia ya Mungu. Na kwa hiyo, Yesu ni jiwe linalowasababisha wakatae, wasitii, na kuasi dhidi ya Mungu. Na kwa sababu hiyo – hawatafurahia uwepo wa Mungu mbinguni. Na hii

inamhusu kila mtu, ambaye anajikwaa kwa Mungu, au anayemkataa Mungu. Biblia inatuambia kwamba, kama mtu hajamfanya Yesu kuwa jiwe la pembeni la thamani, katika maisha yake, atajikwaa jehanamu wakati wa mwisho wa maisha yake. Na hili ni jambo lisilohitaji mzaha. Na ndiyo maana utume wa kanisa ni muhimu sana. Kanisa halipo kwa ajili ya waumini wake tu. Lipo kwa ajili ya utume. Lipo kwa ajili ya kuwaambia wengine kuhusu Yesu, na kuwaonya wasimkatae. Kwa hiyo – katika kipindi hiki, tumemwangalia Yesu kama **Jiwe lililo hai**. Tumeona kwamba Yesu ni jiwe la pembeni lenye thamani. Pia tumeona kwamba Yeye ni jiwe lililokataliwa na watu wengi, na kwamba Yeye ni jiwe la kuwafanya watu wajikwae. Katika kipindi chetu kinachofuata, ninataka tuangalie Petro anamaanisha nini, anaposema kwamba sisi pia ni mawe yaliyohai. Kama Wakristo sisi ni sehemu ya nyumba ya Mungu. Sisi ni watu wateule, na watu wa ukuhani wa kifalme. Na kwa hiyo, hiki ni kitu cha kutufanya tufurahi!

KIPINDI 7: 1 Petro 2:4-12 “Mawe Yalilo Hai – Watu Watakatifu” (2)
Steve Lancaster

Hebu tufungue **1 Petro 2**, na katika kipindi hiki, nataka tulenge juu ya **mst 5 & 9**. Kabla ya mapumziko, tuliangalia juu ya somo la Yesu, kama **jiwe la thamani la pembeni**, na jiwe la kusababisha watu kujikwaa. Lakini je, kifungu hiki kinasema nini kuhusu sisi? Petro alipoandika barua hii, alitaka kuwatia moyo na nguvu Wakristo, ambao walikuwa wametawanyika katika **Asia Ndogo**. Baadhi ya Wakristo hao walikuwa wakiteseka kutokana na imani yao. Baadhi yao walikuwa mbali kutoka nyumbani. Yawezekana baadhi yao, walikuwa wapweke na wenye hofu, na labda baadhi yao, hawakuwa na uhakika wa imani yao. Petro anataka kuwatia moyo. Anataka wajue kwamba wao ni nani katika Kristo. Anataka wajue sehemu yao ni ipi katika Yesu Kristo. Kwa hiyo, katika Yesu Kristo, nafasi yao ni ipi, na wao ni nani? Petro anasema nini? Tunaweza kupata majibu katika **mst 5 ****. Na pia **mst 9&10 ****. Kama wewe ni Mkristo, hivi ndivyo ulivyo, na hii ndiyo nafasi yako katika Kristo. Wewe ni jiwe lililo hai, katika hekala la Mungu. Umejengwa katika nyumba ya roho. Wewe ni mtu wa ukuhani mtakatifu. Umechaguliwa. Wewe ni taifa takatifu. Wewe ni mmoja wa watu wa Mungu, na umeoneshwa rehema na neema. Mkristo ni mtu aliyebarikwa sana!

Yesu ni jiwe lililo hai – lakini wafuasi wake pia wanaitwa ‘*mawe yaliyo hai*’. Wewe na mimi ni ‘*mawe yaliyo hai*’. Umewahi kuitwa ‘jiwe’?! Kama jina lako ni **Petro**, unaweza kujibu ‘*ndiyo*’, kwa sababu tunajua kwamba jina Petro, linamaanisha ya ‘*jiwe*’ katika lugha ya **Kigriki**. Lakini hata leo, baadhi ya watu wanaitwa ‘*Livingstone*’ – ikiwa na maana ya ‘*jiwe lililo hai*’. Kulikuwa na mmisionari maarufu aliyeyitwa **David Livingstone**, ambaye alikuja Afrika katika karne ya kumi na tisa. Alikuwa mpelelezi, daktari, mmisionari, na mtu aliyetaka kukomesha biashara ya utumwa. Alikaa zaidi ya miaka **30** katika Afrika, katika nchi kama Afrika ya Kusini, Malawi, Botswana, Zambia, na pia Tanzania. Alimpenda Mungu, na alitaka kuieneza injili ya Yesu katika Afrika yote. Jina la familia yake lilikuwa Livingstone. Lakini, inapofika kwenye ufalme wa Mungu, kila mmoja ambaye ni mfuasi wa Yesu, pia ni ‘*Livingstone*’ (jiwe lililo hai) – hivi ndivyo unavyosema **mst 5**.

Tunapokuja kwake; tunapomkabidhi maisha yetu; tunapomfuata yeye kila siku, tunatengenezwa kuwa mawe yaliyo hai, ambayo yanatumika katika jengo la kiroho. Siyo jengo la kimwili, kama lile hekalu la **Yerusalemu** – bali nyumba ya kiroho. Siyo ya kutengenezwa kwa matofali, na vitu halisi. Haina madirisha wala milango; haina paa. Kwa kweli, nyumba hii ya kiroho, ni kubwa sana, na imeenea ulimwengu mzima. Ni kanisa, familia ya Mungu. Unaona, Mungu yuko katika mchakato wa kujenga kanisa lake. Yeye ni mjenzi mkuu. Na nyumba yake ya kiroho, imejengwa kwa

mamilioni na mamilioni ya mawe yaliyo hai; watu walioweka imani yao katika Yesu. Je, kwa nini inaitwa nyumba ya kiroho? Ni kwa sababu Roho Mtakatifu anaishi ndani yake. Sikiliza maneno ya **1 Wakorintho 3:16**: Paulo anawaandikia waumini huko **Korintho**: “*Hamjui kwamba ninyi ni hekalu la Mungu, na kwamba Roho wa Mungu anaishi ndani yenu*”. Hiki ndicho anachokisema Petro: “*Ninyi ni mawe yaliyo hai, kwa sababu Roho Mtakatifu anaishi ndani yenu, na mmejengwa katika hekalu la Mungu, nyumba ya kiroho*”.

Lakini tafadhali tambua kwamba unapojenga ukuta, hautumii tofali moja tu! Hautakuwa ukuta mzuri sana, kama una tofali moja tu ndani yake! Tunajua kwamba kuna tofali nyingi, katika ukuta wa nyumba – na matofali yanapaswa kukaa pamoja vizuri, ili yatengeneze nyumba. Kumbuka hivi; sisi siyo matofali ambayo yako menyewe tu, katika ukuta. Tumejengwa kama sehemu ya jamii hai; mwili wa waumini, wanaosaidiana wenyewe kwa wenyewe. Na kama Wakristo, tunapaswa kuwa pamoja, siyo peke yetu. Kama mawe yaliyohai katika nyumba ya roho ya Mungu, tunahitaji kuyasaidia mawe mengine yaliyo karibu nasi – lakini tunaweza kufanya hivyo kikamilifu, kama tutaendelea kuunganishwa na jiwe kuu la pembeni, Bwana Yesu.

Tambua katika **mst 5**, kwamba tunakuwa watu wa ‘**ukuhani mtakatifu**’. Na utaona katika **mst 9**, kwamba Petro anatomia neno lile lile tena; safari hii, anasema ni ‘**ukuhani wa kifalme**’. Je, Petro anamaana gani hapa, anaposema kuhusu ‘**ukuhani**’? Na kwetu ili tuelewe anachosema Petro, tunahitaji kurudi katika Agano la Kale. Kama unalijua Agano la Kale vizuri sana, utajua kwamba Kuhani wa kwanza katika Biblia, baada ya sheria kutolewa, alikuwa **Haruni**, ndugu yake **Musa**. Katika **Kutoka 29**, Musa aliambiwa na Mungu kumpaka mafuta Haruni, awe kuhani mkuu wa Waisraeli. Je, Haruni alifanya nini? Kazi yake ilikuwa nini? Alichaguliwa na Mungu kwa ajili ya kuomba, na kutoa sadaka kwa niaba ya watu wa Israeli. Watu hawakuruhusiwa kumsogelea Mungu; hawakuwa watakatifu, lakini kuhani aliangaliwa kama mtakatifu.

Katika siku hizo, ili dhambi zako ziweze kusamahewa, ulipaswa kutoa sadaka za kuteketezwa juu ya madhabahu. Ingeweza kuwa ng’ombe, kondoo, mbuzi, au hata njiwa. Na kwa hiyo, ulipaswa kuja kwenye hema pamoja na sadaka yako. Kuhani alimchinja, na kumtoa kwa Mungu, kwa niaba yako. Hukuru-husiwa kufanya hivi wewe mwenyewe. Ulipaswa kwenda kwa Mungu, kupitia kuhani. Na jambo hili liliendelea, hata hekalu lilipojengwa katika Yerusalemu, kwa zaidi ya miaka **1000**. Palikuwa na siku maalumu, kila mwaka, iliyoitwa **Siku ya Upatanisho**, ambapo sadaka moja kubwa, ilitolewa kwa ajili ya dhambi za watu wote. Lakini alikuwa kuhani mkuu tu, ambaye aliruhusiwa kuingia ‘**patakatifu pa patakatifu**’, katika hekalu, na kutoa sadaka hii. Na hii ilikuwa mara moja tu kwa mwaka! Unaweza kusema kwamba, kumfikia Mungu kulikuwa na mipaka!

Lakini, yote haya yalibadilika Yesu alipokufa msalabani! **Haruni** alikuwa kuhani mkuu wa kwanza, na Yesu ni kuhani mkuu wa mwisho. Ngoja niwasomee maneno machache kutoka Kitabu cha **Waebrania 5:1**. Mwandishi anaandika kuhusu kazi ya kuhani mkuu, katika siku za Agano la Kale: “*Maana kila kuhani mkuu aliyetwaliwa katika wanadamu, amewekwa kwa ajili ya wanadamu, katika mambo yamhusuyo Mungu, ili atoe matoleo, na dhabihu kwa ajili ya dhambi*”. Lakini kwa Yesu, ilikuwa tofauti. Yeye alichaguliwa, siyo na wanadamu, bali na Mungu, ili awe kuhani mkuu wa mwisho. Alichaguliwa ili awawakilishe wanaume na wanawake, katika mambo yanayohusu uhusiano wao na Mungu. Na alitoa sadaka kwa ajili ya dhambi. Hakutoa sadaka za wanyama wa kuteketezwa, juu ya madhabahu ya hekaluni huko Yerusalemu – lakini alijitoa mwenyewe, kama sadaka kwa ajili ya dhambi. Aliruhusu mwenyewe ku-uawa. Je, unaweza kuamini hili?! Kuhani mkuu, aliyejitoa mwenyewe, juu ya madhabahu, ili kwamba dhambi za ulimwengu, ziweze kusamehewa. Hii ni sadaka ya ajabu! Na kwa sababu hiyo, hakuna haja ya kutoa sadaka zaidi, kwa ajili ya dhambi. Yesu ndiye sadaka ya mwisho, kuhusu mambo ya dhambi.

Waebrania 4:14 unasema hivi: “*Basi, iwapo tunaye kuhani mkuu, aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, tuyashike sana maungamo yetu*”. Lakini, hebu sikiliza **mst 16**: “*Basi, natu-kikaribie kiti cha neema kwa ujasili*”. Kwa sababu ya Yesu, sote tunaweza kwenda kwa Mungu wakati wote. Kwa sababu ya Yesu, tumeruhusiwa kumkaribia Mungu, katika maombi, na kuomba msamaha. Hatuhitaji kupeleka sadaka ya mnyama kwa kuhani. Hatuhitaji kusubiri kwa ajili ya siku moja kwa mwaka, ili ya kuhani mkuu aweze kuingia patakatifu pa patakatifu. Hiyo imekwisha! Nafasi ya Hema, na Hekalu, imechukuliwa na **kanisa**. Mungu alikuwa akiishi katika hekalu; humo ndimo uwepo wake ulipatikana – lakini sasa, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, Mungu anaishi ndani ya wale walio wake. Nafasi ya madhabahu imechukuliwa na Yesu, na damu yake. Makuhani ambao walihudumu katika hekalu, nafasi yao sasa imechukuliwa, na walioamini katika Yesu. Na kwa hiyo, sasa tunaupendeleo wa kwenda kwa Mungu, na kutoa sadaka zetu wenyewe - siyo wanyama walio kufa na kuwekwa juu ya moto, bali tunampa yeye maisha yetu, kama sadaka ya ibada.

Petro anasema katika **mst 5**, katika kifungu chetu: “*Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu*”. **Mst 9** unasema hivi: “*Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu*”. Waumini wote ni sehemu ya ukuhani. Sote tunatumika kama makuhani wa Mungu, katika ulimwengu. Siyo wachungaji na wainjilisti tu – bali wazee wa kanisa, mashemasi, na kila mtu katika kanisa, ambaye ni mwamini wa kweli, ni kuhani katika ufalme wa Mungu! Sote tunaweza kushiriki katika ibada ya Mungu. Sote tunaweza kukikaribia kiti cha enzi mbinguni. Sote tunaweza kuwaombea watu, na sote tunaweza kutoa maisha yetu, kuwa sadaka kwa Mungu. Sisi ni makuhani wa agano jipya.

Lakini vipi kuhusu neno ‘*wateule*’? **Mst 9** unasema hivi: “*Ninyi ni watu wateule*”. Jana, tulipoangalia katika utangulizi wa barua, utakumbuka kwamba, hivi ndivyo Petro anavyowaita wasomaji wake. **1 Petro 1:1**. “*Kwa wateule*”. Ninafikiri neno hili ni muhimu sana kwa Petro, na ninafikiri kwamba ni neno muhimu kwa Mkristo. Hebu elewa jambo hili – kama wewe ni mkristo wa kweli, umechaguliwa na Mungu. Neno hili ‘*mteule*’ tayari, limetumika mara mbili kabla ya kifungu hiki. **1 Petro 2:4**, unatuambia kwamba, jiwe lililo hai “*limechaguliwa na Mungu*”. **1 Petro 2:6** unatuambia kwamba, Yesu ni “*jiwe teule la thamani la pembeni*”. Kwa kweli, katika **1:20** Petro anasema kwamba, Yesu “*alichaguliwa kabla ya ulimwengu kuumbwa*”. Lakini sasa, katika **mst 9**, sisi pia tunaelezewa kuwa ni “*watu wateule*”. Je, hii inakufanya kujisikia vipi? Mungu mwenyewe alikuchagua wewe uwe katika familia yake. Kuna jambo maalumu kuhusu kuchaguliwa, si ndiyo - hasa kama umechaguliwa na Mungu. Watu Waisraeli walikuwa wameteuliwa na Mungu.

Watu wa Kiyahudi katika Agano la Kale, walikuwa wateule wa Mungu. Na hii ndiyo maana Petro, katika **mst 9**, anatumia maneno hayo: “*watu wateule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu*”. Haya yalikuwa ni maneno yaliyotumiwa kuelezea Israeli. Kwa kweli, anatumia maneno ya mstari maarufu, katika **Kutoka 9:5-6**. Musa alikuwa amepanda juu ya mlima **Sinai**, kuongea na Mungu - na Mungu alimpa ujumbe maalumu kwa ajili ya kuwapa Waisraeli. Hivi ndivyo alivyosema Mungu: “*Hapo ndipo mtakapokuwa tunu kwangu kuliko makabila yote ya watu. Maana dunia yote pia ni mali yangu, nanyi mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani, na taifa takatifu*”. Kwa maneno mengine, Mungu anawaambia Israeli, nimewateua ili muwe watu maalumu. Na ninahakika kwamba, jambo hili liliwafanya Waisraeli, kujisikia wao ni watu maalumu sana. Mungu Mwenyezi alikuwa amewachagua! Lakini tunajua hadithi hii, siyo?

Israeli walilivunja agano walilokuwa nalo na Mungu. Walimwasi Mungu. Na kisha Yesu alipokuja, walimkataa; jiwe lililo hai. Na kwa sababu hiyo, badala ya Wayahudi, Mungu akachagua watu wengine kuwa watu wake wateule. Na ndivyo ilivyo leo, watu wateule wa Mungu, ni kanisa la

Kikristo; watu waliotoa maisha yao kwa Mungu, kwa njia ya kuamini katika Yesu Kristo. Hao ni wewe na mimi! Na Petro anaposema katika **mst 10**: “*Ninyi mliokuwa kwanza si watu, bali sasa ni watu wa Mungu*”. Kumbuka kwamba, Petro anawaandikia Wakristo walio-tawanyika katika **Asia Ndogo**. Baadhi yao walikuwa wanateseka kwa ajili ya imani yao; wengine walikuwa wamejisikia wapweke na wenye hofu. Lakini Petro anawaambia – kumbukeni ninyi ni nani. Ni watu wateule. Ni watu wa milki ya Mungu. Kama kundi la Wakristo, mmeteuliwa - lakini pia, kama mtu binafsi, umechaguliwa na Mungu. Kwa kweli, hili lilikuwa ni jambo ambalo Paulo pia, alilitaja katika barua zake. Katika Kitabu cha **Waefeso**, analitaja kama mojawapo ya baraka za rohani, tunayoipokea kama waumini. **Waefeso 1:4** unasema kwamba: “*Mungu alituchagua, kabla ya misingi ya ulimwengu*”. **Waefeso 1:11** unasema: “*katika yeye, pia tulichaguliwa*”. Mungu Baba, kupitia Yesu Kristo, amekuchagua wewe na mimi. Na Paulo anatuambia kwamba, hata kabla ya uumbaji, Mungu alichagua nani watakuwa watoto wake.

Kuna kifungu katika **Yohana 15**, ambacho kinazungumza kuhusu Yesu akichagua wanafunzi wake. Saa chache tu kabla ya kukamatwa kwake, Yesu anazungumza na wanafunzi wake, na anawaambia katika **mst 16**: “*ninyi hamkunichagua mimi, bali mimi niliwachagua ninyi*”. Tunajua kwamba Yesu mara kwa mara, alifanya mafundisho yake katika uwanja wa hekalu, na watu waliokuwa wakipita pale, walisimama kusikiliza ambacho alikuwa akisema. Ndani ya uwanja mkubwa wa hekalu, kulikuwa na walimu wengine (*marabi*), waliokuwa wakifundisha makundi ya watu kuhusu Agano la Kale. Baadhi ya walimu hawa walikuwa wazuri; labda wengine walikuwa wanachosha! Baadhi yao walikuwa wataalamu katika somo fulani; baadhi ya walimu, walikuwa wanafurahisha, na kuleta mkanganyiko. Na kwa hiyo waliweza kuvutia watu wengi kwenye madarasa yao. Watu wanataka kusikiliza walimu wazuri.

Na kwa hiyo, kilichotokea ni kwamba, watu walikuwa wanatembea karibu na uwanja wa hekalu, na kusikiliza mafundisho ya walimu mbali mbali. Na baada ya kuwasikiliza wote, wangeweza kuamua wamfuata mwalimu yupi. Kisha wangukuwa wafuasi wa mwalimu huyo. Wazo hapa ni kwamba, wangeweza kumchagua mwalimu waliyetaka kumfuata – lakini Yesu, katika **Yohana 15**, akijua jinsi ilivyokuwa, anawaambia wanafunzi wake, “*ninyi hamkunichagua mimi, bali mimi niliwachagua ninyi*”. ‘*Niliwaalika kuja kuwa wanafunzi wangu – niliwachagua*’.

Ngoja turudi kwa Paulo katika **Waefeso**. Anaongea na waumini, na anawaambia “*Mungu aliwachagua ninyi kabla ya ulimwengu kuumbwa*”. Hivi ndivyo ilivyo kwetu leo. Mungu alikuchagua, na Mungu alinichagua mimi. Sasa, unaweza kusema: ‘*kwa kweli, mimi nilimchagua Mungu. Nilichagua kumfuata Yesu – ulikuwa uamuzi wangu*’. Ndiyo, uliamua; ulikuwa uamuzi wako, lakini ni kwa sababu tu, kabla ya ulimwengu haujaumbwa, Mungu alikuchagua wewe kama mtu atakaye itikia kwake. Kama asingekuchagua – usingekuwa Mkristo. Hii ni baraka ilioje! Huu ni upendeleo wa namna gani, kwamba Mungu, katika upendo wake, na neema yake, aliamua kukuchagua wewe na mimi! Siyo kwa sababu ya kitu chochote tulichofanya. Hatukustahili – lakini licha ya dhambi zetu, aliamua kutupenda na kutuchagua.

Kwa hiyo – Yesu alichaguliwa na Mungu Baba. Lakini sisi, kama mawe yaliyo hai, pia tumechaguliwa na Mungu, kuwa washirika katika familia yake. Sisi ni watu wateule. Kabla ya kumaliza kifungu hiki, ninataka tuangalie kitu kimoja, ambacho pia ninafikiri ni muhimu sana. Angalia tena katika **mst 5** – mwishoni mwa **mst 5**. Tumejengwa ndani ya nyumba ya kiroho, ili tuwe ukuhani mtakatifu – lakini je, tunapaswa kufanya nini? Tunapaswa “*kutoa sadaka za kiroho, zilizokubaliwa na Mungu, kupitia Yesu Kristo*”. Na pia mwishoni mwa **mst 9**: Sisi ni watu wateule ili kwamba tuweze “*kuzitangaza fadhili zake aliye tuita*”.

Kwa maneno mengine, kama watu wateule katika nyumba ya Mungu, tunawajibu wa kufanya mambo mawili: kutoa sadaka za kiroho - na kutangaza fadhili za Mungu. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Na mambo haya mawili yanaweza kuwekwa katika neno moja – kuabudu. Tumeagizwa kumwabudu Mungu wetu. Kwa hiyo – ngoja tuangalie sadaka ya kiroho ni nini, na kujuliza swali, ni kwa namna gani tunatoa sadaka za kiroho? Kwanza, ngoja nisome anachosema Paulo, katika **Warumi 12:1**: “*Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, yakumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana*”. Mwanzoni, tuliangalia kazi za makuhani katika Agano la Kale, na tuliona kwamba, sadaka zilitolewa juu ya madhabahu. Kwa kawaida sadaka zilikuwa zimekufa. Makuhani waliua mnyama na kumteketezwa juu ya madhabahu. Lakini tambua kwamba, **Paulo** anaongeza neno ‘*iliyo hai*’ katika mstari huu.

Hapa katika **Warumi 12**, sadaka iko hai; ina uhai; ina pumua. Miili yetu iko hai – lakini kwa sababu sisi tunamilikiwa na Mungu, na kwa sababu miili yetu, ni hekalu la Roho Mtakatifu - siyo yetu; ni ya Yesu Kristo. Na kila siku, tunapaswa kupambana na ubinafsi wetu, tunapaswa kuyatoa maisha yetu kwa Kristo. Kila kitu unachofanya kuhusu mwili wako, kinapaswa kufanywa kuwa tendo la ibada kwa Mungu. Kama unapika chakula - fanya hivyo kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kama unajenga nyumba, au kama unaendesha gari, au kama unasafisha nyumba - mambo haya yanaweza kugeuzwa kuwa tendo la kumwabudu Mungu. Kama ningekuwa mjenzi, ningeweza kujiambia mwenyewe: ‘*ninapojenga nyumba hii, ninaenda kufanya kazi kwa bidii, kwa sababu ninataka jina la Mungu liabudiwe kupitia kazi yangu. Na ninataka ubora wa kazi yangu, umwakisi Yesu. Kwa hiyo, kadri ninavyojenga, nitamwabudu Mungu, kwa ujuzi wangu kama mjenzi*’. Kumbuka, kumwabudu Mungu siyo kitu fulani, ambacho unakifanya kanisani tu! Namna unavyoutumia mwili wako, na namna unavyofanya shughuli zako za kila siku, zinapaswa kufanywa kama tendo la ibada. Hata namna unavyoandaa mahubiri yako, inaweza kuwa tendo la ibada kwa Mungu! Kama hutumii muda wakutosha kujiandaa kuhubiri, huwezi kumheshimu Mungu. Itoeni miili yenu kama sadaka zilizo hai, yatoeni maisha yenu yote kwa Mungu, kama tendo la ibada, ili kwamba matendo yenu yote yamtukuze Mungu.

Jambo la pili, tunapotoa zawadi, na tunaposhirikiana na watu wengine, hasa wale walio katika uhitaji, tunatoa sadaka za kiroho. Katika barua yake kwa **Wafilipi**, Paulo anawaandikia ili kusema ‘*asante*’. Walikuwa wamemtumia zawadi. Hatujui zawadi hizo zilikuwa vitu gani, lakini kanisa la **Filipi** lilienda kumsaidia Paulo. Kwa hiyo, walimtuma mmoja wa washirika wao kwenda Roma, pamoja na zawadi kwa ajili ya Paulo. Na Paulo lazima alifurahishwa sana nao. Anawaambia (4:18): “*Vitu vile vilivyotoka kwenu, harufu ya manukato, sadaka yenye kibali, impendezayo Mungu*”. Kanisa walionesha upendo kwa Paulo, na waliamua kuchukua hatua. Walimtumia zawadi – na matendo yao yalikuwa yanampendeza Paulo, na yalikuwa yanampendeza Mungu. Lilikuwa tendo la ibada. Katika **Waebrania 13:16**, mwandishi anasema hivi: “*Msisahau kutenda mema, na kushirikiana; maana sadaka kama hizi ndizo zinazompendeza Mungu*”. Kadri tunavyoshirikiana na watu walio katika uhitaji; kadri tunavyofanya mema kwa wengine; hata tunaposhirikishana injili na mtu asiye mjua Kristo – tunamwabudu Mungu, na tunatoa sadaka za kiroho kwake.

Na kisha jambo la tatu, jambo la kutoa shukrani, na sifa, kwa Mungu, kama sadaka ya kiroho. Katika ulimwengu, Wakristo wanapokutana Jumapili asubuhi, hukutana pamoja ili waimbe, kuabudu na kumshukuru Mungu kwa upendo wake. Kwa kweli, kumwabudu Mungu linapaswa kuwa jambo la msingi katika kanisa. **Waebrania 13:15** unasema hivi: “*na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima – tunapaswa kushukuru jina lake*”. Na tunaweza kuimba sifa za Mungu, tunapokuwa katika nyumba zetu, au tunapokutana pamoja na kundi kubwa la watu. Na tunapofanya hivi – tunatoa sadaka ya kiroho ya sifa. Ninapenda anachosema Paulo katika barua yake kwa Wakristo,

huko **Kolosai**. Katika **Wakolosai 3:16**, anawatia moyo “*waimbe zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni, huku tukimwambia Mungu kwa neema mioyoni mwetu*”. Kuimba sifa za Mungu, na kumshukuru yeye, kwa ajili ya kile alichofanya, ni sadaka ambayo tunapaswa kutoa.

Ngoja niwaulize maswali kadha, kuhusu jambo hili la **kuabudu** – na baadhi ya maswali yanaweza kukufanya usijisikie vizuri. Je, vipi kuhusu ibada katika kanisa lako? Katika kanisa lako, uimbaji ukoje? Je, ni ibada ya kiroho? Je, sadaka za kiroho zinatolewa? Au ni sadaka za kidunia tu? Je, huwa tunaimba katika nguvu za Roho Mtatatu? Je, vipi kuhusu viongozi wa kwaya? Je, vipi kuhusu watu wanaopiga vinanda, na kucheza mbele? Na je, ibada yetu ni ya kiroho? Je, inampendeza Mungu?

Je, ibada yetu inatoka moyoni kiasi kwamba tunataka kumsifu Mungu, au inatoka moyonikana kwamba tunataka kufanya maonyesho tu? Tunapoimba – je, tunamsifu na kumshukuru Mungu kweli, au tunajiburudisha tu? Kama ibada yetu na uimbaji wetu siyo wa kiroho – kama ni maonyesho tu, basi haikubaliki kwa Mungu. Ninaguswa na jambo hili kwamba, katika baadhi ya makanisa ya **AIC**, wanakwaya hawawaongozi waumini kumsifu Mungu - lakini wanataka kufanya maonesho tu mbele ya waumini. Inaonekana kwamba waumini huangalia na kusikiliza kwaya sana, kuliko kushiriki katika kumwambia Mungu! Ni wajibu wa kwaya kuongoza watu katika kumsifu Mungu. Hebu tuhakikishe kwamba tunapokutana Jumapili asubuhi, au wakati wowote tunapokutana, kwamba sote tunatoa sadaka za kiroho za sifa, na shukrani kwa Mungu.

Nataka kuhitimisha kwa maneno kutoka kitabu cha **Waefeso**, kwa sababu anachosema Paulo hapa, ni kile kile ambacho Petro amekuwa akisema. Hivi ndivyo mtume Paulo anavyosema katika **Waefeso 2:19-20**: (Biblia Habari Njema) **

KIPINDI 8: 1 Petro 4:12-19: “Kuteseka kwa sababu ya kuwa Mkristo”
Steve Lancaster

Tufungue **1 Petro 4**, na tutasoma **mst 12-19**. Na kichwa cha somo la kipindi hiki, ni ‘*kuteseka kwa sababu ya kuwa Mkristo*’. Hili linakufanya ujisikiaje? Je, linakujaza furaha?! Labda siyo – kwa sababu siyo somo la furaha kuzungumzia! Na somo hili linatukumbusha kwamba, maisha ya Kikristo, siyo kitu rahisi. Yanaweza kuwa magumu. Wakati mwingine kuna mateso na kuteswa katika maisha yetu, kwa ajili ya Yesu. Na katika nyakati kama hizi, maisha katika Kristo huwa hayafurahishi. Hakuna mtu anayependa kuteseka. Hakuna mtu anayependa kuteswa. Lakini tunajua, tunaposoma Biblia zetu, kwamba mateso ni sehemu ya maisha ya Kikristo. Na jambo hili limechukua sehemu kubwa, katika barua hii.

Kumbuka katika utangulizi wetu, tulijifunza kwamba mojawapo ya malengo ya barua hii, ni somo la mateso. Kwa kweli neno ‘*mateso*’ limetumika mara **17** - mara **5** kutaja mateso kwa ajili ya Kristo, na mara **12** kutaja maisha ya Mkristo. Suala la mateso lipo katika kila sura ya barua hii. Petro anataka kuwatia moyo wasomaji wake kuvumilia mateso, na pia anajua kwamba, kutakuwa na mateso zaidi na zaidi, katika kanisa la mwanzo. Unaposoma barua hii, utaona kwamba kuna vifungu vitatu tofauti, Petro anapozungumza kuhusu mateso. Sura **2:19-24**. Sura **3:13-17**. Na sura **4:12-19** – na kifungu hiki cha mwisho, ndicho ninachotaka tukiangalie pamoja kwa sasa. Lakini pia tutakuwa tunaangalia baadhi ya mistari mingine katika barua hii. Tutakuwa tunazunguka katika **1 Petro**, na sehemu zingine za Agano Jipya. Kwa hiyo, tafadhali kaa na Biblia yako, ikiwa imefunguliwa, na uwe tayari kufungua vifungu mbali mbali.

Karibu miaka **500** iliyopita, mtu mmoja kutoka Uingereza, aliyeitwa **John Foxe**, alichapisha kitabu, kuhusu mateso na kuteswa katika kanisa. Kitabu hicho kiliitwa “**Kitabu cha mashahidi**”. Kitabu hiki kilikuwa marufu sana na ilikubalika kwamba, kiwekwe katika kila kanisa huko Uingereza. Ngoja niwasomee anachosema kuhusu mateso katika Biblia. “*Ni jambo la kutisha unapofikiri kuhusu mateso ya watu watakatifu, ambao walikuwa wengi. Baadhi ya Wakristo walichinjwa kwa upanga; wengine walichomwa moto. Wengine walipigwa mijeredi; wengine walichomwa visu; wengine waligongomewa kwenye msalaba; wengine walizamishwa baharini; wengine waligandishwa kwa barafu; wengine walikufa kwa njaa; wengine hata walikatwa ndimi zao; wengine waliuawa kwa kupigwa mawe; wengine walikatwa mikono yao, na wengine waliachanishwa kati kati kwa msumeno*”.

Pia inajulikana kwamba, wanafunzi wote wa Yesu, waliuawa kwa sababu ya imani yao katika Yesu, isipokuwa mmoja. Mtume Yohana. Yeye alikufa mwaka **98**, baada ya Yesu kuzaliwa, na yeye alikufa kifo cha kawaida huko **Efeso**. Lakini hata yeye, aliteswa kwa sababu ya imani yake katika Yesu. Alifungwa na Waroma katika kisiwa cha **Patimo** - na tunajua kwamba huko ndiko alikoandika kitabu cha **Ufunuo**. Pia tunajua kwamba mtume **Paulo** alifahamu jinsi ilivyo kuteswa kwa ajili ya Kristo. Unaposoma barua zake, utaona ni kwa kiasi gani aliteseka. Katika baadhi ya maeneo katika safari zake, wakati alipokuwa akihubiri injili, watu walijaribu kumuua. Alipigwa, na kuwekwa gerezeni; alipigwa mawe, na kutukanwa. Unaposoma **2 Wakorintho 11:23-28** unaweza kuona orodha ya mateso yake. Inashangaza kuona kiasi ambacho aliteswa kwa ajili ya Kristo, na wanahistoria wanatuambia kwamba, aliuawa huko **Roma**, ambako alikatwa kichwa. Kuteswa, katika kipindi cha kanisa la mwanzo, ilikuwa kitu cha kawaida – lakini kuteswa huko kuliendelea kwa kipindi cha miaka **2000** iliyopita, na hata leo Wakristo wanauawa kwa ajili ya imani yao katika Yesu, katika maeneo kama vile Somalia, Yemen, Irani, Iraki, Sudan, Pakistan na India, na hata Kenya!

Na kuteswa kunaendelea kuongezeka, hasa katika nchi za Kiislamu. Je, Petro anasema nini katika sura **4:12**? “*Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unawapata kama moto ili kuwajaribu, kama kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho*”. Kwa kweli, Petro anasema katika sura **5:9**: “*mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani*”. Je, kuna ujumbe gani hapa? Kama wewe ni Mkristo, unapaswa kutarajia mateso katika maisha yako. Petro anasema, ‘*msishangae mateso yanapokuja*’. Ni kitu cha kawaida. Wakristo wanaposimama kwa ajili ya injili, watateswa. Je, tunapaswa kutarajia mateso? Unajua, kuna baadhi ya wachungaji ambao husema kwamba, Wakristo hawapaswi kuteseka! Na wanasema kwamba, kama unateseka, kuna dhambi katika maisha yako! Pia wanasema kwamba Mkristo anapaswa kutarajia kuwa tajiri! Hii inaitwa ‘*injili ya mafanikio*’.

Ni upuuzi! Ni mafundisho ya uongo! Je, wanapata wapi mawazo haya? Je, wamesoma Biblia zao? Sikiliza mistari hii: Huyu ni Paulo akizungumza katika **2 Timotheo 3:12**: “*Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Yesu Kristo, wataudhiwa*”; watateswa. Na je, vipi kuhusu mistari huu katika **Yohana 15:14 & 20**. Haya ni maneno ya Yesu – na hapa ninatumia toleo la Habari Njema: “*Kama ulimwengu ukiwachukia ninyi, kumbukeni kwamba umenichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi. Ikiwa wamenitesa mimi, watawatesa na ninyi pia*”. Tumeonywa kwamba, Wakristo wanapaswa kutarajia mateso kwa sababu ya imani yao. Kwa kweli, Petro anatuambia kwa uwazi sana, kwamba Yesu ni mfano wetu. Hebu fungua **1 Petro 2:21**: “*Maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuata nyayo zake*”. Tunapaswa kufuata mfano wake ikibidi. Sasa, hii haina maana kwamba tunapaswa kwenda nje, na kutafuta mateso na kuteswa, lakini inamaana kwamba, kama tumeitwa kuteseka kwa ajili ya Kristo, basi tunapaswa

kuenenda kama Yesu. Angalia sura **4:1**: “*Basi kwa kuwa Kristo, aliteswa katika mwili wake, ninyi nanyi jivikeni silaha ya nia ile ile*”. Tunajua jinsi Yesu alivyoteseka. Tunasoma katika injili kwamba, kipindi cha huduma yake, alichekwa; alitukanwa; alidharauliwa, na alichukiwa, kwa sababu ya kile alichokisema, na kufanya. Na pia tunajua jinsi alivyoteseka alipokaribia msalabani.

Je, kuna yeyote amewahi kuona filamu inayoitwa, ‘*The Passion of Christ*’? Ni filamu iliyotengenezwa na Mel Gibson, ambayo inahusu mateso ya Yesu, yaliyompeleka hadi msalabani, na wakati alipokuwa anakufa msalabani. Ninafikiri kwamba filamu hiyo kwa kiasi kikubwa inausahahi wa kibiblia, lakini inazungumzia hadithi chache, ambazo hazimo katika Biblia. Ni filamu yenye vurugu sana, ambayo ni vigumu hata kuitazama – lakini nafikiri kwamba inatuonesha mateso ya ajabu, ambayo Yesu alipaswa kuyapitia. Na bado, Yesu hakuwa na hatia ya kosa lolote! Angalia sura **2:22**: “*Yeye hakutenda dhambi, wala hila haikuonekana kinywani mwake*”. Hii ni nukuu kutoka Agano la Kale; kutoka kitabu cha Isaya . Na kama unataka kusoma kuhusu mateso ya Yesu msalabani, soma **Isaya 53**. Kitu cha ajabu ni kwamba, Isaya aliandika maneno haya, miaka **700** kabla ya Kristo, na bado anaeleza jinsi kilivyo kifo cha kusulubiwa – hata kabla ya kusulubiwa hakujaumbwa. Ilichukuliwa kama namna mbaya sana ya kufa – kuachwa umetundikwa msalabani. Na kwa kawaida muhusika aliachwa uchi. Ilikuwa inadharirisha na kuumiza sana - ingawa misumari katika viganja vya mikono, na miguuni, haikuwa sababu ya kifo. Muhusika alikufa kwa sababu ya kunyimwa pumzi. Hakuweza kupumua kwa sababu asingeweza kusukuma hewa wakati yuko msalabani. Na bado, licha ya maumivu, na kudharirishwa huku - Yesu alitikiaje? Angalia sura **2:23** **.

Usishangae kama utateswa kwa ajili ya imani yako, na kama utateswa, itikia kwa watesi wako katika namna ile ile, aliyoitikia Yesu. Yeye hakurudisha; hakufanya vitisho, na aliwasamehe. Sasa, wewe hutateswa kama Kristo, au mmojawapo wa wanafunzi wake. Sisi hatutasulubiwa msalabani, na pengine hatutauawa kwa ajili ya imani yetu - lakini mateso siyo yote ni ya kimwili. Tunaweza kuteswa katika namna nyingine. Tunaweza kutukanwa; watu katika jamii, wanaweza kutusingizia mambo ambayo siyo kweli, na matokeo yake, ushuhuda wetu unaweza kuharibiwa. Katika baadhi ya mambo, hasa huko **Zanzibar**, baadhi ya wachungaji wamejikuta nyumba zao, na makanisa yao, yamechomwa moto. Hapa Tanzania bara, labda, katika miaka ijayo, watu wanaweza kuchoma kanisa lako, kwa sababu wanachukia unachokisimamia kama Mkristo. Tunaweza hata kupoteza mali zetu. Tunaweza kuvamiwa kwa maneno au kimwili – lakini tunahitaji kuitikia kama Yesu, alivyofanya. Na ili kufanya hivyo, tunahitaji msaada wa Mungu. Asili yetu ya uanadamu ni kupigana, na kutafuta kisasi kwa wale waliosababisha shida kwetu. Je, Petro anasema nini katika sura **4:19**? “*Wale wanaoteseka kufuatana na matakwa ya Mungu, wanapaswa kwa matendo yao mema, kujiweka chini ya Muumba wao ambaye ni wa kuaminika kabisa*”. Endelea kufanya wema; fuata moyo wa Yesu, na fuata nyayo zake.

Tambua katika kifungu chetu, Petro anasema kwamba, tunapaswa kuhakikisha kwamba, mateso yoyote tunayopitia, ni kwa kutokana na sababu njema - na siyo kwa sababu ya tabia mbaya. Angalia sura **4:15**: “*Asiwepo mtu yeyote miongoni mweni ambaye anapaswa kuteseka kwa sababu ni mwuaji, au mwizi, au mhalifu, au mwovu*”. Usifikiri kwamba, kama unateseka kwa sababu ya kufanya jambo baya, kwamba Mungu amethibitisha mateso hayo. Hakuna heshima maalumu katika kuvumulia mateso, kama ni kwa aili ya tabia mbaya. Na kesho tutaangalia suala la ‘*utili*’, ambapo Petro anataja utii katika maeneo yetu ya kazi. Tunapaswa kuwatii wakuu wetu kwa heshima. Petro anasema, wakati mwingine, boshi wako anaweza kukuadhibu, hata kama hujafanya jambo lolote baya. Na anasema, kama itatokeo hivyo, ni vyema kama utavumulia kwa nia ile ile kama ya Yesu. Lakini katika sura **2:20**, anasema: “*Kwa maana ni sifa gani kustahimili, mtendapo dhambi na kupigwa makoff*”. Kama umefanya jambo baya, unastahili adhabu. Hata yule mmoja wa

wezi, waliosulubishwa pamoja na Yesu, alijua hilo. **Luka** anatuambia kwamba alimwambia mwizi mwingine: “*Nayo ni haki kwetu sisi, kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu, bali huyu hakutenda lolote lisilofaa*” (Luka 23:41).

Kwa hiyo, Petro anasema, kama umeadhibiwa kwa sababu ya kufanya jambo baya, na unastahimili kwa uvumilivu, usifikiri kwamba hivyo ni kumheshimu Mungu. Kwa upande mwingine, kama unateseka kwa sababu ya kufanya jambo jema, na kustahilimi katika jina langu, hiyo ni tofauti; hiyo inakubalika. Lakini Petro pia ana baadhi ya maneno zaidi ya kutushauri. Je, mateso yanapokuja tunapaswa kuitikia kwa namna gani? Tufungue sura **3:14**: Petro anasema hivi: Mateso yanapokuja, “*msiogope kutisha kwao, wala msi-fadhaike*”. Msiogope vitisho vya watu wanaotaka kuwatesa ninyi. Unapokumbana na upinzani katika jina la Yesu, usiogope. Unajua, neno ‘*msiogope*’, linaonekana karibia kila kitabu katika Biblia. Mungu alimwambia **Yoshua**, alipokuwa akienda kwenye nchi ya ahadi, ‘*usiogope*’. Malaika **Gabrieli**, alipomtembelea **Mariam** ili kumwambia kwamba atamzaa Mesia, alisema ‘*usiogope*’. Malaika walipowatembelea wachungaji shambani huko **Bethlehem** waliwaambia, ‘*msiogope*’. Kirai hiki kimetumika mara nyingi katika Biblia. Usiogope, Usiogope, Usiogope! Na labda sababu ya kufanya hivyo ni kwamba, sisi kama wanadamu, ni kawaida kuogopa. Lakini wakati mwingine, linaweza kuwa tatizo kubwa katika maisha yetu, hofu inapotushinda na kututawala. Hiyo siyo afya, na Shetani anajua hivyo! Anataka tuogope. Anataka tuondoe macho yetu kwa Yesu. Anataka hofu itutawale.

Kuteswa kunapokuja, hasa kuteswa kunapokuwa kimwili, tunaweza kuogopa. Lakini Petro anasema: “*msifadhaike, na msiogope kutisha kwao*”. Je, hii ina maana gani? “*Msiogope kutisha kwao*”. Ninafikiri kwamba Petro anazungumza kwamba, kwa ujumla watu huogopa mambo wanayoweza kutendewa na watu, na pia wanaogopa kufa.

Lakini sisi kama Wakristo, hatupaswi kuogopa kutisha kwao – kwa sababu tunajua kwamba, hata kama kuteswa kwetu kutatupelekea kufa, huo siyo mwisho wa Mkristo; ni mwanzo tu. Na Yesu anasema hivi katika **Mathayo 10:28**: “*Msiwaogope wauuao mwili, wasiweze kuiua na roho; afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanamu*”. Kumbuka, kwamba kwa Wakristo hawa katika **Asia Ndogo**, kuteswa kuna ongezeko, na kanisa linapata vitisho. Kuteswa na Wayahudi, na kuteswa na Waroma. Wakristo walikuwa chini ya shinikizo.

Katika **Ufunuo 2**, Yesu analiandikia kanisa la **Smirna**. Kumbuka, Yohana anaandika kutoka kisiwa cha **Patimo**, na anawaandikia Wakristo wale wale, ambao Petro anawaandikia. Yohana aliandika Kitabu cha **Ufunuo** yapata miaka **25**, baada ya Petro kuandika barua yake ya kwanza. Hivi ndivyo anavyosema Yohana katika **Ufunuo 2:10** **. Yohana anasema, ‘*usiogope*’. Uwe mwaminifu, hata kufa. Ngoja niwaambie hadithi moja, kuhusu mtu mmoja kutoka **Smirna**, ambaye alitii amri hii kutoka kwa Yohana. Hakuogopa kuteswa. Miaka **60** baada ya Yohana kuandika maneno haya kwa kanisa la Smirna, mmoja wa wazee wa kanisa huko, aliuawa kwa sababu ya imani yake. Jina lake aliitwa **Polycarp**. Alikuwa mwanafunzi wa mtume Yohana, na alikuwa askofu wa Smirna. Sasa, kama uliishi katika Smirna, kila mtu alitakiwa kumwabudu **Kaisari**, mfalme wa **Roma**, na kama usingemwabudu - ungekuwa katika shida. Kwa hiyo, jiulize shinikizo hili lilikuwa la namna gani, kama wewe ungekuwa Mkristo katika Smirna. Kila mwaka, mojawapo ya majaribu, ambayo Waroma walitumia kuwapima wananchi wao, lilikuwa swali hili: “*Bwana ni nani?*” Jibu ulilotarajiwa kutoa ni hili: “*Kaisari ni Bwana, hakuna mwingine lakini Kaisari tu*”.

Lakini **Polycarp** alikataa kusema maneno haya. Askari wa Roma waliagizwa kwenda kumtafuta. Walifika mlango ni kwake, na rafiki zake, waliokuwa pamoja naye ndani ya nyumba, walimsihi atoroke. Lakini Polycarp, ambaye alikuwa na umri wa miaka **86**, alisema hivi: “*ngoja mapenzi ya*

Mungu yatimie". Aliwaruhusu maaskari waingie mlangoni. Kisha alikamatwa, na alipelekwa kwenye mamlaka ya Roma. Kamanda mkuu alimwambia Polycarp: "*kama utamwabudu Kaisari, na kumkana Yesu, nitakuacha huru*". Polycarp hakuogopa kitisho hiki. Alisema hivi: "*Kwa muda wa miaka 86, nimekuwa nikimtumikia Kristo, na hajanidhuru. Je, nitawezaje kumkufuru mfalme aliyeniokoa*"? Lakini kwa mara nyingine tena, kamanda mkuu alimwamuru amkane Kristo. Alisema: "*Nina wanyama wa mwitu, na kama hutabadili akili yako, nitakurushia kwao*". Na jibu la Polycarp lilikuwa rahisi. "*Waache wanyama wa mwitu waje*". Na kwa hiyo, kamanda mkuu alimwambia: "*Kama hutabadili akili yako, na kwa sababu huwaogopi wanyama wa mwitu, basi nitakuua kwa moto*".

Na mara nyingine tena, Polycarp alijibu bila hofu: "*kwa nini unachelewa? Fanya unachotaka. Mimi siogopi*". Maaskari walimshika, wakaanza kumgongomea misumari kwenye mbao, ili kwamba asiweze kutoroka. Lakini Polycarp aliwakitiza, na kuwaambia; "*Niachene kama nilivyo. Mungu atakayenisaidia kustahimili moto, pia atanisaidia kubaki juu ya moto. Hakuna haja ya kunifunga*". Kisha aliomba kwa sauti kubwa, na kujikabidhi mwenyewe kwa Mungu. Moto uliwashwa, na alichomwa hadi kufa. Huyu ni mtu huko Smirna, ambaye hakuogopa kufa kwa ajili ya Yesu. Sura **3:14** inasemaje? "*Msiogope kutisha kwao; msifadhaike*". Mateso yanapokuja - je, tunapaswa kuyakabili kwa namna gani? Pasipo hofu – Petro anasema. Lakini ili tufanya hivyo, tunahitaji msaada wa Mungu, ili atupe nguvu. Tunapaswa kufanyaje vitishwa vya mateso vinapokuja kwetu? Ngoja tufungue kifungu chetu katika sura **4:16**: "*Kama mtu akiteseka kwa sababu ni Mkristo, basi asione aibu, bali amtukuze Mungu, kwa sababu mtu huyo anaitwa kwa jina la Kristo*". Usione haya, bali mtukuze Mungu. Kwa kweli, unapoangalia **mst 13**, Petro anasema "*Furahini kwamba mnashiriki mateso ya Kristo*". Unaona, katika Agano Jipya, kuteseka kwa ajili ya Kristo, haikuwa ishara ya kutelekezwa na Mungu. Waumini hawakufikiri kwamba, Kristo alikuwa amewasahau. Badala yake, walifikiri hiyo ilikuwa ni ishara kwamba, neema ya Mungu ilikuwa ikifanya kazi katika maisha yao.

Na ndiyo maana, mara kwa mara, tunaona Wakristo wa mwanzo, wakitoka gerezani huku wakimsifu, na kumshukuru, Mungu. Walikuwa wakiambiana: "*Ni heshima kuteseka kwa ajili ya Bwana wangu. Yesu aliteseka kwa ajili yangu, na sasa katika kuitikia, ninateseka kwa niaba ya Kristo*". Tunapomwangalia Paulo, anaposhiriki mateso ya Kristo, badala ya kumkasirikia Mungu, anamsifu Mungu! Je, unaikumbuka hadithi, ambapo **Paulo** na **Sila** waliwekwa gerezani? Hawakufanya kitu chochote kibaya – lakini walikuwa wamekamatwa, na kuwekwa gerezani, kwa sababu ya kumtoa pepo msichana mmoja, katika jina la Yesu. Lakini katikati ya usiku, walikuwa wakiimba kwa kumsifu Mungu; walikuwa wanafurahia!

Matendo 16:22 unasema hivi: "*Mahakimu wakawavua nguo zao kwa nguvu, wakaamuru wapigwe viboko. Baada ya kupigwa sana wakatiwa ndani, na askari wa gereza akaamriwa kuwaweka chini ya ulinzi mkali*". Unaweza kupata picha, jinsi mambo yalivyo wakati umevulishwa nguo zako zote, na kusimama uchi, huku ukipigwa kwa rungu, tena na tena. Paulo na Sila walikuwa na majeraha, na vidonda juu ya miili yao. Vidonda vyao vilikuwa vinavuja damu. Hawakuweza kwenda hospitali! Badala yake, walifungwa na kutupwa gerezani. Lakini, walianza kuimba sifa kwa Mungu! Unaweza kufanya hivi, kama tu unampenda Bwana Yesu, na kama Roho Mtakatifu anafanyakazi ndani ya maisha yako. Walifurahia kwa sababu walijua kwamba, watakapoonekana mbele ya Yesu, wataweza kusimama mbele yake, pasipo kuona aibu. Angalia tena **mst 13**: "*Furahini kwamba mnashiriki mateso ya Kristo*". Kwa nini? "*ili muweze kuwa na furaha tele wakati utukufu wake utakapofunuliwa*". Kwa sababu walishiriki katika mateso ya Yesu, atakapokuja tena, wataweza kushiriki katika utukufu wake, mbele za ulimwengu wote! Na hili litakapotokea, watajawa na furaha, kiasi kwamba hawataweza hata kufikiri kuhusu mateso waliyoyapitia!

Petro anasema *'furahini katika mateso kwa ajili ya Kristo'*. Na anaweza kusema kwamba, kwa sababu yeye mwenyewe, aliipitia furaha hii. Katika **Matendo 5**, Petro alikuwa amekamatwa pamoja na wanafunzi wengine, kwa sababu ya kuhubiri kuhusu Yesu, na waliwekwa gerezeni. Katika usiku huo, malaika alikuja, na kufungua milango ya gereza, na mitume wakatoka nje. Walinzi hata hawakujua kwamba, mitume walikuwa wamekwenda hadi asubuhi! Siku iliyofuata, je, Petro na mitume, walienda wapi? Walirudi hekaluni, na kuanza kuhubiri tena! Viongozi wa Wayahudi hawakuweza kuamini jambo hili! Mwishoni, walifunguliwa kutoka mahakamani, na tumeambiwa kwamba walienda nyumbani huku wakifurahi, kwa sababu walikuwa wamehesabu kuwa ni fahari kuteseka kwa ajili ya Kristo (Matendo 5: 41).

Hatimaye, matokeo yake ni nini, kama tutateseka kwa ajili ya Kristo? Angalia sura **4:14**: *"Heri yenu ikiwa mnatukanwa kwa sababu ya jina la Kristo; jambo hilo lamaanisha kwamba Roho Mtakatifu, yaani Roho wa Mungu, anakaa nanyi"*. Hii ni ahadi ya ajabu! Utapokea msaada wa Roho Mtakatifu, utajisikia kujazwa na Roho Mtakatifu kadri anavyokuimarisha, na kukubariki. Hiki ndicho kilichowawezesha mitume, na watu kama Paulo, kuteseka kwa ajili ya Kristo. Walikuwa na utayari wa kuteseka, na kwa sababu hiyo, Roho Mtakatifu katika nguvu zake, alikuwa juu yao. Hii ni heshima ya namna gani! (Hadithi kuhusu **Mmasai**).

Je, Petro anasema nini? Rafiki wapendwa, msishangae kama mtateseka kwa ajili ya Kristo; ni kawaida. Mamilioni ya watu wameteseka kwa ajili ya Kristo – na hata sasa, watu wanakufa kwa ajili ya imani katika Kristo. Amua sasa, kama umeitwa kuteseka kwa ajili ya Kristo, utafanya hivyo. Kumbuka, yeye aliteseka kwa niaba yako. Katika nguvu za Roho Mtakatifu, furahia unapotukanwa kwa ajili ya Kristo. Utabarikiwa, na Roho Mtakatifu atakupua nguvu.

KIPINDI 9: 1 Petro 2:13-19, 3:1-7, 5:5-7: "Utii" **Steve Lancaster**

Hebu tufungue **1 Petro 2** na tutasoma **mst 13-19**. Na asubuhi hii, tunaangalia juu ya swala la *'utii'*, ambalo ni mojawapo ya mambo makubwa, ambayo Petro anayazungumzia katika barua hii. Ni somo kubwa sana, na ni somo lenye kuchanganya sana, kwa baadhi ya watu. Lakini Petro anapoangalia somo hili, anashughulika na makundi manne ya watu. **Kundi namba moja**: katika sura **2:13-17**, Petro anamwandikia kila mtu katika kanisa, na anazungumzia swala la **kuitii serikali**, na wale walio katika mamlaka. **Kundi la pili**: katika sura **2:18**, Petro anawaandikia watumwa na watumishi. Anamwandikia kila mtu aliye na ajira! Anazungumza kuhusu sisi kuwa watii kwa waajiri wetu. **Kundi la tatu**: kama unaangalia sura **3:1-7**, Petro anawaandikia wale walio oa, au kuolewa. Anawaagiza wake kuwa *'watii'* kwa waume zao - na waume kuwaheshimu wake zao. Na kisha, **kundi la nne**, katika sura **5:5**, anataja wanaume vijana katika kanisa, na anawaagiza kuwatii watu walio wazidi kiumri.

Je, neno *'utii'* linamaana gani hasa? Niliona kwamba maelezo haya yanasaidia. *"Utii ni kitendo cha kutii, mamlaka ya mtu mwingine"*. Kama askofu amekuambia kufanya kitu fulani, unapaswa kumtii, kwa sababu yeye yupo katika nafasi ya mamlaka juu yako. Unamtii yeye, kwa sababu yeye ni boshi wako. Na *'utii'* ni muhimu sana katika maisha yetu, na pia ni kitu muhimu sana, katika Ufalme wa Mungu. Mungu anawataka watoto wake wawe na utii kwake. Tunawezaje kufanya hivi? Kwa kuitii neno lake. Pia tunapaswa kuwa na moyo wa utii kwa ndugu zetu katika Kristo. **Waefeso 5:21**, uko wazi sana kuhusu jambo hili: *"Hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo"*.

Hata Yesu mwenyewe yuko chini ya mamlaka – yeye humtii Baba. Wakati wahuduma yake Yesu hapa duniani, siku zote alikuwa mtii kwa Mungu. Katika **Yohana 6:38**, anawaambia wanafunzi wake: “*Mimi siyo bos! Nimekuja kutoka mbinguni, siyo kwa ajili ya kuyafanya mapenzi yangu, bali kuyafanya mapenzi ya Baba yangu*”. Je, unakumbuka Yesu katika **Bustani ya Gethsemane**, katika usiku ule alipokamatwa? Aliomba: “*Baba kikombe hiki kiondoe kwangu, lakini kama ukisema kwamba ninahitaji kufanya hivi, basi nitafanya*”. Huu ni utii kamili kwa Baba yake. Utii, utii, utii! Na bado, hili ni neno, ambalo watu wengi hawalipendi. Kwa kweli ‘*utii*’ ni mojawapo ya mambo magumu sana, na maneno yasiyopendwa katika Biblia. Kwa nini?

Kwa sababu, mara kwa mara, hatupendi kuambiwa cha kufanya. Tunapenda kuwa waamuzi wa maisha yetu! Na kwa hiyo, wakati mwingine, tunaona kwamba ‘*utii*’ ni jambo gumu. Lakini Petro anasema, katika **mst 13** **. Na hii siyo sehemu pekee katika Agano Jipya, ambapo utii kwa serikali umeagizwa. **Paulo** anazungumza kuhusu *utii* katika **Tito 3**, na pia katika **Warumi 13**. Hata Yesu mwenyewe anatuambia kwamba, tunapaswa kuwa watii kwa serikali, katika kulipa kodi zetu (Luka 20:25). Hata kama hatupendi kufanya hivyo, na hata kama tunafikiri kwamba siyo haki, bado tunapaswa kuwa watii katika jambo hili. Tunapaswa kuishi kama raia wema, na kutii maagizo ya serikali, na pia mamlaka za serikali za mitaa.

Petro anatuagiza kuwa watii kwa mfalme, na kwa wale walio katika mamlaka. Sasa, najua kwamba **Tanzania** haina mfalme - lakini ina rais. Na kwa hiyo, ujumbe kwetu ni kwamba, tunapaswa kuwa watii kwa rais, na serikali ya Tanzania - na pia, kwa viongozi wa serikali zetu za mitaa - hata kama siyo Wakristo! Unapofikiri kuhusu jambo hili, haya hapa ni maneno ya kushangaza kutoka kwa Petro. “*Mtiini mfalme, na serikali yake*”. Petro alipokuwa anaandika barua hii - je, nani alikuwa mfalme? Alikuwa mtu mmoja aliyetitwa **Nero**, naye hakuwapenda Wakristo! Ni mtu huyu, ambaye baadaye aliwaua Petro na Paulo! Alikuwa mfalme wa **Roma**, akiwa na umri wa miaka **16**, na alitawala kwa miaka **14**. Lakini wakati wa utawala wake, aliwaua mama yake mzazi, na mke wake! Kila mtu aliyempinga aliuawa pia. Alipandisha kodi, ili kwamba aweze kujenga nyumba za gharama kubwa kwa ajili yake. Na watu wengi walifikiri kwamba alikuwa mwovu, na hakujuu tofauti kati ya jema au baya. Katika mwaka **64**, baada ya Yesu kuzaliwa, kulikuwa na moto mkubwa katika mji wa Roma, ambao ulichukua siku **6** kuzimika, na uliteketeza sehemu nyingi za jiji. Wanahistoria wanafikiri kwamba, Nero mwenyewe aliwasha moto huo, ili kwamba aweze kujenga nyumba zake mwenyewe. Lakini, Nero aliwasingizia Wakristo katika Roma kuwa waliwasha moto huo, na aliwakamata Wakristo wengi. Baadhi yao waliuawa kikatili. Waliwekwa katika mazizi pamoja na simba, na simba waliwavamia na kuwala. Baadhi yao walisulubiwa, na wengine walichomwa moto wakiwa hai. Nero ndiyo alikuwa mtu waaina hii. Alikuwa mtu katili asiyewapenda Wakristo. Na bado, katika **mst 13**, Petro anasema hivi: “*Mtiini mfalme, na serikali yake*”. Kwa nini? Kwa nini tuwe watii kwa mamlaka inapokuwa na tabia ya namna hii?

Hebu angalia tena **mst 13**: “*Tiini – kwa ajili ya Bwana*”. Unaona, mamlaka ya mfalme na serikali, zimewekwa na Mungu - na kwa hiyo wale wasiyo taka kutii sheria za nchi, kwa kweli hawamtii Mungu. Fungua **Warumi 13:1-2** – na angalia Paulo anasema nini kuhusu hili **. Sasa, tunapaswa kuwa makini hapa. Paulo hasemi kwamba, serikali mbaya - ni nzuri. Hasemi kwamba kila kitu anachofanya mfalme, au rais, ni kizuri. Bali, kwa ajili ya faida ya jamii, Mungu aliamua kwamba, tuwe na mfumo wa kusimamia sheria, na maagizo, ya jamii zetu. Kama hakuna sheria katika jamii, basi kutakuwa na machafuko, na kila kitu kitaharibika. Na tunaweza kuona kwamba yanatokea katika nchi kama **Somalia**, **Yemen**, na **Siria**. Mungu alipanga kwamba, kuweko na serikali na wafalme, watakaongoza watu.

Na kama tunavyosoma katika sura **2:14**, tunaweza kuona sababu ya kuwepo kwa jambo hili. Angalia **mst 14**: “wanatumwa naye ili kuwalipiza kisasi watenda mabaya, na kuwasifu watenda mema”. Hiyo ni kazi ya serikali. Na wanapofanya hivyo – kila kitu kinakwenda vizuri. Tatizo ni kwamba, leo, kuna baadhi ya serikali katika ulimwengu, ambazo zimejaa dhuluma na hazina haki, na hazifanyi kazi ya kuwaadhibu watenda mabaya. Hilo siyo kosa la Mungu. Mungu hakumthibitisha **Nero**. Mungu hakuthibitisha tabia ya Robert Mugabe. Mungu hawathibitishi marais wabaya, na serikali mbaya – lakini mfumo wa mamlaka alioweka katika utaratibu utafanya kazi - kama serikali na viongozi watafanya kazi kama inavyotakiwa. Na kwa hiyo, tunahitaji kutii mamlaka zao.

Katika **mst 18 & 19**, anawaagiza wafanya kazi kuwatii mabwana zao - hata kama waajiri hao watawatendea vibaya. Kama si waaminifu, na hata kama hawakujali, hakikisha kwamba unakuwa mtii kwao. Kwa nini? Kwa ajili ya Bwana. Na kama unaangalia **mst 15**, utaona kwamba kama Mkristo ni mtii, ni ushuhuda mzuri kwa Yesu. Petro anasema: “Kwa sababu ndiyo mapenzi ya Mungu, kwamba kwa kutenda mema, mzibe vinywa vya ujinga vya watu wapumbavu”. Kwa maneno mengine, usimpe nafasi adui yako ya kukutuhumu kwa kosa lolote. Kwa hiyo, hakikisha kwamba unamtii mfalme kadri iwezekanavyo, ili kwamba watu hawa wasiseme jambo lolote baya kuhusu ninyi. Kama utaitii mamlaka, jina la Yesu litatukuzwa. Kwa kweli, utakuwa unaiga tabia ya Yesu, na utaleta utukufu kwa Mungu.

Lakini – ninahitaji kusema kitu fulani hapa. Tiini mamlaka; mtiini mfalme; itiini serikali – **isipokuwa** watu wanapowaambia kufanya kitu fulani, ambacho ni kinyume na Mungu, na neno lake. Na kwa hiyo, kanuni hapa ni hii: siku zote tii, isipokuwa unapoamrisha kutenda dhambi. Unaposoma Biblia yako, utaona kwamba kuna wakati katika Biblia, ambapo watu wa Mungu hawakumtii mfalme au serikali, na Mungu amewasifu kwa kufanya hivyo. Ngoja niwape mifano michache: Katika Kitabu cha **Kutoka 1**, mfalme wa Misri, Farao, aliwaagiza wakunga wa **Kiebrania**, kuwaua watoto wakiume wanapozaliwa.

Na tumeambiwa kwamba wakunga hao, walikuwa na hofu ya Mungu, na waliamua kutoitii amri ya Farao. Katika **mst 20** tumeambiwa kwamba “Mungu alikuwa mwema kwa wakunga hao”. Katika hali kama hii, Mungu alithibitisha uasi wao kwa mfalme, kwa sababu walichokuwa wameambiwa kufanya na Farao, kilikuwa kibaya. Katika Kitabu cha **Danieli 3**, Danieli na rafiki zake, waliagizwa na mfalme, kuabudu sanamu ya dhahabu, iliyokuwa imetengenezwa. Je, walifanya nini? Walikataa. Ingawa mfalme aliwatahisha kuwatupa katika moto, bado walikataa kutii. Kwa nini? Kwa sababu walijua kwamba, kama wangemtii mfalme, basi wangemuasi Mungu. Je, cha muhimu zaidi ni nini? Kwa kweli – ni kumtii Mungu. Lakini kufanya hivyo katika hali yao, lilikuwa jambo la kijasiri sana. Na pia ilitokea tena. Katika **Danieli 6**, mfalme **Dario** alipitisha sheria. Alisema hivi: *Mnapaswa kuniabudu mimi tu – siyo miungu mingine*. Na kwa hiyo, Danieli aliamriwa asimwombe Bwana Mungu. Je, alifanya nini? Alikataa. Aliendelea kuomba. Na tunajua kwamba alitupwa katika tundu la simba – lakini aliokolewa na Mungu. Hii ni habari yenye nguvu sana ya Mungu akimlinda Danieli, alichagua kumheshimu yeye badala ya mfalme. Alimtangukiza Mungu.

Kuna mfano mwingine katika Agano Jipya. Katika **Matendo 4**, Petro na Yohana walikuwa wamekamatwa, kwa sababu ya kuhubiri kuhusu Yesu. Walikuwa wameagizwa na viongozi wa Wayahudi, kwamba wasifundishe tena. Je, walifanya nini? Walikataa kutii agizo lao. Katika **mst 19**, kuna jibu la kijasiri kutoka kwa Petro: “Ni haki mbele za Mungu kuwasikiliza ninyi, kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe. Maana sisi hatuwezi kuacha kuyanena mambo, tuliyoyaona na kuyasikia”.

Hili ni jibu la ajabu – na ni jibu la kijasiri. Na kwa hiyo, tunaweza kuona kutoka kwenye Biblia, kwamba kuna nyakati, ambapo ni sahihi kutowatii wafalme, na serikali - lakini kabla hatujafanya hivyo, tunahitaji kuwa na uhakika kwamba, majibu yetu ni ya kibiblia. Hii ni kanuni: “*Waheshimuni watu wote. Mcheni Mungu. Mpeni heshima mfalme*”. Hivi ndivyo unavyosema **mst 17**. Siku zote tiini mamlaka, **isipokuwa** unapokuwa umeagizwa kutenda dhambi na kumuasi Mungu.

Kabla hatujamaliza kipindi chetu asubuhi hii, ninataka tuangalie kile ambacho Petro anawaambia **wake** na **waume** - kwa hiyo tufungue sura **3**, na tutasoma **mst 1-7** **. “*Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu*”. Kama jinsi tunavyotii wenye mamlaka na waajiri, vivyo hivyo anataka wake wawatii waume zao. Tafadhali tambua kwamba, waume hawajaambiwa kuwatii wake zao. Katika **mst 17**, waume wameambiwa kuwaheshimu wake zao. Kama wewe ni mwanaume uliyeoa, mke wako anahitaji matunzo, upendo, na heshima kutoka kwako. Lakini kamwe mume, hujaambiwa kumtii mke wako.

Hii ndiyo namna ambavyo Mungu amefanya. Huu ni utaratibu wa kibiblia. **Paulo** pia anazungumza kuhusu wake na waume katika kanisa. Na anasema kitu kile kile kama Petro, katika **Waefeso 5:21**: “*Enyi wake, watiini waume zenu, kama kumtii Bwana wetu*”. Kwa hiyo, jambo hili liko wazi, tunaposoma Agano Jipya kwamba, haya ni maagizo ya kibiblia, na kwamba yanatuhusu sisi leo. Sasa, kwa baadhi ya wanawake, hasa katika nchi za magharibi, hapa ndipo neno ‘*utii*’ huanza kuleta mkanganyiko. Wanawake wengi katika Uingereza, hasa wale wasio Wakristo, hawata-kubaliana na Petro. Kwa kweli, baadhi yao wangeweza kukasirika sana, kama utawaambia kwamba, wanapaswa kuwatii waume zao, kwa sababu hawataki kufanya hivyo. Badala ya neno ‘*utii*’, wanaona maneno kama ‘*kunyanyaswa, kugandamizwa, kutawaliwa*’. Wanaona swala la ‘*utii*’ kama jambo baya, na siyo kitu chema – na bado mwanzoni, liliumbwa kuwa kitu chema. Mwanaume aliumbwa kuwa mtu mnyenyekevu, na mwenye upendo, aliyemwongoza mke wake katika ndoa. Na mwanamke kwa hiari, na kwa kupenda, alitii uongozi wa mume wake. Lakini, baadaye dhambi ikaja! Dhambi ilipoingia ulimwenguni, kupitia **Adamu** na **Eva**, mambo yakachanganywa. Badala ya kuwa mnyenyekevu, na mwenye upendo kwa mke wake, mwanaume akaanza kumnyanyasa, na kumgandamiza mke wake.

Na matokeo yake, wanawake wakawa hawataki kutii, na wakaanza kuasi dhidi ya waume zao. Dhambi imetawala na kuharibu picha kamili ya ndoa – na kwa hiyo sasa, kwa wanawake wengi, suala la utii kwa waume zao, siyo kitu kilichozoeleka. Kwa hiyo, tunapoangalia somo hili, ninataka tuelewe Petro anamaana gani anapotoa amri hii, na pia tuelewe ambacho hasemi kuhusu jambo hili la utii. Lakini nafikiri pia itatusaidia tukisoma ambacho Paulo, anasema kuhusu utii na ndoa pia. Hebu ngoja turudi katika **Waefeso 5**, na tutasoma kuanzia **mst 22-33** **. Kwa dakika chache, nataka tulenge katika kifungu hiki, na tuone lengo la Mungu katika ndoa. Hili ni muhimu katika majadiliano yetu juu ya ‘*utii*’. Angalia tena **mst 31**: Na hapa Paulo ana nukuru kutoka **Mwanzo 2:24**: “*Kwa hiyo mwanaume atamwacha baba yake, na mama yake, naye ataambatana na mkewe, nao watukuwa mwili mmoja*”. Je, tunajua nini kutoka mstari huu? Tangu mwanzo, tunajifunza kutoka kitabu cha kwanza cha Biblia, kwamba ndoa ni mpango wa Mungu. Siyo uvumbuzi wa mwanadamu. Lakini angalia mwanzoni mwa **mst 32**, kwa sababu kama vile Paulo anavyofikiri kuhusu ndoa, anasema hivi: “*siri hiyo ni kubwa*”. Sasa, kwa nini Paulo anasema kwamba ndoa ni siri? Jibu lipo mwishoni mwa **mst 32**, kwa sababu Paulo anasema hivi: “*mimi ninazungumza kuhusu habari ya Kristo na kanisa*”.

Je, kuna uhusiano gani kati ya ndoa, na Kristo na kanisa? Je, yanahusiano gani? Na kwa nini ni siri? Basi, kabla ya Yesu kuja kufa msalabani, maana kamili ya ndoa, ilikuwa imefichwa kwa kiasi fulani. Watu walijua kwamba ndoa inatoka kwa Mungu, lakini hawakujua kwamba pia ilikuwa na

maana ya ndani sana. Kuna uhusiano na Kristo. Paulo anasema ndoa ni picha ya Yesu, na kanisa. Uhusiano kati ya mume na mkewe, umeumbwa kwa ajili ya kuuaksi uhusiano kati ya Kristo, na kanisa. Kama vile mume na mke, walivyo kitu kimoja pamoja, vivyo hivyo kanisa ni mwili wa waumini, wa Kristo. Na hii ndiyo maana ndoa ni kitu muhimu sana. Kuna uhusiano wa kiroho.

Na katika kifungu hiki, Paulo anatuonesha kwamba, Mungu ametoa majukumu tofauti kwa wanaume na wanawake, katika ndoa. Hayakutokea menyewe, au kwa bahati mbaya. Mungu alikuwa na malengo, katika kutoa majukumu kwa mume, na majukumu kwa mke. Na hatupaswi kuyapindisha. Na mojawapo ya majukumu ambayo amepewa mwanaume, ni kuwa kiongozi katika ndoa; kichwa cha familia. Na majukumu ambayo Mungu amewapa waume na wake, yanaakisi majukumu ya Kristo, na kanisa. Kwa maneno mengine, ndoa inapaswa kuwa shahidi kwa ulimwengu; picha ya jinsi Yesu, alivyo na uhusiano na kanisa lake.

Angalia **mst 23**: “*kwa maana mume ni kichwa cha mkewe – kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa*”. Na kisha katika **mst 25**: “*Enyi waume, wapendeni wake zenu – kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake*”. Je, unaona uhusiano huu? Waume, uangalieni mstari huu kwa makini sana! Waume wanapaswa kuwapenda wake zao, kama Kristo naye anavyolipenda kanisa. Fikiri kuhusu hili. Je, Yesu alifanya nini ili kutuonesha upendo wake? Alijitoa mwenyewe kwa ajili ya kanisa. Alikufa msalabani kwa ajili yetu. Alitoa maisha yake kuwa sadaka kwa ajili yetu. Kama kiongozi katika ndoa, mume ameagizwa kumpenda mke wake, kama vile Kristo alivyolipenda kanisa. Na jukumu la mke ni kumpenda mumewe, na kutii uongozi wake, kama vile kanisa linavyotii uongozi wa Yesu Kristo. Sasa, tumeangalia jinsi ulivyo utii wa kibibilia – lakini nataka kuoneshe utii usio wa kibibilia. Mke anapomtii mumewe, kama Petro na Paulo wanavyoagiza, haimaanishi kwamba, yeye anahadhi ya chini kwa mumewe. Haimaanishi kwamba mume ni bora kuliko mke. Haimaanishi kwamba mume ni mtu muhimu kuliko mke. Wote ni sawa mbele ya macho ya Mungu. Utii hauna maana kwamba mume anahaki ya kumpiga mke wake. Hiyo itakuwa siyo sahihi.

Utii hauna maana kwamba, mume anaruhusiwa kumtendea mke wake vibaya. Kama atafanya hivyo, atakuwa anapuuza kile, ambacho Petro anasema katika **mst 7**.

Mwanzoni tulipozungumza kuhusu kuitii serikali, nilisema kwamba, kila siku tunapaswa kuzitii mamlaka, **isopokuwa** zinapotuagiza kumtenda dhambi Mungu. Na kanuni hiyo pia inahusika hapa, tunapozungumza kuhusu utii wa wake kwa waume zao. Kwa mfano: kama mume atamwambia mke wake, kuiacha imani yake katika Kristo, basi huyo mke anapaswa kumtii Mungu, badala ya mume wake. Kama mume anamwambia mke wake kutenda dhambi, basi mke atakuwa na haki ya kuacha kumtii. Utii hauna maana kwamba, mke hapaswi kufanya chochote hata kama mume wake hana uaminifu kwake. Utii hauna maana kwamba, kama mume anaendelea kumnyanyasa mke wake, kwamba anapaswa kukaa kimya, na kukubali ukatili wake. Hapaswi kufanya hivyo. Kwa hiyo **1 Petro 3:1** ungesema hivi: “*Wake watiini waume zenu – isipokuwa wanapowaambia kumtenda dhambi Mungu*”.

Lakini Petro pia anazungumza kuhusu jambo lingine hapa. Anatoa ushauri kwa mke, ambaye mume wake siyo Mkristo. “*Mke mtii mume wako – hata kama haamini Neno la Mungu*”. Na kisha mwishoni mwa **mst 1**, anasema kwamba, tabia ya mke ni muhimu sana. Inatarajiwa kwamba, mume asiye Mkristo anapomwona mke wake akimtii, yeye naye atataka kuwa Mkristo. Kadri anavyoona tabia nzuri ya mke wake, na heshima yake kwa Mungu, atavutiwa na injili. Na kwa hiyo, katika hali hii, utii wa mke kwa mume ambaye si Mkristo, unaweza kuwa njia nzuri ya kumleta kwa Yesu. Petro anasema kwamba, matendo yananguvu kuliko maneno. Hata anapendekeza katika

mst 1, kwamba mke hata haihitaji kumhubiri neno mume wake, lakini anachohitaji ni kuonyesha utii pamoja na tabia yake nzuri kwa mumewe. Lakini kuna kitu kingine, ambacho Petro anataka kuwaambia wake.

Ni kuhusu tabia na uzuri. Angalia **mst 3-4** **. Je, hii inamaana gani? Je, Petro anasema kwamba wanawake hawapaswi kuvaa mavazi mazuri katika kanisa? Je, mstari huu unamaana kwamba, tunapaswa kuweka mabango, katika milango ya makanisa, yaliyoandikwa: “*Wanawake hawaruhusiwi kuvaa vitu vya dhahabu; hawaruhusiwi kusuka nywele zao*”? Je, hiki ndicho anachosema Petro hapa? **Hapana**. Ninafikiri kwamba ni sawa kwa wanawake kuvaa vitu vya dhahabu katika kanisa, na ni sawa kwa wanawake kuvaa mavazi mazuri. Wanaruhusiwa kupendeza! Lakini - jambo muhimu zaidi kwa Mungu, ni ule uzuri wao wa ndani. Petro anawaambia wake, na wanawake wote kwa ujumla, tafadhali msifikiri kwamba, mwonekano wenu wa nje ni muhimu – sivyo. Anachoangalia Mungu ni mambo ya ndani. Ni tabia yako, na matendo yako, ndiyo muhimu zaidi. Uzuri wa nje utaharibika kadri unavyozeeka, lakini tabia yako ya ndani, itadumu milele. Angalia **mst 4**: Petro anasema hivi, badala ya kutegemea mavazi mazuri, na vitu vya dhahabu ili kupendeza, fikiri kuhusu utu wako wa ndani, siyo utu wa nje. Tabia yako, na roho yako, ni vya thamani kwa Mungu kuliko mwonekano wako wa nje.

Kwa huzuni, katika ulimwengu wa leo, hasa katika nchi za magharibi, watu wengi hawafikiri kwamba hii ni kweli. Unapotazama TV, matangazo yakibiashara yanakuambia kwamba, unapaswa kuonekana vizuri kwa nje. Magazeti pia yanakuambia hivyo, ili uonekane vizuri, unapaswa kutumia pesa nyingi kwa ajili ya mavazi - kwa sababu kama hutafanya hivyo, watu hawatakupenda. Katika **UK** na **Marekani**, kuna kutekwa na uzuri, na mwonekano wa nje. Kwa wanawake wengi, na hata wanaume wengi, mwonekano wa nje ni muhimu zaidi kuliko mwonekano wa ndani. Nafikiri kwamba hili pia limekuwa tatizo hapa Tanzania. Jambo hili linaweza hata kuleta mgogoro katika ndoa pale mwanamke anapotaka kutumia pesa nyingi, kwa ajili ya nguo mpya, na mtindo mpya wa nywele.

Katika siku za Agano Jipya, baadhi ya wanawake walitekwa na mwonekano wa nywele zao, na hili lilikuwa tatizo katika baadhi ya makanisa. Paulo hata alimwandikia **Timotheo** kuhusu jambo hili. Baadhi ya wanawake walikuwa wanafanya maonesho kanisani. Walikuwa wakitumia muda mwingi sana, na pesa nyingi, wakijiandaa kwa ajili ya kanisa. Walivaa mavazi, na vitu vya dhahabu vya gharama, kwa sababu walitaka kila mtu awatazame wao. Lakini hivi sivyo inavyopaswa kuwa. Na kwa hiyo, Petro anawaambia wanawake, msitumie muda mwingi sana, katika kutengeneza mwonekano wenu wa nje, bali badala yake, hakikisheni kwamba, mnatumia muda mwingi, katika kutengenza tabia zenu, na kukua kwenu kiroho. Huko ndiko uliko uzuri. Kama wake watii, zingatieni kuikuza roho ya upole, na utulivu. Na Petro anasema katika **mst 5**, hivi ndivyo walivyofanya wanawake watakatifu wa zamani, ili kujifanya wawe wazuri. Waliwatii waume zao, na waliwatii kwa tabia ya upole. Na katika **mst 6**, Petro anatoa mfano wa **Sara**, mke wa **Abrahamu**, kama mwanamke aliyekuwa mtii kwa mume wake.

Utii kwa serikali. Utii kwa waajiri. Na utii wa wake katika ndoa. Kwa nini tunapaswa kuwa watii? Kwanza, kwa sababu Neno la Mungu linaagiza hivyo. Pili, kwa ajili ya Bwana. Tunapoonesha utii kwa mamlaka hizi, na watu wengine, tunamtii Mungu, na tunalipa utukufu jina lake.

KIPINDI 10: 1 Petro 5:1-5: Wachungaji wa Kundi Steve Lancaster

Tufungue Biblia zetu tena – na safari hii, tunaenda kuangalia, sura ya mwisho ya barua hii. Ngoja tusome **1 Petro 5:1-5**. Na mistari hii inauhalisia kwa viongozi wa kanisa, na wachungaji, na wainjilisti. Kumbuka, Petro anawaandikia Wakristo ambao wametawanyika katika mikoa mitano tofauti katika **Asia Ndogo**. Anamwandikia kila mmoja katika makanisa haya, lakini pia anasema na makundi ya watu mbali mbali, katika barua hii. Katika **sura 2**, anawaandikia watumwa, au wafanyakazi. Anawaagiza kuwa watiifu kwa waajiri wao. Katika **sura 3**, anawaandikia wanawake walioolewa; anawaagiza wanawake kuwa watiifu kwa waume zao - kama tulivyoona jana. Katika **sura 3**, anawaandikia wanaume waliooa, na anawaagiza kuwapenda wake zao. Na kisha, kama unavyoweza kuona katika **sura 5:1**, anawaandikia wazee wa kanisa katika makanisa haya. Anawashauri wazee na wachungaji, jinsi ya kuenenda katika kazi yao – na hiki ndicho tutakuwa tunaangalia katika kipindi hiki. Na kisha, katika **mst 5-9**, ninafikiri kwamba, anatoa maelekezo ya jumla kwa wazee, na wachungaji, na kila mmoja katika kanisa, Utaona katika **mst 5** anasema kwamba: “*ninyi nyote, jifungeni unyenyekevu mpate kuhudumiana*”.

“*Nawasihi wazee walio kwenu*”. Vipi kuhusu neno hili ‘**wazee**’. Tafadhali usifikiri kwamba, mistari hii inawahusu watu katika kanisa, ambao wana nafasi ya uongozi ya wazee. Neno ambalo limetumika katika lugha ya Kigriki, linajumuisha: wazee, maaskofu, viongozi wa kanisa, wachungaji, na wainjilisti pia. Hawa ni watu wenye wajibu kwa afya ya kiroho ya kanisa. Na kwa hiyo, mistari hii inawahusu ninyi nyote leo. Umepewa wajibu wa kuongoza kanisa lako. Unawajibika juu ya afya ya kiroho, ya waumini wako. Hili ni jukumu kubwa sana, lakini pia ni nafasi ya upendaleo! Je, wewe ni mchungaji mzuri, au ni mchungaji mbaya? Je, unalilisha kundi lako chakula kizuri, au chakula kibaya? Je, unatunza kundi lako, au unawatelekeza washirika wako? Je, wewe ni mfano mzuri kwa kundi lako?

Ninataka utambue kwamba katika **mst 1**, Petro anajiita mwenyewe mzee mwenzi. Nafikiri kwamba jambo hili, linaonesha unyenyekevu wake hapa. Mwanzoni mwa barua, Petro anasema: “*Mimi Petro, mtume wa Yesu Kristo*”. Na kama mwanafunzi wa Yesu, alikuwa anaitwa mtume – alikuwa mtu ambaye alitumwa na Kristo mwenyewe. Na kwa hiyo, cheo hicho kilimpa mamlaka. Alikuwa miongoni mwa viongozi wakuu wa kanisa, na kila mtu alimjua Petro ni nani. Lakini hapa, katika **mst 1**, anapowaandikia wazee na wachungaji wa makanisa haya, anasema: “*Nawaandikia nikiwa mzee mwenzi wenu*”. Kwa maneno mengine, ‘*mimi ni mmoja wenu*’. Ingawa ni mmoja wa viongozi wa kuu katika kanisa, anafuraha kujitambulisha mwenyewe, pamoja na wazee wa kawaida, ambao anawaandikia.

Kama mchungaji, unyenyekevu ni kitu muhimu sana - ndiyo maana Petro anajitaja mara nyingi, katika kifungu hiki. Na bado, ndani ya kanisa, baadhi ya watu wanahimiza kwamba waitwe kwa vyeo vyao. Wanapoenda kwenye vikao, wanawataka watu wawaite kwa vyeo vyao, kwa sababu wanafikiri kwamba wao ni muhimu sana! Ngoja ni wape mfano. Miaka mingi iliyopita, niliandaa mkutano, na kuwaalika watu kuja kwenye mkutano. Nilikuwa mwenyeji wa mkutano, na nilikuwa nimemwomba mkurugenzi wa chama cha Wakristo kuja, kuzungumza katika tukio hilo. Na muda mfupi kabla hajaanza kuhutubia, aliniambia kwamba nimtambulisho kama mkurugenzi wa chama. Alitaka cheo chake kitajwe kikamilifu – siyo jina lake tu, lakini cheo chake, ingawa kila mmoja katika ukumbi, alimjua yeye ni nani! Alijisikia kuwa ni muhimu – na alitaka watu wajue kwamba yeye ana nafasi muhimu.

Katika **sura 5:5**, Petro anasema kwamba, hatupaswi kujivuna. Badala yake, tunapaswa kujinyenyekeza. Ngoja pia ni kupe mfano mwingine mzuri wa unyenyekevu. Miaka michache iliyopita, nilikuwa **Nairobi** nikihudhuria mkutano wa **AIM**. Nilikuwa nikikaa katika nyumba ya wageni, na rafiki mmoja akaja kunitembelea. Alikuwa rafiki kutoka **Burundi**, ambaye alijihusisha na huduma ya wakimbizi wa **Kirundi**. Tulipokuwa tunaongea pamoja, mmoja wa viongozi wakuu wa AIM, akaja ndani ya chumba. Alikuwa mmoja wa viongozi wenye mamlaka makubwa, na watu wengi walimheshimu. Na kwa hiyo, nilimtambulisha rafiki yangu Mrundi kwake, na wakaanza kuongea pamoja. Rafiki yangu kutoka Burundi, alimuuliza kiongozi wa AIM: *'je, unafanya nini katika AIM?'*

Sasa, kiongozi angeweza kusema: *'mimi ni mkurungenzi msaidizi wa AIM. Mimi ni wa pili katika taasisi yote. Ninanafasi muhimu katika huduma'*. Lakini hakusema kitu chochote kati ya vitu hivi. Alisema hivi: *'ninafanya kazi katika taasisi ile ile, ambayo Stefano anafanyia'*. Hivi ndivyo alivyo sema kuhusu kazi yake. Na nilivutiwa sana na jibu lake. Hakujisikia kusema kwamba: *'mimi ni mmoja wa mabosi wakubwa katika AIM'*. Vyeo na nafasi, havikuwa kitu kwa kiongozi huyu. Alikuwa mnyenyekevu, na hakujivuna. Je, unaona tofauti kati ya watu hawa wawili? Kiongozi mmoja alitaka kusikia cheo chake kimetajwa, kwa sababu kilimpa umuhimu na heshima – na kiongozi mwingine hakutaka kutumia cheo chake, kwa sababu lengo lake lilikuwa unyenyekevu. Alitaka kujitambulisha pamoja nami kama mfanyakazi wa kawaida katika AIM.

Na ninafikiri kwamba hivi ndivyo anavyofanya Petro hapa, katika **mst 1**. Petro hajichukulii kama boshi mkubwa, anayekaribu kuwavutia watu kwa nafasi yake katika kanisa. Hasemi kwamba: *"ninyi watu ni wazee wa kanisa tu, lakini mimi ni mtume"*. Anazungumza, *"kama mtu fulani ambaye ni mzee mwenzao, niko pamoja nanyi; mimi ni mmoja wenu; najua nini maana ya kuwa mzee wa kanisa – kwa hiyo, nataka kuwatia moyo ninyi"*. Na kisha katika **mst 2**, Petro anaanza kuzungumza kuhusu kazi ya mchungaji. *"Lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu"*. Na katika lugha ya Kigriki, inasema hivi *"wachungeni kondoo wa Mungu"*. Na hii inavutia – kwa sababu neno *'kondoo'* ambalo limetumika hapa, ni neno lile lile, lililo tumika katika **Yohana 21**. Je, unakumbuka maongezi ambayo Yesu alifanya pamoja na Petro, karibu na ziwa Galilaya, baada ya Yesu kufufuka kutoka wafu? Ni hadithi ya ajabu. Yesu anamwambia Petro mara **3**: *"Je, wanipenda"*? Na kila wakati, Petro anasema: *"ndiyo Bwana, wewe unajua nakupenda"*.

Je, Yesu anasema nini katika kumjibu Petro? Anazungumza kuhusu kuwa mchungaji mwema. *"Lisha kondoo zangu"*. *"Linda kondoo zangu"*. *"Lisha kondoo zangu"*. Na ninahakika kwamba, Petro anapoongea kuhusu kuwa mchungaji mwema, hapa katika **sura 5**, anakumbuka nyuma katika wakati huu, ambapo Yesu alimwambia kuwa mchungaji mwema. Lazima jambo hili, lilikuwa mojawapo ya mambo aliyoyakumbuka sana. Petro alikuwa amemkana Yesu – lakini alikuwa amesamehewa na Kristo, na kisha Yesu anamwelekeza kuwa mchungaji mwema. Hii inaniambia kwamba, hata kama mimi ni mwenye dhambi, Mungu ananisamehe na anataka kunitumia.

Petro alikuwa mchungaji wa kwanza! Kama mchungaji, alipewa wajibu wake na Yesu mwenyewe. Na sasa, anawapa wengine kile ambacho kilisemwa kwake na Yesu, kwa wazee wa kanisa wote, na wachungaji, ambao anawaandikia - tukiwemo wewe na mimi. Kama mchungaji au mwinjilisti, ni kazi yako kulisha kondoo wa Mungu, na kuwalinda. Na kama nilivyosema mwanzo, umepewa kazi ya kuongoza kanisa lako. Unawajibika kuhusu afya ya kiroho ya washirika wako. Ni jukumu kubwa sana, lakini pia ni upendeleo mkubwa. Unajisikiaje kuhusu kazi yako? Je, unaifurahia, au huipendi? Kutoka kifungu hiki, tunawezaje kujua kama sisi ni wachungaji wazuri?

Petro anapendekeza njia nzuri chache, za namna ya kuwa mchungaji mzuri, lakini pia anatuambia mambo tunayopaswa kujiepusha nayo. **Mst 2:** “*Lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia. Si kwa kulasimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo. Si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo*”. Kwa hiyo, kama unataka kuwa mchungaji mzuri, unapaswa kuwa mtu anayetumikia kundi. Petro anasema hakikisheni kwamba mnawatumikia wengine kwa hiari – kwa sababu hivyo ndivyo Mungu anavyotaka. Usijaribu kuwatumikia wengine kwa sababu tu, umeagizwa ufanye majikumu ya kazi yako. Unapaswa kuwatumikia wengine, kwa sababu unataka kutoka moyoni. Ngoja niseme neno la angalizo hapa. Kama umeshinikizwa kuwa mchungaji, wakati hutaki kufanya hivyo – basi umefanya kosa. Kama umekuwa mchungaji kwa sababu inakufanya ujisikie kuwa mtu muhimu - basi uko katika kazi isiyo sahihi. Tunakuwa wachungaji kama tunataka kuwatumikia wengine – hivyo ndivyo anavyofanya mchungaji mwema. Ngoja nifafanue hapa. Kama wewe ni mchungaji – na hutaki kutumika, basi nenda kwenye ofisi ya dayosisi haraka, na ukajiuzulu! Upate kazi nyingine! Kazi ya mchungaji ni kutumikia. Inahusu kuwa mtumishi.

Unaweza kukumbuka, mwaka jana, katika moja ya vipindi vyetu, tuliangalia juu ya somo la kiongozi mtumishi na mnyenyekevu. Je, inamaana gani kuwa mchungaji anayetumikia watu wake? Na tuliangalia mfano wa Yesu akiosha miguu ya wanafunzi wake, katika Chumba cha Juu. Katika kitabu chake, “*Nioneshe Kiongozi Mwadilifu*”, **Askofu Mtetemela**, alisema hivi: “*mojawapo ya malengo ya kitabu hiki, ni kuweka mkazo juu ya aina hii ya uongozi. Hii ni kuhusu huduma. Haihusu kutafuta cheo cha juu, au umuhimu. Utumishi ni kitu ambacho ni msingi wa watumishi wote wa Kikristo. Kuwa kiongozi ni ishara ya mtu aliye jitoa kumfuata Yesu Kristo*”.

Na kama wewe unatazamiwa kumfuata Yesu, basi huwezi kupuuza ukweli kwamba, Yesu alikuwa kiongozi aliyekuwa mtumishi. Yesu aliwaambia wanafunzi wake, katika **Mathayo 20:28:** “*Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika*”. Huu ni mfano wetu - Bwana Yesu Kristo, na kama hufuati mfano wake, basi, wewe siyo mchungaji mzuri. Ninafikiri kwamba, uongozi mbaya ni jambo kubwa katika Afrika, na katika nchi nyingi ulimwenguni. Katika siasa, na biashara, sote tumesikia hadhithi za viongozi, ambao hawafikiri kwamba, uongozi ni kuhusu kuwatumikia wengine. Badala yake, wanafikiri kwamba kila mtu anapaswa kuwa-nyenyekea wao! Lakini, pia nafikiri kwamba hili nitatizo katika makanisa mengi. Viongozi wengi, na wachungaji wengi, hupata shida kuiga mfano huu wa uongozi. Bila shaka, kuna wachungaji, na hata maaskofu, ambao hutaka tu kuwa kwenye nafasi hizo za uongozi, ili wawe watu wakubwa! Wanafikiri kwamba wao ni watu muhimu sana. Hawataki kabisa kutumika, na kuchafua mikono yao – lakini wanataka kutumikiwa! Nataka kusema kwamba, hakuna nafasi ya viongozi katika kanisa, ambao wanatenda hivyo. Je, Yesu alisema nini, katika Chumba cha Juu? “*Basi, ikiwa mimi niliye Bwana, na Mwalimu, nimewaosha ninyi miguu, nanyi pia mnapaswa kuoshana miguu*” – mnapaswa kutumikiana kila mmoja.

Hiki ndicho ambacho Petro pia anasema katika **mst 6:** “*Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu uliyohodari*”. Petro anatoa maelekezo ya Yesu Kristo hapa. Na angalia katika **mst 5** pia: “*Ninyi nyote jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana*”. Kwa nini? Petro anatupa jibu mwishoni mwa **mst 5**, na anatumia nukuu kutoka **Mithali 3:34:** “*Mungu huwapinga wenye kiburi, bali huwapa neema wanyenyekevu*”. Kwa maneno mengine, Mungu hawapendi wenye kiburi, bali huwapa neema wale wanaotumika, na wenye unyenyekevu. Wakati wa asubuhi, tunapovaa, huwa tunavaa nguo zetu. Na Petro anasema – unapovaa kwa ajili ya huduma ya kiroho; unapotembea kama mchungaji, vazi unalopaswa kuvaa, ni unyenyekevu. Hapa kuna wazo la kuvutia - na ninafikiri litatusaidia kuelewa kwa nini Petro anasema hivi. Ninafikiri kwamba amekumbushwa kitu fulani, ambacho kilitokea katika Chumba cha Juu. Fungua **Yohana 13:4**. Tunaijua hadithi hii vizuri, kwa sababu tuliangalia mwaka jana. “*Yesu aliondoka kwenye chakula, akavua vazi lake la nje, na akajifunga taulo kiunoni mwake*”.

Katika lugha ya Kigriki, mstari huu unasema kwamba *'alijiweka kwenye taulo ambayo ilivaliwa na mtumwa, au mtumishi'*. Katika siku za Agano Jipya, watu waliovaa taulo, kwa ujumla walikuwa watumishi – na kwa hiyo walikuwa watu wenye hadhi ya chini. Hivi ndivyo alivyofanya Yesu. Alijifanya kuwa mtu mwenye hadhi ya chini. Alijiweka kwenye taulo ya unyenyekevu. Na Petro anasema hapa, katika **1 Petro 5:5**, jifungeni taulo ya unyenyekevu, ili muoneshe kwamba, mko tayari kuwa watu wanaotumikia wengine. Anasema, *'ninyi nyote mnapaswa kufanya ambacho Yesu alifanya. Mnapaswa kujiweka kwenye taulo ya mtumishi'*. Je, unaweza kuona uhusiano kati ya Chumba cha Juu, na mstari huu katika **sura 5**? Na huu ndio ushauri wa Petro kwa wachungaji – *'iweni wachungaji wa kundi; watumikieni kwa hiari, na jifungeni unyenyekevu'*. Kama hutaki kutumika, basi usiwe mchungaji! Kama unataka kuwa mtu mkubwa, basi usiwe mchungaji!

Kuna kitu kingine ambacho Petro anatuonya mwishoni mwa **mst 2**. Kama unataka kuwa mchungaji mzuri, *"msiwe na tamaa ya fedha"*. Kwa huzuni, mambo yanayohusu fedha yanaweza kuwa chanzo kikubwa cha migogoro, katika makanisa mengi ya Kiafrika. Labda hili ni jaribu kubwa sana, kwa viongozi wa kanisa leo. Je, ni mara ngapi tunasikia kwamba pesa zimetumiwa vibaya, kwa sababu watu walio katika madaraka, wamejaribiwa kuiba. Inatokea mara kwa mara. Ngoja tuweke wazi jambo hili; katika baadhi ya makanisa, hapa Tanzania, na ulimwenguni pote, wachungaji huwaibia watu wao. Baadhi yao hukusanya pesa nyingi kupitia sadaka. Wamechukua hizo pesa kwa ajili yao wenyewe, na kuwa matajiri sana. Baadhi yao wamejulikana, na kukamatwa, na kupelekwa mahakamani. Baadhi yao wako gerezani.

Tatizo la pesa, linaweza kuteka moyoni, na kwa hiyo, watu huwa na kiu zaidi ya kupata pesa, katika maisha yao. Katika **1 Timotheo 6:9-10** Paulo anatuonya kuhusu jambo hili. Anasema hivi **. Kama mchungaji, unapaswa kuulinda moyo wako dhidi ya jambo hili. Kuwa makini sana. Katika **1 Timotheo 3:3** mtume Paulo anasema kwamba, *"kiongozi hapaswi kuwa mpenda fedha"*. Mwandishi wa barua kwa **Waebrania**, anasema hivi: *"Msiwe watu wa kupenda fedha; toshekeni na vile vitu mlivyo navyo"* (Waebrania 13:5). Huwezi kuwa mchungaji mzuri, kama ni mpenda pesa. Na Petro anasema katika **sura 5:2** *"Msiwe wapenda fedha, bali muwe na shauku ya kutumika"*.

Lakini pia anasema katika **mst 3**: Msiwe na tamaa ya madaraka. *"Msiwatawale kwa mabavu hao walio wekwa chini ya ulinzi wenu"*. Kwa maneno mengine: msitawale kwa ukatili juu ya wale mnaopaswa kuwalinda. Usiwe kiongozi anayewatisha, na kuwalazimisha watu kufanya mambo. Yesu aliwaonya wanafunzi wake kuhusu hili. Katika **Mathayo 20:25** anasema hivi: *"Mnajua ya kuwa wakuu wamataifa hutawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha - lakini haitakuwa hivyo kwenu"*. Je, Yesu anasema nini? Je, anasema kwamba kiongozi hapaswi kuongoza kwa mamlaka? Hapana, kiongozi ana mamlaka ya kuongoza, lakini kiongozi mzuri hatumii mamlaka yake, kwa kuwanyanyasa watu. Msiwe kama baadhi ya wafalme, au marais, au wanasiasa, au polisi - ambao huchukulia nafasi zao kama fursa. Baadhi yao hujaribu kujipatia fedha na rushwa kutoka kwa watu.

Usiwalazimishwe washirika wa kanisa lako, kufanya unachotaka wafanye. Usiwe kama mtu mkubwa, ambaye anatoa maelekezo ya amri, na kutarajia watu wamtumikie, na kumtii. Mchungaji mzuri ni mtu anayeongoza watu wake, lakini hatumii vibaya mamlaka yake. Na tunapaswa kuwa makini hapa. Tunajua kwamba moyo wa mwanadamu ni wenye dhambi. Jaribu la kutumia vibaya nafasi za uongozi, wakati mwingine linaweza kuwa jambo lenye nguvu sana. Na ndiyo maana wachungaji wanapaswa kuwa waangalifu sana. Hili lilikuwa tatizo kubwa kwa watu wa **Israeli**, katika Agano la Kale. Viongozi wao walikuwa hawawatendei vyema watu. Hawakuwa wakiwalinda, na walikuwa wakiwatumia kama fursa. Na Mungu hakuwa na furaha nao. **Katika Ezeieli 34:2-5** Ezeieli anaelezea jinsi hali ilivyokuwa katika Israeli, miaka **600** iliyopita kabla ya Yesu kuzaliwa. Mungu hapa anazungumza kuhusu wachungaji wa kiroho, ambao wanaongoza Israeli.

Anawaambia makuhani, na manabii; watu ambao walikuwa kama wachungaji. Na kifungu hiki kina waelezea wachungaji wabaya. Ni kifungu cha huzuni – na Mungu hanafuraha na hawa wachungaji. Hawakuwa wakifanya kazi yao vizuri. Na ninasikitika kusema kwamba, kifungu hiki kinawaelezea baadhi ya wachungaji, na wazee wa kanisa leo. Baadhi ya wachungaji hawajali makundi yao, lakini wanahakikisha kwamba wanajijali wenyewe tu! Hawalishi, wala kuimarisha makundi yao. Hawawatafuti waliopotea, na wanawatawala kwa ukatili. Matokeo yake ni kwamba, kundi linatawanyika, na lina kuwa na afya mbaya ya kiroho. Tofauti na hao, kiongozi wa kimungu siyo mbinafsi. Mchungaji mwema huwatafuta walio dhaifu, na kuwatembelea wagonjwa. Anawafunga watu walio pata majeraha ya kiroho, na anatawala kwa upole na neema. Ngoja ni ulize swali tena: Je, wewe ni mchungaji mzuri, au ni mchungaji mbaya? Petro anasema, katika **mst 3**: “*Msiwatawale kwa mabavu hao walio wekwa chini ya ulinzi wenu*”, badala yake, “*muwe mfano kwa hilo kund*”.

Je, unajua kwamba, sehemu mojawapo ya kazi yako, ni kuwa mfano mzuri kwa watu unaowaongoza? Kama mchungaji, watu wanakuangalia kwa makini, na unaweza kuyavutia maisha yao. Na hii ndiyo maana, ninasema kwamba kuwa mchungaji ni wajibu mkubwa sana. Ni wajibu wako kuwa mfano mzuri kwa watu wako. Na kama watu katika kanisa lako wataiga tabia yako njema, hii itamaanisha kwamba wewe umekuwa mchungaji mzuri. **Paulo** mara kwa mara anawaagiza wasomaji wake kumuiga yeye! Katika **1 Wakorintho 4:16** anasema hivi: “*Ninawasihi kuniiga mimi – nawasihi fuateni mfano wangu*”. Pia, katika **1 Wakorintho 11:1** katika toleo la **Habari Njema**, anasema hivi: “*Niigeni mimi, kama nami ninavyomwiga Kristo*”. Unapaswa kuwa na uwezo wa kuwaambia kanisani: “*niangalieni mimi na mwigie tabia yangu; fuateni mfano wangu*”. Sasa shinikizo liko juu yako na mimi! Kama utasema hivi, unapaswa kuhakikisha kwamba, tabia yako ni nzuri. Na njia pekee unayoweza kutumia, ni kujikita mwenyewe katika mfano wa Yesu Kristo. Tambua mpangilio ambao jambo hili linatokea. Paulo anasema: “*Niigeni mimi, kama nami ninavyomwiga Kristo*”. Siyo vizuri kusema kwa watu, “*niigeni mimi*”, kama wewe hufuati mfano wa Yesu. Kama humuigi Yesu katika maisha yako, basi mfano wako kwa wengine utakuwa mbaya. **Mst 3**: “*Msiwatawale kwa mabavu hao waliowekwa chini ya ulinzi wenu*”, lakini, badala yake, “*muwe mfano kwa hilo kund*”.

Je, mfano wetu ni nani? **Mst 4**: Mchungaji mkuu – Yesu Kristo mwenyewe. Sisi ni wachungaji wa kundi. Tumechaguliwa kuwa wachungaji, na kulinda watoto wa Mungu. Lakini bosi wetu, Bwana Yesu Kristo, ni mchungaji mkuu, na yeye ndiye mfano wetu. Kwa kweli, hii ni sehemu pekee katika Agano Jipya, ambapo Yesu anaitwa mchungaji mkuu, ingawa katika **Yohana 10**, Yesu anajitaja mwenyewe kama mchungaji mwema. Pia tunaweza kufuata mfano wa **Baba Mungu** wetu, kwa sababu yeye mwenyewe anajiita ‘*mchungaji*’. Dakika chache zilizopita, tuliwaangalia wachungaji wabaya, katika **Ezekieli 34** – lakini mwishoni mwa kifungu hicho, Mungu anajitaja mwenyewe kama mchungaji. Ngoja nisome anachosema Ezekieli, katika **mst 11-12** **. Na bila shaka, hapa Mungu anazungumza kuhusu kuliokoa watu wa Israeli.

Tunapomalizia kipindi hiki – tafakari kuhusu hili kwa makini. Mungu Mwenyezi anaitwa mchungaji. Yesu Kristo anaitwa mchungaji mwema. Kama wewe ni mchungaji, au mwinjilisti, wewe pia ni mchungaji. Tunajua kwamba Mungu, na Bwana Yesu, wana majina mengi, lakini furahia, kwa sababu unashiriki mojawapo ya majina yao! Huu ni upendeleo ulioje! Tusiwe watu wakupenda fedha. Tusitumie vibaya nafasi zetu za mamlaka. Tuwe watumishi wanyenyekevu. Na tuwe mfano mzuri kwa watu tunao-waongoza. Angalia **mst 4**, kwa sababu tumeambiwa thawabu yetu itakuwa nini, kwa ajili yetu kuwa wachungaji wazuri: “*Na mchungaji mkuu atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka*”.

KIPINDI 11: 1 Petro 5:6-11: *Simameni Imara na Mpingeni Shetani* Steve Lancaster

Hatimaye, tumefika mwisho wa barua hii! Na mchana huu, katika kapindi cha mwisho cha mafundisho, ninataka tulenge juu ya mistari miwili, katika **sura 5**. Ujumbe ni huu: muwe makini na adui yenu Shetani. Mpingeni, na simameni imara. Kwa hiyo, tufungue **1 Petro 5:6-11** **. Tumejifunza katika masomo yetu kwamba tunahitaji kuwa watu wanyenyekevu. Petro anatuagiza kuwa viongozi wanaotumikia. Tunahitaji kuwa viongozi wanao ongesha mfano mzuri, kwa watu wetu. Petro anatuambia kuvaa vazi la unyenyekevu, kama Yesu alivyofanya katika Chumba cha Juu. Na katika **mst 6**, Petro anasema hivyo tena. “*nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari*”. Tunahitaji kuwa weka wengine mbele, na sisi nyuma. Tunapaswa kunyenyekeana sisi kwa sisi, na tunapaswa kuwa wanyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu.

Na katika unyenyekevu wetu, Petro anasema katika **mst 7**, kwamba hatupaswi kuhuzunika. Kwa kweli, badala ya kuhuzunika, tunapaswa kumtwika Bwana huzuni zetu. Kwa nini? Kwa sababu anatumia. Kama mchungaji anavyojali kondoo, Mungu pia anatumia sisi. Kwa hiyo, wakati wowote tunapokutana na magumu, na majaribu, tunapaswa kumtwika huzuni zetu Mchungaji Mkuu; Baba Mungu. Lakini pia, kuna kitu kimoja ambacho tunapaswa kufanya – na hii ni muhimu sana kama tunataka kufanikiwa katika maisha yetu ya Kikristo, na katika huduma zetu. Je, unajua kwamba tukovitani!? Kila mmoja ambaye ni Mkristo anahusika katika vita dhidi ya adui – na adui ni Shetani. Baadhi ya Wakristo wanajua kwamba wako vitani. Wakristo wa kanisa la mwanzo walijua kwamba walikuwa vitani – kwa sababu walikutana na mateso na magumu.

Lakini baadhi ya Wakristo katika kanisa la leo, hawajui hata kwamba wako vitani! Hawafahamu kwamba kuna vita inatokea! Hawafahamu kwamba Shetani anazungukazunguka akiunguruma kama simba. Na kwa sababu hiyo, mara kwa mara, wanakuwa dhaifu, na wanashindwa kwa urahisi Shetani anapowavamia. Je, Petro anasema tunapaswa kufanya nini, tunapopigana vita hivi dhidi ya Shetani? Anatuambia katika **mst 8-9**, kwamba tunapaswa kufanya mambo manne: Jambo la **kwana** - muwe na kiasi. Jambo la **pili** - muwe wenye kukesha. Jambo la **tatu** - mpingeni Shetani. Jambo la **nne** - simameni imara katika imani. Kwa nini Petro anatuagiza kufanya mambo haya? Kwa sababu Shetani yupo, na anatafuta kuwaharibu Wakristo. **Mst 9** unasema kwamba Shetani anatafuta watu awameze! Pamoja na wasaidizi wake, roho wachafu - na pepo wachafu, Shetani anajaribu kuleta shida katika maisha na akili za Wakristo. Anajaribu kuleta matatizo katika kanisa. Anajaribu hata kufanya kazi yako kama mchungaji isiwe hai.

Biblia inasema mengi kuhusu kazi za Shetani. Kadri unavyosoma katika Injili, na kitabu cha **Matendo**, utaona pepo wengi wakifanya kazi. Katika Agano Jipya, kuna zaidi ya mistari **100** inayozungumza juu ya pepo; wafanya kazi wa Shetani. Kila mwandishi anataja pepo, au roho wa chafu, isipokuwa mwandishi wa **Waebrania**. Kila mwandishi katika Agano Jipya. Kwa kweli, kufukuza pepo ilikuwa kazi iliyochukua sehemu kubwa, katika huduma ya Yesu. Baada ya ubatizo wa Yesu, tunajua kwamba Shetani alimjaribu katika jangwa, kwa siku **40**. Majaribu hayo, yalikuwa halisi kabisa – hasa Yesu alipokuwa dhaifu, wakati alipokuwa hajala kwa majuma **6**! Na bado, tunajua kwamba Yesu alipinga majaribu, na akashinda vita dhidi ya Shetani. Alitumia Biblia kumpinga Shetani. Kama asingempinga Shetani, wakati wa majaribu hayo, pasingekuwa na wokovu kwa ajili yetu. Katika Sala ya Bwana, Yesu anamtaja Shetani, kutuonesha kwamba tunahitaji kumpinga kwa maombi. Anawaambia wanafunzi wake kuomba maneno haya: “*usitutiye majaribuni, lakini utuokowe na yule mwovu*”. Kwa maneno mengine, tulinde dhidi ya Shetani. Tunahitaji kuomba kwamba Mungu atulinde dhidi ya yule mwovu.

Mara kwa mara, tunasoma kuhusu kazi ya Shetani katika injili. Na leo, Shetani na wajumbe wake, bado wanafanya kazi. Huwa hafanyi kazi kwa kujifunua kupitia roho wachafu tu. Lakini pia, anafanya kazi katika njia ya kujificha. Huwa anajaribu kazi zake katika maisha yetu. Huwa anajaribu kutujaribu. Huwa anatushitaki, na kutusababisha tuwe na mashaka juu ya wema wa Mungu. Na kama unaangalia huku na huku katika ulimwengu leo, utaona njia ambazo Shetani anatawala na kuwateka watu. Na ingawa Shetani anaweza kuwa katika sehemu moja tu kwa wakati mmoja, ana maelfu ya roho wachafu, ambao hufanya kazi kwa ajili yake, katika jamii zetu, na hata katika serikali zetu. Kwa kweli, Mtume **Yohana** anatuambia kwamba: “*dunia yote iko chini ya yule mwovu*” (1 Yohana 5:19). Lakini, ushauri wa Petro, kwa watu wa Mungu, ni kuwa na kiasi, na kukesha. Tunapaswa kumpinga Shetani, na kusimama imara katika imani.

Utaona katika **mst 8** - Petro anamfananisha Shetani - na simba. Katika tamaduni nyingi, simba mara nyingi ni alama ya nguvu, na ushupavu. Ni mnyama ambaye yuko juu ya wanyama wote. Wanyama wengine wote wanamwogopa simba. Na hata sisi wanadamu tunamwogopa simba! Ni mnyama mkali wa porini. Hapa Tanzania, unaweza kutembelea Hifadhi ya Taifa, na wakati mwingine utaweza kuwaona simba porini. Wakati wa mchana, wanatumia muda mwingi kulala chini, lakini wakati wa usiku, wanafanya kazi, na hapo ndipo wanafanya kazi zao za kuwinda. Simba ni mwindaji mwenye nguvu sana, na anapokamata mawindo yake na kuuu, anaweza kupasua mnyama kwa meno yake. Ni wanyama hatari sana, na wauaji wenye nguvu.

Wakati wa Agano la Kale, simba waliishi katika Israeli. Tunajua hivyo kwa sababu wametajwa katika Biblia. **Yeremia, Ayubu, Zefania** – wote wanamtaja simba. Na tunajua hadithi maarufu ya **Danieli** katika tundu la simba. Danieli alikuwa kiongozi mahili – na alikuwa mtu mwadilifu, lakini adui zake walitaka afe. Walimshawishi mfalme atengeneze sheria mpya – ili kwamba iwe kosa kuomba kwa miungu mingine, isopokuwa kwa mfalme peke yake. Walijua kwamba Danieli alikuwa amejitoa kwa Mwenyezi Mungu. Na tunafahamu hadithi yote. Danieli alitupwa katika tundu la simba, lakini Mungu alifanya miujiza akafunga midomo ya simba, na Danieli akawa salama. Kwa namna tuliyokuwa tunaangalia asubuhi hii, tuliangalia somo la kutii serikali - na hili ni mojawapo ya matukio ambapo ilikuwa haki kwa Danieli asimtii mfalme. Amri ya mfalme ilikuwa kinyume na amri ya Mungu – na kwa hiyo Danieli alichagua kumtii Mungu badala ya mfalme, ingawa alijua kwamba anaweza kufa. Je, nini kilitokea kwa washitaki wa Danieli? Sikiliza hii, kwa sababu inakupa picha jinsi simba alivyomkali. **Danieli 6:24**: “*mfalme akaamuru, nao wakawaleta wale watu waliomshitaki Danieli, wakawatupa katika tundu la simba, na wale simba wakawashinda wakaivunja mifupa yao vipande vipande, kabla hawajafika chini ya tundu*”. Hivyo ndivyo simba walivyo na nguvu. Kwa jinsi ile ile, Petro anasema, Shetani ni kama simba mwenye nguvu, akitafuta mtu ammeze; akitafuta kuharibu maisha. Huu ndio mpango wake.

Pia tunajua kwamba simba waliishi katika Israeli wakati wa **Daudi**, kwa sababu amewataja mara nyingi. Kama mchungaji, aliwalinda kondoo dhidi ya simba, na dubu. Na tumeambiwa katika Samweli ya kwanza (17:35) kwamba katika matukio mengi, ambapo simba alikuwa amevamia kondoo, na kukamata mmoja wa kondoo katika mdomo wake, Daudi alimfukuza, na kumuua! Alikuwa mchungaji jasiri sana! Na labda, kuna somo kwetu hapa kama wachungaji. Ni kazi yako, na wajibu wako, kuwajali kondoo wako. Je, huwa unafanya nini simba anapokuja na kuchukua mmoja wa kondoo wako? Je, huwa unakaa na kutazama, na bila kufanya chochote – au huwa unajaribu kuokoa kondoo aliyekamatwa? Kwa hakika, sizungumzi kuhusu simba halisi anayekuja katika kanisa lako! Lakini Shetani akizungukazunguka akinguruma kama simba, na kujaribu kuharibu Wakristo.

Anaweza kufanya hivyo kupitia magonjwa, au mateso, au kupitia majaribu ya aina nyingi. Shetani anaweza kutuma walimu wa uongo katika kanisa lako; mtu ambaye anajaribu kuiba kondoo zako kwa mafundisho ya uongo. Je, huwa unafanya nini kuhusu hili? Kama mchungaji, je - huwa unatumia bidii zako kuwalinda kondoo zako, dhidi ya simba anaye zungukazunguka katika kanisa lako? Je, huwa unaomba kwamba kondoo zako watalindwa dhidi ya adui? Hii ni mojawapo ya kazi zako. Ingawa yaweza kuwa Daudi alimwogopa simba, lakini bado, alimkimbiza, na kuwalinda kondoo zake. Alikuwa na uzoefu mwingi wa kupambana na simba.

Kila tunaposoma kuhusu tabia ya simba katika Biblia, na kila tunapokumbuka kuhusu walivyo wakali na hatari, tunahitaji kukumbuka, kwamba hii ni picha ya Shetani, na tabia yake. Pia simba wanajulikana kuwa wajanja na welevu wanapowinda mawindo yao. Hii ni hadithi maarufu ya simba wa wili, ambao waliua, na kuwavamia wafanya kazi wengi, katika mkoa wa **Tsavo**, huko Kenya. Kwa kiasi fulani, ingawa wawindaje walijaribu kuwakamata, waliweza kuepuka wasiuawe kwa miezi **9**. Huko nyuma mwaka **1898**, serikali ya Uingereza ilikuwa inajenga reli kutoka Mombasa hadi Uganda. Maelfu ya wafanya kazi wa kihindi walitumiwa kujenga tawi la reli, ambalo lilipita kwenye pori la Kenya. Lakini kulikuwa na tatizo kubwa. Simba wa wili walikuwa wakivamia wafanya kazi hao, wakati wa mchana na usiku. Yapata wanaume **30** waliuawa nakumezwa na hawa simba. Baadhi ya watu wanasema kwamba zaidi ya watu **100** waliuawa na simba hawa. Watu walijaribu kujilinda wenyewe. Walijenga boma kuzunguka hema lao wakati wa usiku; waliweka mitego, na kuwasha moto kuzuia simba wasije, lakini haijalishi walichofanya, simba kwa namna moja, walikuwa bado wanavamia. Walikuwa wajanja na waelevu, na walikwepa kunaswa na mitego kwa muda wa miezi **9**.

Wafanya kazi wengi waliacha kazi zao, na kurudi nyumbani. Walikuwa wameogopa sana kuendelea na kazi. Hofu ilienea katika kambi, na kazi katika tawi la reli ilisimama, kwa sababu simba walikuwa wanakula watu wa Tsavo. Hatimaye, simba waliuawa na kazi ikaendelea. Na hii ni picha ya kile ambacho kinaweza kutokea kwa kanisa. Shetani ni mjanja na mwelevu. Anaunguruma kama simba akitafuta windo lake, na kutafuta kuua chakula chake. Wakati mwingine huvamia kanisa, na wakati mwingine anavamia wachungaji kupitia mateso na mambo magumu. Shetani anataka uanguke. Anataka ushindwe katika huduma yako, na atajaribu kufanya hivi kwa kukujaribu ufanye vitu kinyume na Neno la Mungu. Sote tumewahi kusikia kuhusu wachungaji na maaskofu, ambao wameanguka katika majaribu, kwa pesa, na mambo ya uzinzi, na kila kitu kikaharibika. Huduma zao na makanisa yao yakaanguka. Hivi ndivyo Shetani anavyofanya kazi. Hivi ni kama vile kazi ya ujenzi wa reli ilivyo simama, Shetani anajaribu kusimamisha kazi ya kanisa.

Hivyo basi – tunapaswa kufanya nini? Angalia **mst 8**. *Muwe na kiasi, na kukesha*. Kwa maneno mengine, msilale kiroho! Muwe macho na uvamizi wake. Jihadharini. Labda, Petro alipoandika maneno haya, alikuwa akifikiri kuhusu tukio, ambapo hakuwa imara na macho. Je, unakumbuka kilichotokea katika Bustani ya Gethsemane? Yesu aliwachukua Petro, Yakobo, na Yohana, na akawaambia: *“roho yangu imezidiwa na huzuni nyingi. Kaeni hapa na muwe macho pamoja nami”*. Na kisha Yesu akaenda mbele ndani ya bustani, na akaomba kwa uchungu kwa Baba yake. Kama saa moja hivi baadaye, Yesu akarudi walipokuwa. Je, aliwakuta imara na wenye kujilinda? Hapana, aliwakuta wamelala! Yesu alikuwa amewapa amri. Alikuwa amewaagiza kuwa macho – lakini walikuwa wamelala. Akawaambia hivi katika **Mathayo 26:41**: *“Kesheni na kusali ili msije mkaingia katika majaribu. Roho inataka, lakini mwili ni dhaifu”*. Baada ya kuomba tena, Yesu alirudi na kuwakuta wamelala tena. Na baada ya kuomba tena, alirudi mara ya tatu, na kuwakuta bado wamelala. Yesu akawaambia: *“bado mmelala”*?

Yesu alikuwa amewaambia kukaa macho, na kusimama imara – lakini hawakuweza. Walikuwa wameshindwa kufanya alichokuwa amewaambia. Hawakukaa macho na hawakuwa na kiasi. Na matokeo yake, Petro hakuwa tayari kwa vita iliyokuwa mbele. Yesu alijua kilichokuwa kinakuja, lakini Petro hakujua. Yesu alijua kwamba Shetani angemjaribu Petro katika saa chache zijazo – labda hiyo ndio maana Yesu aliwaambia kukesha na kuomba, ili kwamba asije akaingia majaribuni. Lakini, saa chache tu baadaye, wakati Petro alipokuwa amekaa kuzunguka moto katika uwanja wa Kuhani Mkuu, hakuwa amejiandaa dhidi ya mpango wa Shetani. Hayuko tayari kwa vita. Hayuko imara katika imani yake. Hawezi kupinga jaribu la kumkana Yesu. Aliulizwa mara tatu kama alikuwa mwanafunzi wa Yesu. Je, alisema nini katika jibu lake? “*Mimi sijui unachosema; mimi hata simjui huyu mtu*”. Jaribu hili la kumkana Yesu, lilikuwa na nguvu sana, kwa sababu Petro alikuwa ameogopa watu wangepanya nini, kama wangepua kwamba alikuwa mwanafunzi wa Yesu. Lakini tambua - wawili miongoni mwa watu walio muuliza swali hili, walikuwa wasichana. Hawakuwa watu wenye nguvu kwamba wangeweza kupigana naye na kumuua!

Mmoja alikuwa msichana mtumishi. Unaweza kufikiri kwamba Petro asingeweza kumuogopa msichana mtumishi mdogo – lakini alimwogopa! Je, unakumbuka Petro alikuwa amesema nini kwa Yesu, saa chache kabla? “*Niko tayari kwenda gerezani pamoja nawe. Niko tayari kufa pamoja nawe. Hata kama wengine watakuacha, sitakuacha*” (Mathayo 26:33 & Marko 22:33). Lakini, alipoulizwa na msichana mtumishi kama alikuwa mwanafunzi wa Yesu, alimwambia kwamba, hata sijui unaongea kuhusu nani! Kumbe! Dakika chache zilizopita, nilisema kwamba, Shetani mara nyingi ni mwerevu. Anatomia mbinu nyingi kudanganya watu. Haikuonekana kama simba alikuwa mbele ya Petro wakati alipokuwa amekaa kuzunguka moto. Ilikuwa kama msichana mtumishi mdogo! Lakini bado alilemewa na hofu. Hakuwa na nguvu za kuweza kupinga jaribu.

Petro – uwe macho na uombe. Kesheni na kusali - uwe na kiasi. Hakikisha kwamba umejilinda mwenyewe, na kwamba uko tayari dhidi ya uvamizi wa Shetani. Ujihadhari naye, kwa kuwa atakuja katika namna nyingi, ili akujaribu na kukuangusha. Na huu ni ujumbe kwetu leo. Kadri tunavyotumia muda mwingi katika maombi, na katika Biblia zetu, ndivyo tutakavyo kuwa imara katika kumpinga simba aungurumaye. Hebu tusimame imara kiroho. Hebu tusilale kiroho, lakini tuhakikishe kwamba tuko tayari dhidi ya uvamizi wa Shetani - ili kwamba Shetani anapotuvamia, tusishangae, lakini tuwe tayari kupigana katika jina la Yesu.

Kwa kweli, nini anatuambia Petro katika **mst 9**? “*Tunapaswa kumpinga Shetani, na kusimama imara katika imani yetu*”. Na neno ‘*mpingeni*’ linamaana kwamba tunahitaji kumkabili Shetani. Tunahitaji kumpinga, yeye na mpango wake. Hatupaswi kuingiwa na woga; tunapaswa kupigana dhidi yake. Na ndio maana nilisema mwanzoni, tunahusika katika vita. Tuko katika mapambano, na tunapaswa kumpinga. Tunapaswa kumkabili, siyo kwa nguvu zetu, lakini katika jina la Yesu Kristo. Mkristo hapaswi kumwogopa Shetani – bali kumpinga. Wote tunajua woga ni nini – na wote tunajua kwamba inamaana ya kuogopa, kama Petro alivyoogopa alipokabiliwa na msichana mtumishi.

Na kumbuka tukio moja nilipotembelea **Afrika ya Kusini**, miaka **20** iliyopita. Nilikuwa ninatembelea mbuga ya wanyama, kama Mikumi au Serengeti. Na tulipiga kambi katika mojawapo ya hifadhi za taifa, na tulikuwa tumelala katika hema. Na unapokuwa umelala porini wakati wa usiku, unaweza kusikia sauti nyingi! Na nilipokuwa nimelala katika hema langu, ghafla kulikuwa na sauti ya simba akinguruma. Sijui ilikuwa umbali gani, lakini najua kwamba mungurumo wa simba, unaweza kusikika kutoka umbali wa kilometa nyingi. Inawezekana haikuwa karibu sana, lakini ilisikika kama ni karibu sana. Lakini nakumbuka nilivyokuwa najisikia kuogopa sana. Nililala mle kwenye hema langu, kwa kutulia sana.

Sikutaka kujongea! Niliendelea kufikiri, vipi huyu simba akija kwenye hema langu, ninahitaji kukaa kimya - kwa hiyo nilikaa kimya sana! Na sikulala usiku mzima. Hofu ilikuwa imeniingia, niliposikia sauti ya simba akinguruma! Wakati mwingine, Shetani anaweza kudhihakiki, na kujaribu kutufanya tumwogope. Anaweza kuunguruma kama simba ili atutishe. Anaweza kufanya mambo ya kutufanya tuhuzinike. Anataka tumwogope. Lakini - Petro anasema: hatupaswi kumwogopa Shetani. Tunapaswa kumpinga katika jina la Yesu. Tunapaswa kumkabili.

Tambua **mst 9** unasema kwamba tunapompinga Shetani, tunapaswa '*kusimama imara katika imani yetu*'. Imani katika nini? Imani katika sisi wenyewe? Imani katika nguvu, na uwezo wetu? Hapana. Tunapaswa kusimama imara katika imani yetu katika Kristo Yesu. Kumbuka, tayari yeye ameshinda vita dhidi ya Shetani. Yesu amemshinda Shetani kupitia kifo chake msalabani, na nguvu za Shetani zimezuiliwa. Tunajua kitakachotokea kwake wakati wa mwisho – hawezi kukwepa mwisho wake. Tunajua mwisho wa hadithi. Hii ndio maana hatupaswi kumwogopa Shetani. **Ufunuo 21** inatuambia nini kitatokea kwa Shetani siku ya mwisho. Na kwa sababu hii, tunaweza kusimama imara katika Kristo, tukijua kwamba Shetani hawezi kugusa urithi wetu wa kiroho. Kwa sababu ya imani yetu katika Kristo, tunaweza kuwa na uhakika kwamba, Mungu ataingilia kati, na kutupa ushindi, kadri tunavyosimama na kumpinga Shetani. Katika Kristo, tunaweza kumshinda Shetani.

Fungua **Waefeso 6:10** – kwa sababu hapa ndipo **Paulo** anatuambia jinsi ya kumpinga Shetani. Anatuagiza kuvaa silaha zetu za kiroho. Anatuagiza kujiandaa kwa vita dhidi majeshi ya kiroho ya Shetani. Paulo anataka tujue kwamba kuna vita halisi ya kiroho, ambayo inayaendelea – na anatuagiza tusimame tumpinge Shetani. **Waefeso 6:10** unasema hivi: "*Iweni na nguvu katika Bwana, na iweni na nguvu katika uweza wake*". Tambua, hatuwezi kufanya hivyo kwa nguvu zetu. Tunapaswa kutegemea nguvu za Bwana. **Mst 11** unasema hivi: "*Vaeni silaha za Mungu ili mweze kumpinga Shetani*". Na kisha anataja – mshipi wa kweli, dirii ya haki, ngao ya imani, chapeo ya wokuvu, na upanga wa Roho. Hatuna muda wa kutosha kuangalia mambo haya kwa undani, lakini mistari hii inatuonesha, jinsi tunavyopaswa kusimama nakumpinga Shetani.

Unaweza kugundua kwamba, Paulo pia anatumia neno '*kusimama*' katika **mst 13&14**. Kama ni askari, huwezi kupigana vita yako ukiwa umekaa chini! Unapaswa kusimama ili upigane. Na hivi ndivyo tunavyotakiwa kufanya kama Wakristo; siyo kimwili, bali kiroho. Tunapaswa kusimama katika Kristo. Kwa kweli, Paulo anatuambia katika **mst 15** kwamba, tunapaswa kuvaa viatu vinavyofaa wakati tunapokuwa katika vita na Shetani. Anasema kuhusu kuwekewa "*miguu yenye utayari itupasayo kwa injili ya imani*". Wasomi wengi wa Biblia wanafikiri kwamba, Paulo alipoandika barua hii, alikuwa gerezani, na inawezekana, alikuwa amefungwa na askari wa Roma.

Alipoandika kuhusu silaha za kiroho, anaangalia silaha alizovaa askari; kofia, dirii, upanga, ngao, na viatu maalumu ambavyo askari wa Roma walivaa. Vilikuwa viatu vya wazi, lakini kwa chini vilikuwa na vitu kama misumari. Na hivi vilitengenezwa kwa ajili ya askari, kwa ajili ya vita – misumari hiyo ingeweza kushika vizuri chini na kuzuia askari asiteleze. Kupigana, katika siku hizo, ilikuwa ana kwa ana, na kwa hiyo aina ya viatu hivyo, viliweza kumsaidia askari wa Roma asimame chini, bila kusukumwa kwa kurudi nyuma. Na kwa jinsi ile ile, mtu anaposimama juu ya Yesu Kristo, anaweza kusimama imara wakati anapopigana dhidi ya Shetani. Wanahitaji kusimama imara. Muhubiri maarufu, **John Stott**, alisema hivi: "*Wakristo wasio simama – na hawajasimama imara katika Kristo, wanawindwa kiurahisi na Shetani. Wakristo wanaoyumba kama matete hawawezi kumpinga Shetani wakati anapoanza kuvamia*". Nina swali. Je, umesimama imara katika Kristo? Je, umevaa viatu sahihi? Paulo anataka kuona Wakristo waliyosimama imara katika Kristo.

Anataka kuhakikisha kwamba hawamkimbii Shetani kwa hofu, bali wanasimama imara, na kumkabili Shetani.

Nilipokuwa nikiandaa ujumbe huu, nilisoma jarida kuhusu kwenda kutembea porini. Kichwa kilisema hivi: Unachopaswa kufanya unapokuwa porini, ni kukutana ni simba uso kwa uso! Sasa, sijawahi kukutana na hali hii – wala sitaki kuwa katika hali hii! Lakini huu ulikuwa ushauri wa mwandishi: Usi-babaike; kaa mtulivu. Kumbe! Nafikiri ingekuwa vigumu kuacha kubabaika, kama ungeona simba anakuja kwako! Kisha anasema, simba anaweza kuunguruma – na hii inaweza kutisha sana, lakini jaribu kukaa mtulivu. Kama utababaika itasababisha mambo yahaaribike. Na kisha, mwandishi anasema hivi: Usikimbie – bali **simama**. Ingawa unaweza kuwa ndogo, mwonyeshe simba kwamba wewe ni tishio kwake. Piga makofi, piga kelele, na pungua mikono yako. Hakikisha haukimbii, lasivyo simba hakika atakukimbiza. Simama tu! Na anasema, kama utafanya hivi, labda - unaweza kupona! Labda tunahitaji kwenda kwenye hifadhi ya taifa na tuone kama hii inafanya kazi!

Lakini ninafikiri kwamba hadithi hii inatupa ushauri mzuri, wakati tunapomkabili simba ambaye ni Shetani. Na hiki ndicho anachosema Petro, katika mistari ambayo tumekuwa tukiangalia. Kupitia magumu, kupitia mateso, kupitia majaribu – Shetani anaweza kutafuta kutuvamia, kama simba anavyoinguruma. Wakati anapovamia, tunapaswa kuwa na utulivu, hatupaswi kubabaika, tunapaswa kuwa na kiasi. Hatupaswi kumkimbia Shetani kwa hofu, bali tumpinge, na kusimama imara katika imani yetu. Je, tunawezaje kufanya hili? Kwa maombi. Kwa sifa na kuabudu. Kupitia kujifunza Neno la Mungu. Kwa msaada wa waumini wengine. Tunafanya haya kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, ambaye anakaa ndani yetu, na tunafanya hivi kadri tunavyotaka kuishi maisha matakatifu, katika huduma ya Mungu.

Wakati mwingine tunaweza hata kuhitaji kupiga kelele kwa nguvu, na kumkemea Shetani, kama atataka kutujaribu. Wakati mwingine tunahitaji kuingia katika vita vya kiroho, kwa kuamuru pepo kuachia maisha ya mtu fulani. Tunahitaji kusimama, na kupigana kwa maombi kwa niaba ya wengine, ambao wametekwa na Shetani. Je, Petro alisema nini? *Muwe na kiasi. Kesheni. Mpingeni Shetani. Simameni imara katika imani.*

Mst 10 unasema hivi: *“Na Mungu wa neema yote, aliyewaita katika utukufu wake wa milele katika Kristo, baada ya kuteswa kwa muda kidogo, yeye mwenyewe atawathibitisha, na kuwapa nguvu, na kuwafanya imara. Uweza una yeye milele hata milele, amina”*.
